



TAASISI YA UHAMASISHAJI UWAZI NA UWAJIBIKAJI KATIKA RASILIMALI ZA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA

RIPOTI YA TISA

KWA KIPINDI CHA JULAI 1 2016 MPAKA JUNI 30
2017

JUNI 2020



YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI	III
ORODHA YA VIELELEZO	V
SHUKRANI.....	VI
MUHTASARI	VII
1 UTANGULIZI.....	1
1.1 MAELEZO YA AWALI	1
1.2 MADHUMUNI	1
1.3 TARATIBU ZILIZOFUATWA KATIKA UTEKELEZAJI WA KAZI	1
2 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA KUANDAA RIPOTI.....	3
2.1 UTAFITI KUBAINI WIGO WA ULINGANISHI.....	3
2.2 UKUSANYAJI WA TAARIFA	4
2.3 ULINGANISHI NA UCHUNGUZI WA TOFAUTI.....	5
2.4 USAHIHI NA KUAMINIKA KWA TAARIFA ZILIZORIPOTIWA	6
2.4.1 Uwasilishaji wa Taarifa	6
2.4.2 Uthibitisho wa Taarifa.....	7
2.5 REKODI ZA UHASIBU	9
2.5.1 Kampuni za Madini, Mafuta Na Gesi Asilia.....	9
2.5.2 Taasisi wa Serikali.....	10
3 HALI YA SEKTA YA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA.....	11
3.1 TAARIFA MUHIMU ZA SEKTA YA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA.....	11
3.1.1 Sekta ya Madini	11
3.1.2 Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.....	13
3.2 MFUMO WA SHERIA NA UDHBIBITI KATIKA SEKTA YA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA.....	14
3.2.1 Sekta ya Madini	14
3.2.2 Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.....	18
3.3 MFUMO WA UTAWALA WA KODI NA MALIPO.....	23
3.3.1 Sekta ya Madini	23
3.4 MCHANGO WA SEKTA YA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA KWENYE UCHUMI.....	26
3.4.1 Mchango wa Sekta Kwenye Pato la Taifa	26
3.4.2 Mchango wa Sekta Kwenye Ajira	27
3.5 UZALISHAJI NA UUZAJI WA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA NJE.....	27
3.5.1 Uzalishaji na Uuzaji wa Madini Nje	27
3.5.2 Uzalishaji na Uuzaji wa Mafuta na Gesi Asilia Nje.....	29
3.6 MASHIRIKA YANAYOMILIKIWA NA SERIKALI	30
3.6.1 Shirika la Taifa la Madini	30
3.6.2 Shirika la Taifa la Maendeleo.....	35
3.6.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	36
3.7 UKUSANYAJI NA USAMBAZAJI WA MAPATO YATOKANAYO SHUGHULI ZA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA	41
3.7.1 Mchakato wa Bajeti	41
3.7.2 Ukusanyaji wa Mapato.....	43
3.7.3 Mgawanyiko wa Mapato.....	45
3.8 LESENI ZA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA	46
3.8.1 Utoaji wa Leseni.....	46
3.8.2 Utoaji wa Leseni za Mafuta	51

3.9	UWAZI KATIKA MIKATABA YA SEKTA YA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA	55
3.10	TARATIBU ZA UKAGUZI NA UHAKIKISHO	56
3.10.1	Makampuni ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia	56
•	Taasisi za Serikali	56
4	UAMUZI WA WIGO WA ULINGANISHI.....	58
4.1	AINA ZA MAPATO	58
4.1.1	Wizara ya Madini	58
4.1.2	Mamlaka ya Mapato Tanzania	58
4.1.3	Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	59
4.1.4	Mamlaka za Serikali za Mitaa	59
4.1.5	Wizara ya Fedha na Mipango	59
4.1.6	Wizara ya Maliasili na Utalii.....	60
4.1.7	Malipo ya Kijamii na Mengineyo	60
4.1.8	Mchango wa Serikali katika Uzalishaji na Mapato yasiyo ya Kifedha.....	60
4.1.9	Taratibu za Kubadilishana Bidhaa kwa Bidhaa	61
4.1.10	Malipo Mengine Makubwa	61
4.1.11	Aina ya Mapato yaliyoingizwa katika Ulinganishi	61
4.2	MAKAMPUNI YA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA	61
4.3	WIGO WA ULINGANISHI.....	63
4.4	KIWANGO CHA MGAWANYIKO KATIKA KWASILISHA TAARIFA	70
4.5	KIWANGO CHA UKOMO WA ULINGANISHI.....	70
4.6	WAMILIKI WANUFAIKA WA KAMPUNI	70
5	MATOKEO YA ULINGANISHI	72
5.1	ULINGANISHI WA MALIPO YA MAKAMPUNI NA MAPATO KATIKA TAASISI ZA SERIKALI	72
5.1.1	Ulinganishi kwa Kampuni	72
5.1.2	Ulinganishi kwa Aina ya Malipo	74
5.2	TOFAUTI ZA MALIPO NA MAPATO ZILISALIA	75
6	UCHAMBUZI WA TAARIFA ZILIZOWASILISHWA	77
6.1	UCHAMBUZI WA MAPATO YA SERIKALI.....	77
6.1.1	Uchambuzi wa Malipo ya Makampuni	77
6.1.2	Uchambuzi wa Aina ya Malipo.....	78
6.1.3	Mapato yaliyoripotiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	79
6.2	UCHAMBUZI WA MALIPO KWA SEKTA	79
6.2.1	Sekta ya Madini	79
6.2.2	Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia	80
6.3	MALIPO KWA JAMII.....	81
6.4	MALIPO AMBAYO HAYAKUINGIZWA KWENYE ZOEZI LA ULINGANISHAJI	81
6.5	TAARIFA ZA AJIRA	82
6.6	TAARIFA ZA UZALISHAJI.....	83
6.7	TAARIFA ZA MAUZO YA NDANI NA NJE	83
6.8	MANUNUZI YA BIDHAANNA HODUMA ZA KITANZANIA.....	84
7	MAPENDEKEZO.....	85
7.1	MAPENDEKEZO YATOKANAYO NAULINGANISHAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17	85
7.2	UFUATILIAJI WA MAPENDEKEZO YA RIPOTI ILYIOPITA.....	86
7.3	MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA EITI TANZANIA.....	88
7.4	UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA KATIKA RIPOTI YA TEITI YA 2015/16	90
	VIAMBATISHO	92

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Uthibitisho wa Fomu za Kutolea Taarifa	7
Jedwali Na. 2: Uthibitisho wa Fomu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa	9
Jedwali Na. 3: Aina Kuu na Kiasi cha Madini Yanayopatikana Tanzania	11
Jedwali Na. 4: Aina za Malipo katika Sekta ya Madini	23
Jedwali Na. 5: Aina za Malipo Kwenye Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia	24
Jedwali Na. 6: Mchango wa Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia Katika Pato la Taifa....	26
Jedwali Na. 7: Pato la Taifa kwa Sekta (kwa Bei ya Sasa)	27
Jedwali Na. 8: Uzalishaji wa Madini katika Mwaka wa Fedha 2016/17	27
Jedwali Na. 9: Uuzaji wa Madini Nje	28
Jedwali Na. 10: Miradi Mikubwa Iliyouza Madini Nje 2016/2017	29
Jedwali Na. 11: Uzalishaji wa Gesi Asilia.....	30
Jedwali Na. 12: Ushiriki wa Shirika la Taifa la Madini Kwenye Shughuli za Madini.....	33
Jedwali Na. 13: Miradi ya Shirika la Taifa la Maendeleo kwenye Sekta ya Madini.....	35
Jedwali Na. 14: Ushiriki wa Shirika la Taifa la Maendeleo kwenye Miradi ya Madini	36
Jedwali Na. 15: Maelezo ya Miradi ya Gesi Asilia ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	37
Jedwali Na. 16: Ushiriki wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania Kwenye Shughuli za Mafuta na Gesi Asilia	39
Jedwali Na. 17: Aina za Leseni za Madini.....	46
Jedwali Na. 18: Leseni za Kushughulika na Madini	47
Jedwali Na. 19: Mahitaji na Vigezo vya Kutoa Leseni za Madini	48
Jedwali Na. 20: Leseni za Madini Zilizotolewa Mwaka 2016/17	48
Jedwali Na. 21: Vigezo vya Kuhamisha Umiliki wa Leseni za Madini	49
Jedwali Na. 22: Leseni za Madini Zilizohamishwa Mwaka 2016/17	49
Jedwali Na. 23: Aina za Leseni za Mafuta na Gesi	51
Jedwali Na. 24: Vigezo na Utaratibu wa Utoaji Leseni za Mafuta na Gesi Asilia	53
Jedwali Na. 25: Aina ya Ada na Malipo yanayolipwa kwa Wizara ya Madini.....	58
Jedwali Na. 26: Aina ya Kodi na Ada zilizolipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania	58
Jedwali Na. 27: Aina ya Ada zilizolipwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	59
Jedwali Na. 28: Mtiririko wa Mapato kwa Zoezi la Ulinganishaji	61
Jedwali Na. 29: Malipo yaliyofanywa na Makampuni.....	61
Jedwali Na. 30: Kampuni zilizoingia kwenye Ulinganishi 2016/2017	62
Jedwali Na. 31:Maelezo ya Mtiririko wa Kodi na Malipo kwa Serikali.....	64
Jedwali Na. 32: Kampuni zilizoingia katika zoezi la Ulinganishaji	65
Jedwali Na. 33: Mashirika Yanayomilikiwa na Serikali	66
Jedwali Na. 34: Taasisi za Serikali.....	66
Jedwali Na. 35: Kampuni zilizorejesha Fomu kwa Mwaka 2016/2017 (TZS Milioni)	67
Jedwali Na. 36: Kampuni ambazo hazikushiriki katika Ulinganishaji 2016/17	68
Jedwali Na. 37: Kampuni ambazo hazikuwasilisha Taarifa Mwaka wa Fedha 2016/17	69
Jedwali Na. 38: Taarifa za Makampuni na Wanufaika wake.....	70
Jedwali Na. 39: Twakimu za Ujumla za Makampuni ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia	72
Jedwali Na. 40: Twakimu za Malipo kulingana na Aina ya Malipo.....	74
Jedwali Na. 41: Tofauti za Malipo na Mapato Zilizosalia	75
Jedwali Na. 42: Mapato ya Serikali	77
Jedwali Na. 43: Orodha ya Malipo	78
Jedwali Na. 44: Mapato yaliyori potiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	79
Jedwali Na. 45: Kampuni za Madini.....	79
Jedwali Na. 46: Kampuni za Mafuta na Gesi Asilia	80
Jedwali Na. 47: Malipo kwa Jamii	81
Jedwali Na. 48: Malipo ambayo hayakulinganishwa	81
Jedwali Na. 49: Aina ya Malipo ambayo hayakulinganishwa	82

Jedwali Na. 50: Twakimu za Ajira	82
Jedwali Na. 51: Kiasi cha Uzalishaji kwa Kampuni	83
Jedwali Na. 52: Mauzo ya Dhahabu	83
Jedwali Na. 53: Mauzo ya Almasi Ghafi	83
Jedwali Na. 54: Mauzo ya Fedha	83
Jedwali Na. 55: Mauzo ya Gesi Asilia.....	84
Jedwali Na. 56: Manunuzi ya Bidhaa na Huduma kutoka Makampuni ya Kitanzania.....	84
Jedwali Na. 57: Ufutiliaji wa Mapendekezo ya Ripoti iliyopita	87

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1: Mtiririko wa Malipo ya Ukusanyaji wa Mapato ya Madini, mafuta na gesi asilia	45
Kielelezo Na. 2: Asilimia ya Mapato ya Serikali kutoka katika Taasisi za Serikali	78
Kielelezo Na. 3: Mchango wa Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwenye pato la Serikali.....	81

SHUKRANI

Chuo Kikuu Mzumbe, ambaye ndiye Mlinganishi huru katika uandaaji wa ripoti hii, anatoa shukrani za dhati kwa taasisi mbali mbali na watu binafsi ambao walichangia kufanikisha kuandaa na hatimaye kuchapisha ripoti hii. Kwanza, tunaishukuru Kamati ya TEITI, wajumbe wa Kamati Ndogo ya TEITI, na Sekretarieti ya TEITI kwa msaada waliota kwa Mlinganishi huru. Tunashukuru kwa mawazo mazuri na mwongozo tuliopeka kutoka kwa Bi. Ines Marques na Bi. Lyydia Kilpi wakati tunandaa ripoti hii.

Mwisho, tunatambua ushirikiano tulipopata kutoka kwa taasisi za serikali na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia wakati wa ukusanyaji wa taarifa na katika awamu mbalimbali za mchakato wa ulinganishi. Kwa taasisi za serikali tunapenda kuwatambua wafuatao; Wizara ya Madini, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Utumishi wa Umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Shirika la Madini la Serikali, Mamlaka ya Usajili wa Biashara na Leseni, na Tume ya Madini.

MUHTASARI

Hii ni ripoti ya 9 ya TEITI inayowasilisha ulinganishi wa malipo na mapato yaliyori potiwa na makampuni na taasisi za serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17. Zoezi la ulinganishi lilihusisha kampuni za madini, mafuta na gesi asilia ambazo zilifikia kiwango cha wigo wa malipo kama ilivyoidhinishwa na Kamati ya TEITI. Kama inavyotakiwa na viwango vya EITI, makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia yamayomilikiwa na serikali yanahitajika pia kuripoti malipo yake kwa serikali hata kama hayajaingia kwenye wigo wa ulinganishi. Katika zoezi hili, makampuni ya serikali yaliyohusishwa ni Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Shirika la Madini la Serikali na Kampuni ya STAMIGOLD.

Mchango wa Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia Katika Uchumi

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, mchango wa sekta ya madini, mafuta na gesi asilia kwa pato la taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulikuwa 4.8%. Mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa haujabadilika ikilinganishwa na mwaka wa fedha wa 2015/2016.

Kwa mujibu wa Utafiti wa mwisho uliofanya na Ofisi ya Taifa ya Takwimu inayohusu Ajira na Kipato, sekta ya madini, mafuta na gesi asilia iliajiri watu wapatao 35,900 (ajira za kawaida na vibarua) ambayo ni sawa na asilimia 1.4 ya wafanyakazi katika sekta zote nchini. Viwango vya ajira katika sekta hii vimeonesha ukuaji mdogo ikilinganishwa na mwaka 2015, ambapo jumla ya ajira zilikuwa 30,259 ambayo ni sawa na asilimia 1.3 ya jumla ya ajira katika sekta zote nchini.

Uzalishaji wa Uuzaji wa Madini Nje

Kwa mujibu wa Tume ya Madini, uzalishaji wa madini katika mwaka wa fedha 2016/17 ulikuwa na thamani ya TZS 4.78 trilioni. Uzalishaji wa dhahabu uliongoza kwa jumla ya thamani ikilinganishwa na madini mengine kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini.

Aina ya Madini	Kipimo	Bei kwa Kipimo	Jumla (Uzito)	Thamani (TZS)
Dhababu	Kilo	73,502,684.91	43,759.99	3,216,476,759,838.89
Almasi	Kilo	549,278.63	249,911.05	137,270,798,016.00
Fedha	Karati	1,275,427.85	14,767.64	18,835,053,622.27
Shaba	Ratili	5,231.25	10,395,693.40	54,382,519,484.83
Mawe Chokaa	Tani	116,892.51	4,004,241.73	468,065,849,169.00
Chumvi	Tani	97,535.73	148,637.80	14,497,495,848.57
Mchanga/Udongo/Udongo Mwekundu	Tani	16,960.39	4,646,806.23	78,811,655,123.52
Jasi (Gypsum)	Tani	63,147.28	181,080.34	11,434,730,549.75
Aggregates	Tani	23,906.68	6,070,808.37	145,132,887,071.66
Marumaru	Tani	148,753.59	255,568.95	38,016,799,406.29
Bati	Tani	17,343.36	180,064.80	3,122,928,741.49
Kaolin	Tani	101,215.92	2,326.80	235,509,204.23
Galena	Kilo	5,235.60	185,231.00	969,795,423.60
Bauxite	Tani	141,928.08	8,299.00	1,177,861,111.87

Aina ya Madini	Kipimo	Bei kwa Kipimo	Jumla (Uzito)	Thamani (TZS)
Tanzanite	Karati	6,538,260.43	8,817.88	57,653,579,442.60
Makaa ya Mawe	Tani	87,496.29	429,709.85	37,598,019,450.90
Vito vya Mawe Mengine	Tani	47,154.04	1,589,732.59	74,962,321,927.47
Phosphates	Tani	97,773.00	213,306.00	20,855,567,114.26
Dolomite	Tani	21,147.48	6,836.47	144,574,090.49
Pozzolana	Tani	24,052.72	138,051.49	3,320,513,789.69
Mchanga, Mawe na Matofali	Tani	15,616.82	5,628,598.59	87,900,825,792.70
Dioksidi Kaboni (CO2)	Tani	1,446.53	7,557,612.79	10,932,322,581.22
Madini ya Shaba	Kilo	557,490.53	2,013.04	1,122,250,884.23
Madini ya Chuma	Kilo	48,454.41	16,555.53	802,188,387.36
Madini Mengineyo	Tani	212,220.00	1,411,965.85	299,647,392,663.88
Jumla				4,783,370,198,736.77

Kwa upande mwingine, thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 13.3 hadi dola za kimarekani milioni 1,860.52 mwaka 2017 kutoka dola za kimarekani 2,145.17 milioni mwaka 2016. Hii ilitokana na kuendelea kupungua kwa usafirishaji wa madini kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya 2010 mnamo 2017, ambayo inakataza usafirishaji wa madini ghafi na kuhamasisha usafirishaji wa madini yaliyochakatwa ili kuongeza thamani na hivyo kulinda masilahi ya Taifa kwa faida ya umma wa Watanzania kwa ujumla. Jedwali lifuatalo linaonesha kiasi na thamani ya madini yaliouzwa nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Aina ya Madini	Kipimo	Kiasi cha Madini		Thamani ya Mauzo (Dola za Marekani '000')	
		2016	2017	2016	2017
Almasi (Ghafi)	Karati ('000')	239,305	304,456	85,090	67,510
Dhahabu	Gramu ('000')	45,155	43,490	1,824,815	1,636,535
Vito vya Mawe	Gramu ('000')	2,944,107	1,185,697	60,483	53,596
Chumvi	Tani	145,718	100,017	4,806	3,803
Phosphate	Tani	23,658	1,351	721	585
Mawe Chokaa	Tani ('000')	4,170	3,301	22,710	27,610
Bati	Tani	138	91	1,499	1,037
Jasi (Gypsum)	Tani	213,744	123,675	6,279	3,187
Makaa ya Mawe	Tani	276,030	563,053	11,580	22,250
Graphite	Tani	1,180	128	2,132	18
Fedha	Gramu ('000')	17,984	10,911	9,901	5,850
Shaba	Ratili ('000')	16,247	2,934	35,421	7,741
Madini ya Viwandani	Tani	4,769,577	708,047	78,491	29,896
Bauxite	Tani	74,660	12,090	1,242	898
Jumla				2,145,170	1,860,516

Katika uchimbaji wa mafuta, Tanzania bado ipo katika hatua za utafutaji sehemu mbalimbali nchini. Kwa kiasi kikubwa Tanzania bado inategemea uagizaji wa mafuta kutoka nchi nyingine. Hata hivyo, kwa upande wa gesi asilia, nchi imezalisha kiasi kikubwa katika mwaka huu wa fedha. Kufikia sasa, idadi ya gesi asilia inayozalishwa kwa kiasi kikubwa inachangiwa na kampuni kubwa mbili, ambazo ni, M & P Exploration Production (T) Limited (amabyo inafanya shughuli za uchimbaji katika vitalu vya Mnazi

Bay na Pan African Energy Tanzania Limited (inayofanya shughuli za uchimbaji katika vitalu vya Songosongo). Kampuni hizi mbili kwa ujumla zilizalisha gesi kiasi cha ujazo fiti za ujazo 35,539,541,976. Uzalishaji wa gesi asilia unaendelea kukua huku ukichagizwa na ongezeko la mahitaji ya bidhaa hii kwa ajili ya matumizi ya viwandani na majumbani.

Kampuni	Eneo (Kitalu)	Kiasi (futi za Ujazo) '000'		Thamani (Dola za Kimarekani)	
		2016	2017	2016	2017
M & P Exploration (T) Limited	Mnazi Bay	5,792,142	17,960,300	13,818,715	19,466,121
Pan African Energy Tanzania Limited	Songosongo	29,747,400	29,496,560	38,172,718	22,795,142
Jumla		35,539,542	47,456,860	51,991,433	42,261,263

Wigo wa Ulinganishaji

Ripoti hii inashughulikia ulinganishi wa malipo na mapato kwa mwaka wa fedha 2016/17. Malipo na mapato yote yaliyofanywa kabla ya tarehe 1 Julai 2016 na yale ambayo yaliyofanywa baada ya tarehe 30 Juni 2017 yaliondolewa kwenye ripoti ya ulinganishi.

Taasisi za Serikali na Makampuni yaliyoshiriki kwenye Zoezi la Ulinganishi

Kulingana na mapato yaliyopotiwa na taasisi za serikali, Kamati ya TEITI ilikubaliana kwamba makampuni yote yaliyolipa kuanzia TZS milioni 900 kwa mwaka wa fedha 2016/17 yajumuishwe kwenye ulinganishaji. Makampuni yanayomilikiwa na Serikali hutakiwa kushiriki zoezi la ulinganishaji hata kama hayapo ndani ya wigo ulioidhinishwa na Kamati ya TEITI. Kati ya makampuni sabini na mbili (72) yaliyochaguliwa kushiriki zoezi la ulinganishi, Mlinganishi huru aliweza kuwasiliana na makampuni hamsini na tatu (53). Kati ya makampuni hayo hamsini waliyopatiwa fomu za ukusanyaji wa taarifa, ni makampuni 41 tu yaliwasilisha fomu zilizojazwa. Kampuni hizi 41 zilizojaza fomu zinachangia asilimia 86.78 ya jumla ya mapato yariyopatiwa na na serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Usahihi wa Taarifa

Kama inavyotakiwa na viwango vya kimataifa vya uhamasishaji uwazi na uwajibikaji katika rasilimali za nchi, Mlinganishi huru alizingatia mahitaji viwango hivyo ili kuhakikisha usahihi na uaminifu wa taarifa zilizoripotiwa na makumpuni na taasisi za serikali. Hii ilihuisha kupata uthibitisho wa taarifa zilizotolewa toka kwa viongozi waandamizi; kiambatisho cha stakabadhi husika za malipo, na majedwali yanayoonesha malipo-kwa-malipo, tarehe-kwa-tarehe; na uthibitisho wa mkaguzi wa nje wa fomu zilizojazwa za kutolea taarifa.

Kuhusu kampuni za madini, mafuta na gesi asilia, uthibitisho ultolewa na mkaguzi wa nje kuwa taarifa za kifedha za 2016/17 zimekaguliwa kwa kutumia Viwango vya Ukaguzi wa Kimataifa na kwamba taarifa zilizoripotiwa katika fomu za kutolea taarifa

ni kulingana na maagizo yaliyotolewa na Mlinganishi huru kama ilivyoidhinishwa na Kamati ya TEITI. Kwa taasisi za serikali, uthibitisho kama huo ultolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kati ya taasisi za serikali na kampuni arobaini na moja (41), thelathini na tisa (39) waliwasilisha fomu zao zilizosainiwa na uongozi (afisa mwandamizi aliyeidhinishwa). Kati ya taasisi za serikali na kampuni hizo 39, taasisi za serikali na kampuni ishirini na tano (25), fomu zao pia zilisainiwa na wakagazi wao wa nje. Kampuni mbili (2) za madini ambazo fomu hazikusainiwa na wasimamizi, pia hazikusainiwa na wakagazi wao wa nje. Kwa msingi wa uthibitisho uliotolewa na kiongozi mwandamizi na/au mkaguzi wa nje, Mlinganishi huru aliweza kuhitimisha kuwa ukamilifu wa jumla na usahihi wa taarifa kutoka kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na taasisi za serikali kuwa ni wa kuridhisha.

Muhtasari wa Matokeo ya Ulinganishi

Sura ya tano inawasilisha matokeo ya kina ya zoezi la ulinganishi, pamoja na tofauti zilizobainika kati ya kiwango cha fedha kilicholipwa na makapuni ya madini, mafuta na gesi asilia na kiasi kilichopokelewa na Taasisi za Serikali. Sura hii ya tano inaonesha kiasi kilichowasilishwa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na Taasisi za Serikali kabla ya zoezi la ulinganishi na marekebisho yaliyofanywa kufuatia kazi ya ulinganishi, na vile vile viwango vya mwisho na tofauti ambazo hazikufanikishwa ulinganishi wake. Marekebisho yalifanywa kwa msingi wa uthibitisho wa vielelezo ilipoonekana inahitajika kutoka kwa makumpuni na taasisi za serikali.

Tofauti halisi iliyobaki katika zoezi la ulinganishaji ni TZS 3,462,017,296.70 ikiwakilisha asilimia 0.39 ya malipo yote yaliyoripotiwa na taasisi za serikali. Ukokotoaji wa tofauti ulianza kwa kujumlisha tofauti za malipo yote ambayo kampuni zimelipa zaidi ya kiasi ambacho serikali imekiri kupokea. Hizi zinatambuliwa kama tofauti chanya, na jumla yake ni TZS 21,831,583,764.60. Hatua ya pili, ni kujumlisha tofauti za malipo yote ambayo serikali iliripoti kupokea zaidi ya kiasi ambacho makampuni yamelipa. Hizi zinatambuliwa kama tofauti hasi na jumla yake ni TZS 19,844,873,327.59.

Mapungufu

Wakati wa mchakato wa ulinganishaji, Mlinganishi huru alipata changamoto kadhaa ambazo zilipelekea ugumu wa kupata taarifa muhimu kwa muda muafaka. Changamoto hizi ni pamoja na:

- Ukosefu wa kanzidata ya kisasa yenyе taarifa kamilifu za makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia yaliyojumuishwa katika wigo wa ulinganishaji.
- Baadhi ya makampuni kusita kujaza na kurudisha fomu za taarifa kwa wakati, na baadhi ya makampuni hayaku jaza fomu hizo licha ya ufuutiliaji wa karibu.
- Utunzaji duni wa kumbukumbu mionganoni mwa wachimbaji wadogo/wachimbaji binafsi ambao walijumuishwa katika zoezi la ulinganishi kwa mwaka wa fedha 2017/18. Baadhi ya wachimbaji wadogo hawakuweza kutoa ushahidi wa malipo

waliyofanya kwa taasisi za serikali. Changamoto hii ilirefusha mchakato wa ulinganishaji.

- Baadhi ya makampuni kutotoa taarifa za wanufaikaji wa umiliki wa makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia. Licha ya ufuatiliaji wa karibu, zaidi ya nusu ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia hazikutoa taarifa za wanufaikaji wa umiliki wa makampuni.
- Baadhi ya makampuni kutojaza taarifa sahihi kwenye fomu za kutolea taarifa. Mlinganishi huru alilazimika kutafuta ufanuzi na uthibitisho kutoka kwa kampuni hizo, ambazo mwishowe zilichelewesha zoezi la ulinganishi.

Matokeo na Mapendelekezo

Kulingana na hadidu za rejea za kazi hii, Mlinganishi huru ameandaa ripoti ya 10 ya TEITI ya malipo yaliyofanywa na makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia na mapato yaliyopokelewa na taasisi za serikali katika mwaka wa fedha 2017/18. Matokeo yanaonesha kuwa kuna tofauti za malipo na mapato yaliyosalia katika zoezi la ulinganishaji. Kwa kuongezea, masuala yafuatayo pia yaligunduliwa:

- i. Utoaji mdogo wa taarifa za wamiliki wanufaika wa makampuni
- ii. Mapungufu katika kanzidata ya taarifa za makampuni
- iii. Ucheleweshwaji wa kuwasilisha fomu za taarifa
- iv. Fomu za kuwasilishia taarifa kutojazwa vizuri na kwa usahihi
- v. Zoezi la ulinganishaji wa mapato na malipo lifanyike katika muda stahiki

Masuala yaliyo hapo juu yanapewa kipaumbele cha juu, na mapendelekezo kadhaa yametolewa kwa kuzingatia masuala haya katika sura ya saba. Iwapo mapendelekezo haya yatashughulikiwa, Tanzania itakuwa katika nafasi nzuri sana katika kuripoti taarifa za madini, mafuta na gesi asilia na pia kuweza kuripoti utekelezaji wa viwango vya EITI.



CPA. Dkt. Gabriel Komba

CHUO KIKUU MZUMBE

1 UTANGULIZI

1.1 Maelezo ya Awali

The Extractive Industries Transparency Initiative (EITI), ambayo tafsiri ya Kiswahili ni Mpango wa Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Maliasili za Madini, mafuta na gesi asilia, ni umoja wa kimataifa wa Serikali, Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia, na Asasi za Kiraia (CSOs) zinazofanya kazi pamoja kuboresha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa mapato yatokanayo na maliasili. Tanzania ilijiunga na EITI mnamo Februari 2009, kwa nia ya kuboresha utawala bora katika sekta za madini, mafuta na gesi asilia. Tanzania ilipata uanachama kamili wa EITI mnamo Desemba 2012, baada ya kufikia viwango vya uwazi vya EITI. Tanzania ilitunikiwa hadhi ya “meaningful progress” kwa ya kwamba nchi imepiga hatua muhimu katika masuala ya uwazi na uwajibikaji kutoka na tathimini ya utekelezaji wa viwango vya EITI ya mwaka 2017. Tangu Tanzania ijiunge na EITI imechapisha ripoti 8 za TEITI za kati ya kipindi cha 1 Julai 2008 hadi 30 Juni 2016. Ripoti ya 8 ya TEITI ilikuwa ya mwaka wa fedha 2015/16 na ilichapishwa tarehe 30 Aprili 2018. Hii ni ripoti ya 9 ya TEITI na inahusisha kipindi mwaka wa fedha cha 1 Julai 2016 hadi 30 Juni 2017.

1.2 Madhumuni

Madhumuni ya ripoti hii ni kulinganisha taarifa za malipo yaliyopotiwa na makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia na taarifa za mapato yaliyopokelewa na taasisi za serikali. Dhumuni kuu la Ulinganishi wa malipo na mapato ni kusaidia serikali kubaini mchango unaotokana na uvunaji wa rasilmali za madini, mafuta na gesi asilia katika uchumi wa taifa. Aidha ulinganishaji wa malipo na mapato unasaidia kuongeza uwazi katika usimamizi wa rasilmali hizo.

1.3 Taratibu Zilizofuatwa katika Utekelezaji wa Kazi

Kazi hii ya ulinganishi wa malipo na mapato ilifanywa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa na taratibu na mashariti yaliyoainishwa kwenye hadidu za rejea na mkataba wa huduma ya ushauri na kupitishwa na Kamati ya TEITI. Taratibu za kazi hii ya ulinganishaji haijumuishi ukaguzi wa hesabu za makampuni au taasisi za serikali kuhusu malipo na mapato yatokanayo na shughuli za madini, mafuta na gesi asilia. Ulinganishaji ulifanywa kwa kutumia taarifa za malipo zilizowasilishwa na makampuni na taasisi za serikali.

Ripoti hii ina sura saba (7) kama ifuatavyo:

- i. Utangulizi;
- ii. Njia zilizotumika kukusanya na kuchambua taarifa;
- iii. Hali ya sekta ya madini, mafuta na gesi asilia;
- iv. Zoezi la Ulinganishaji;
- v. Matokeo ya Zoezi la Ulinganishaji;

vi. Uchambuzi wa taarifa zilizoripotiwa; na

vii. Mapendekezo.

Malipo na mapato katika ripoti yapo katika Shilingi ya Tanzania (Tzs) isipokuwa imeelezwa vinginevyo. Ripoti hii inajumuisha taarifa zilizopokelewa hadi 3 Juni 2020.

2 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA KUANDAA RIPOTI

Mchakato wa ulinganishaji wa malipo na mapato kutoka sekta ya madini, mafuta na gesi asilia ulikuwa na hatua zifuatazo:

- Hatua ya 1: Kufanya utafiti ili kubaini wigo wa zoezi la ulinganishi. Hasa, utafiti huo ulihusisha kuandaa orodha ya kampuni za madini, mafuta na gesi asilia ambayo yalilipa TZS milioni 900 ua zaidi Serikalini, na orodha ya taasisi za Serikali ambazo zilipokea malipo hayo kutoka kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia, ambazo zinapaswa kuwepo katika ripoti ya nyongeza ya 2016/17;
- Hatua ya 2: Utayarishaji wa fomu za kutolea taarifa na maelekezo ya kuripoti, baada ya kupata taarifa zinazohusiana na aina tofauti za ushuru, ada, tozo zinazolipwa katika sekta ya madini, mafuta na gesi;
- Hatua ya 3: Uwasilishaji na kupata idhini ya kufanya utafiti wa kubaini wigo, kutumia fomu za kutolea taarifa, na maelekezo ya kuripoti kwa Kamati ya TEITI;
- Hatua ya 4: Kufanya mafunzo kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na taasisi za serikali juu ya namna ya ujazaji fomu za kutolea taarifa;
- Hatua ya 5: Ukusanyaji wa taarifa za malipo kutoka kwa taasisi za serikali na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia, ambazo zilitumika katika ulinganishi;
- Hatua ya 6: Kulinganisha kiwango kilichoripotiwa na wakala wa taasisi za serikali na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia ili kubaini ikiwa kuna tofauti kati ya vyanzo viwili vya taarifa; na
- Hatua ya 7: Kuwasiliana na taasisi za serikali na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia ili kuchunguza na kutatua tofauti zilizotambuliwa.

2.1 Utafiti Kubaini Wigo wa Ulinganishi

Mlinganishi huru alifanya utafiti wa kubaini wigo wa ulinganishaji kulingana na hadidu za rejea. Utafiti huo ulianza na mkutano kati ya Mlinganishi huru, Wizara ya Madini (MoM), Kamati ya TEITI, na wawakilishi kutoka Sekretarieti ya Kimataifa ya EITI (Bi. Ines Marques na Bi. Lyydia Kilpi). Mkutano ulifanyika tarehe 21 Oktoba 2019, na ulijadili ucharaka wa Tanzania kuchapisha ripoti za TEITI za 2016/17 kufikia tarehe 31 Disemba 2019

TEITI imechapisha ripoti nane (8) za kubaini wigo wa ulinganishaji kuanzia miaka ya fedha ya 2008/09 hadi 2015/16. Ripoti hii ya utafiti wa kubaini wigo wa ulinganishaji ilihusisha miaka ya 2016/17 na 2017/18 na utafiti ulifanywa kutoka tarehe 4 hadi 15 Novemba 2019. Wakati wa kufanya utafiti huo, Mlinganishi huru alikusanya taarifa kutoka kwa taasisi zifuatavyo za Serikali:

- i. Wizara ya Madini;
- ii. Mamlaka ya Mapato Tanzania;
- iii. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania;
- iv. Shirika la Hifadhi ya Jamii;
- v. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Utumishi wa Umma; na
- vi. Tume ya Madini.

Kulingana na matokeo ya utafiti, Mlinganishi huru aliripoti masuala mbalimbali kwa Sekretarieti ya TEITI ili yazingatiwe katika kuamua wigo wa ulinganishaji wa mwaka wa fedha wa 2016/17. Masuala haya ni pamoja na:

- Maelezo ya hali ya sekta ya madini, mafuta na gesi asilia, pamoja na maendeleo ya hivi karibuni katika miundo ya sheria na udhibiti;
- Wigo wa ulinganishi uliopendekezwa kwa ajili ya kujumuishwa makampuni katika mchakato wa ulinganishi;
- Ushuru, kodi, ada, tozo, na mapato yakayojumuishwa katika ripoti ya ulinganishi;
- Kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na wakala wa taasisi za Serikali zitakazojumuishwa kwenye ripoti;
- Fomu za kutolea taarifa zitakazojazwa; na
- Uthibisho unaopaswa kutolewa na taasisi za serikali na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zilizopendekezwa kuripoti ili kuhakikisha usahihi wa taarifa iliyotolewa.

Utafiti wa kubaini wigo wa ulinganishaji uliwasilishwa mbele ya Kamati ya TEITI kwa uhakiki na kuidhinishwa. Kamati iliidhinisha matokeo ya utafiti na kutoa idhini ya kuendelea na utayarishaji wa ripoti ya ulinganishi.

2.2 Ukusanyaji wa Taarifa

Kabla ya ukusanyaji wa taarifa, tulitengeneza fomu za kupekelea taarifa na maelekezo ya namna ya kujaza kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na taasisi wa serikali. Kisha, Sekretarieti ya TEITI iliandaa warsha ya wadau ambayo ilikusudia kuwajulisha wawakilishi wa taasisi za serikali na kampuni jinsi ya kujaza fomu za kutolea taarifa. Hasa, wawakilishi hao walielekezwa kuhusu:

- Mchakato wa EITI;
- Wigo wa ulinganishi;
- Fomu za kutolea taarifa na maelekezo ya namna ya kujaza;
- Mambo tuliojifunza kutokana na ripoti za awali za ulinganishi; na
- Masuala ya ulinganishi.

Warsha ya wadau ilifanyika Chuo Kikuu cha Mzumbe - Chuo cha Kampasi ya Dar es Salaam mnamo tarehe 5 Desemba 2019. Wakati wa warsha hiyo, Mlinganishi huru alifafanua masuala yote ambayo wawakilishi wa taasisi za serikali na kampuni zilizojumuishwa walitaka kujua juu ya fomu hizo kutolea taarifa. Mwenyekiti wa Kamati

ya TEITI na wawakilishi kutoka Kamati ya TEITI, serikali, kampuni za madini, mafuta na gesi asilia, na asasi za kiraia walihudhuria.

Kabrasha la kukusanya taarifa lilijumuisha fomu za kutolea taarifa na maelekezo ya jinsi ya kujaza. Sekretarieti ya TEITI ilituma kabrasha kwa njia ya kielektroniki kwa taasisi za serikali na makampuni husika baada ya warsha hiyo. Taasisi za serikali na kampuni zilielekezwa kutuma fomu zilizoja zwa sawasawa ndani ya muda uliotolewa kwa Mlinganishi huru. Taasisi za serikali na kampuni ziliombwa pia kumwuliza Mlinganishi huru chochote kinachohusiana na ujazaji wa fomu endapo kungetokea tatizo. Tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa fomu zilizoja zwa ilikuwa tarehe 12 Desemba 2019. Walakini, tarehe hiyo ya mwisho iliongezwa hadi tarehe 30 Januari 2020 ili kuruhusu taasisi za serikali na kampuni zaidi ambazo hazikuweza kuwasilisha fomu zao ndani ya muda uliopangwa awali kufanya hivyo. Fomu ya mwisho ilijoja zwa na kujumuishwa katika ripoti hii ilipokelewa mnamo tarehe 3 Juni 2020. Fomu zilizoidhinishwa za kutolea taarifa zimewekwa kama Kiambatisho 1 na 2 cha ripoti hii.

2.3 Ulinganishi na Uchunguzi wa Tofauti

Mlinganishi huru alifanya mchakato wa ulinganishi kwa msingi wa uhasibu wa fedha taslimu. Tuliandaa ukurasa wa kufanya kazi katika programu ya kompyuta ya Excel kwa kila kampuni ya madini, mafuta na gesi asilia ili kujua jumla ya malipo yaliyofanywa kwa kila taasisi ya serikali inayopokea malipoke. Taarifa zinazohusiana na mapato zilizoripotiwa na taasisi wa serikali ziliingizwa katika kurasa hizo kwa madhumuni ya kulinganisha. Tuliunda pia ukurasa tofauti katika faili hilo ambao unatoa muhtasari wa mapato yote ya Serikali kulingana na aina za mapato na ukurasa ambao unatoa muhtasari wa jumla ya malipo yaliyofanywa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zilizoshiriki katika mchakato wa ulinganishi.

Mchakato wa kulinganisha taarifa na kuchunguza tofauti ulifanywa kati ya tarehe 10 Februari na 22 Aprili 2020. Katika zoezi la ulinganishi, tulifanya taratibu zifuatazo:

- Tarakimu zilizoripotiwa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zililinganishwa kipengele-kwa- kipengele na tarakimu zilizoripotiwa na taasisi za serikali. Kwa hivyo, tofauti zote zilizoainishwa ziliorodheshwa kwa kila kitu kuhusiana na kila taasisi za serikali na kampuni ya madini, mafuta na gesi asilia ;
- Pale ambapo taarifa iliyoripotiwa na kampuni ya madini, mafuta na gesi asilia ilikubaliana na taarifa iliyoripotiwa na serikali, tarakimu za serikali zilizingatiwa kuwa zimethibitishwa, na hakukuchukuliwa hatua zaidi;
- Tulifanya uchunguzi zaidi ambapo kama tofauti kati ya kila mtiririko wa kifedha ilizidi TZS milioni mbili na kuhitimisha zoezi la ulinganishi wakati tofauti ilikuwa chini ya asilimia moja ya jumla ya malipo ya kampuni yaliyoripotiwa na mapato ya serikali, na
- Mlinganishi huru aliomba taasisi za serikali na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kutoa nyaraka za ziada na ushahidi wa marekebisho yoyote ya taarifa

iliyotolewa kwenye fomu za kutolea taarifa za awali zilizojazwa.

Katika hali ambazo hatukuweza kutatua utofauti, tuliomba taasisi za serikali na kampuni zilizojumuishwa katika zoezi la ulinganishi kuleta nyaraka za ziada za malipo yaliyotamkwa katika fomu. Katika hali nyingine, tofauti hizi zilibaki bila kutatuliwa. Sura ya 5 inatoa matokeo ya zoezi la ulinganishi.

2.4 Usahihhi na Kuaminika kwa Taarifa Zilizoripotiwa

Ili kuzingatia viwango vya EITI na kuhakikisha usahihhi wa taarifa, Kamati ya TEITI katika mkutano wake wa tarehe 24 Novemba 2019 ilikubali kwamba:

- Kwa kila kampuni, ripoti ya malipo inapaswa kusainiwa na afisa Mwandamizi aliyeidhinishwa wa kampuni;
- Kwa kila taasisi ya serikali, ripoti ya mapato inapaswa kusainiwa na Afisa Mwandamizi aliyeidhinishwa wa taasisi;
- Taarifa zote zilizoripotiwa katika fomu ya mtiririko wa malipo/mapato lazima ziwe maelezo ya kina ya malipo kwa malipo na tarehe kwa tarehe katika nyaraka za ziada;
- Kila fomu ya kutolea taarifa lazima ithibitishwe na Mkaguzi wa nje:
 - *Kampuni za madini, mafuta na gesi asilia:* zinatakiwa kupata uthibitisho kutoka kwa mkaguzi wa nje kuwa taarifa zao za kifedha za 2016/17 zimekaguliwa kwa kuzingatia viwango vya ukaguzi wa kimataifa na kwamba takwimu zilizoripotiwa katika fomu ya kutolea taarifa ni kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na Mlinganishi huru, yamekamilika, na wanakubaliana na taarifa ya fedha ya kipindi cha 2016/17; na
 - *Taasisi za Serikali:* zinatakiwa kupata uthibitisho kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba miamala iliyoripotiwa katika fomu ya kutolea taarifa ni kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na Mlinganishi huru, yamekamilika, na yanakubaliana na hesabu za Serikali kwa kipindi cha 2016/17.
- Ili kufanya mabadiliko yoyote kwenye taarifa iliyowasilishwa awali kwenye fomu, Mlinganishi huru alizionomba taasisi za serikali na kampuni husika kutoa nyaraka za ziada kama ushahidi au kutoa uthibitisho wa maandishi kabla ya marekebisho kukubaliwa.

2.4.1 Uwasilishaji wa Taarifa

Jumla ya taasisi za serikali na kampuni arobaini na moja (41) zilizojumuishwa katika wigo wa ulinganishi ziliwasilisha fomu zao za kutolea taarifa. Kati ya hizi, tatu (3) zilikuwa Kampuni zinazomilikiwa na Serikali na zilizobaki thelathini na nane (38) zilikuwa kampuni/watu binafsi. Taasisi zote za serikali zilizojumuishwa katika wigo wa ulinganishi ziliwasilisha fomu zao. Taarifa zinazotakiwa kuwasilishwa na taasisi za

serikali na kampuni zilizojumuishwa katika wigo wa ulinganishi zimo katika fomu zilizoidhinishwa kama zinavyoonekana katika Kiambatisho 1 na 2 cha ripoti. Taarifa zilizokusanywa zilichunguzwa na Mlinganishi huru ili kuhakikisha kuwa ni kikamilifu na sahihi.

2.4.2 Uthibitisho wa Taarifa

Kati ya taasisi za serikali na kampuni arobaini na moja (41), thelathini na tisa (39) waliwasilisha fomu zao zilizosainiwa na uongozi (afisa mwandamizi aliyeidhinishwa). Kati ya taasisi za serikali na kampuni hizo 39, taasisi za serikali na kampuni ishirini na tano (25), fomu zao pia zilisainiwa na wakagazi wao wa nje. Kampuni mbili (2) za madini, mafuta na gesi asilia ambazo fomu hazikusainiwa afisa mwandamizi, pia hazikusainiwa na wakagazi wao wa nje kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Namba 1.

Jedwali Na. 1: Uthibitisho wa Fomu za Kutolea Taarifa

Na.	Kampuni	Saini ya Kiongozi wa Kampuni	Saini ya Mkaguzi wa Nje	Jina la Kampuni ya Ukaguzi
1	GEITA GOLD MINING LIMITED	✓	X	-
2	NORTH MARA GOLD MINE LIMITED	✓	✓	Ernst & Young Tanzania
3	BULYANHULU GOLD MINE LIMITED	✓	✓	Ernst & Young Tanzania
4	PAN AFRICAN ENERGY TANZANIA LIMITED	✓	✓	KPMG Tanzania
5	PANGEA MINERALS LTD	✓	✓	Ernst & Young Tanzania
6	M&P EXPLORATION PRODUCTION TANZANIA LIMITED	✓	✓	KG Consulting
7	SHANTA MINING COMPANY LIMITED	✓	✓	BDO East Africa
8	AUMS (T) LIMITED	✓	✓	PwC Tanzania
9	SHELL EXPLORATION AND PRODUCTION TANZANIA LIMITED	✓	✓	Deloitte Consulting Ltd
10	WILLIAMSON DIAMONDS LTD	✓	✓	Deloitte Consulting Ltd
11	HANCIENDA GROUP LTD	✓	X	-
12	NDOVU RESOURCES LIMITED	✓	✓	Hekima Associates
13	POA POA COMPANY LTD	✓	✓	Danis Associates
14	AFRICAN EXPLOSIVES (T) LTD	✓	✓	Diamond Financial Consultants
15	EQUINOR TANZANIA AS	✓	✓	KPMG Tanzania
16	PANAFRICAN MINING SERVICES (TANZANIA) LIMITED	✓	✓	KPMG Tanzania
17	JOSIA MASANJA & PTNS	✓	X	-
18	MANTRA TANZANIA LIMITED.	✓	✓	KPMG Tanzania
19	NYAMIGOGO	✓	✓	Hassanali Rutakyamirwa & Co
20	TANCOAL ENERGY LIMITED	✓	✓	VA Business Assurance Services
21	OPHIR TANZANIA (BLOCK 1) LIMITED	✓	✓	Ernst & Young Tanzania
22	AROBOGAST SILIO LULILA LIMITED	✓	X	-

Na.	Kampuni	Saini ya Kiongozi wa Kampuni	Saini ya Mkaguzi wa Nje	Jina la Kampuni ya Ukaguzi
23	GLOBELEQ TANZANIA SERVICES LIMITED	✓	✓	Ernst & Young Tanzania
24	GODFREY MITTI & PTNS	✓	X	-
25	NITRO EXPLOSIVES (T) LTD.	✓	X	-
26	RAS AL KHAIMAH GAS TANZANIA LTD	X	X	-
27	SEA SALT LIMITED	X	X	-
28	JAC RIJK AFRICA LIMITED	✓	✓	Ark Partners
29	ORECORP TANZANIA LIMITED	✓	X	-
30	DODSAL HYDROCARBONS & POWER (TANZANIA) LTD.	✓	X	-
31	KABANGA NICKEL COMPANY LIMITED	✓	X	-
32	MBOGO MINING AND GENERAL SUPPLY LIMITED	✓	✓	G-Washington & Company
33	BUSOLWA MINING LIMITED	✓	✓	G-Washington & Company
34	BEARING MAN GROUP TANZANIA LIMITED	✓	X	-
35	KATAVI MINING COMPANY LIMITED	✓	X	-
36	HENAN AFRO-ASIA GEO-ENGINEERING (TANZANIA) CO. LTD.	✓	X	-
37	TNR LIMITED	✓	✓	Tanna Sreekumar Grant Thorntorn
38	ABG EXPLORATION LIMITED	✓	✓	Ernst & Young Tanzania
39	TANZANIA PETROLEUM DEVELOPMENT CORPORATION	✓	✓	CAG
40	STATE MINING COOPERATION (STAMICO)	✓	X	-
41	STAMIGOLD COMPANY LIMITED	✓	✓	KPMG Tanzania

Ufunguo: ✓ = Ndiyo; X = Hapana

Isipokuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, fomu zilizowasilishwa za taasisi zingine za Serikali zilisainiwa na maafisa walioidhinishwa tu. Kwa kuwa taasisi hizi za serikali zilikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mnamo 2016/17¹, Mlinganishi huru alitegemea saini ya kiongozi mwandamizi wa taasisi ili kuhakikisha uhalali wa taarifa iliyoripotiwa. Kwa sababu ya changamoto za kupatikana kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zinazofanya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wa Kamati ya TEITI kupitia Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa aliomba Makatibu Tawala wa Mikoa kusaidia kutambua kampuni zinazofanya malipo kwa Halmashauri zilizo chini ya mamlaka yao. Mlinganishi huru, kwa hivyo, alipokea barua kutoka kwa Makatibu Tawala au Wakurugenzi Watendaji wakithibitisha kiasi ambacho Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilijaza katika fomu za kutolea taarifa kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia

¹ <https://www.nao.go.tz/uploads/reports/CENTRAL-GOVERNMENT-GENERAL-REPORT-2017-2018.pdf>
<https://www.nao.go.tz/index.php/reports/category/general-audit-reports>

zinazofanya kazi katika Halmashauri hizo. Jedwali Namba 2 linaonyesha hali ya uthibitisho wa fomu zilizojazwa na Halmashauri.

Jedwali Na. 2: Uthibitisho wa Fomu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka ya Serikali za Mitaa	Afisa Aliyethibisha Fomu
Halmashauri ya Wilaya ya Msalala	RAS - Mkoa wa Shinyanga
Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga	RAS - Mkoa wa Ruvuma
Halmashauri ya Mji wa Geita	Mkurugenzi wa Mji - Geita
Halmashauri ya Mji wa Kahama	Mkurugenzi wa Mji - Kahama
Kinondoni Municipal Council	Mkurugenzi wa Manispaa - Kinondoni
Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu	Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya - Kishapu
Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya - Mtwara
Halmashauri ya Wilaya ya Songwe	Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya - Songwe
Halmashauri ya Wilaya ya Tarime	Mweka Hazina wa Wilaya - Tarime

Kwa msingi wa uthibitisho uliotolewa na uongozi na/au mkaguzi wa nje, na isipokuwa athari za mambo yaliyoelezewa hapo juu, Mlinganishi huru alihitimisha kuwa ukamilifu wa jumla na usahihi wa taarifa kutoka kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na taasisi za serikali kuwa wa kuridhisha.

2.5 Rekodi za Uhasibu

Kwa mujibu viwango vya EITI, makampuni lazima yatoe taarifa kwa mtiririko wa malipo yaliyolipwa kwa kila taasisi ya serikali. Taasisi za serikali na kampuni ziliojumuishwa katika mchakato wa ulinganishi ziliombwa kutoa maeleo sahihi katika fomu za kutolea taarifa kwa kila mtiririko wa malipo, na taarifa nyingine za msingi kama zilivyoanishwa kwenye fomu.

Ulingenishi ulifanywa kwa msingi wa fedha taslimu. Hivyo basi, malipo yaliyofanywa kabla ya tarehe 1 Julai 2016 yalitengwa. Ilifanyika vivyo hivyo kwa malipo yaliyofanywa baada ya tarehe 1 Julai 2017.

Fedha iliyotumika katika kutolea taarifa ni shilingi ya Tanzania (TZS). Kwa malipo yaliyofanywa kwa fedha za kigeni, taasisi za serikali na kampuni zilitakiwa kutoa taarifa kwa fedha iliyofanyiwa malipo. Hata hivyo, katika kuandaa ripoti hii, malipo yaliyofanywa kwa Dola za Kimarekani yalibadilishwa kuwa ya TZS kwa kiwango cha wastani cha kila siku kwa kipindi cha 2016/17 kulingana na Benki Kuu ya Tanzania wa US\$ 1 = TZS 2,210.62.²

2.5.1 Kampuni za Madini, Mafuta Na Gesi Asilia

Kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kwa kawaida huandaa rekodi za kila mwaka za uhasibu kwa msingi wa mapato na matumizi halisi, kwa mfano, gharama ya ushuru inatambuliwa na kurekodiwa pale inapotokea badala ya wakati fedha taslimu inalipwa.

²<https://www.bot.go.tz/FinancialMarkets/IFEMsummaries/IFEMsummaries.asp>

Walakini, ni fedha taslimu tu ambazo zililipwa wakati wa mwaka wa fedha wa Serikali kutoka tarehe 1 Julai 2016 hadi 30 Juni 2017 zilijumuishwa katika fomu.

2.5.2 Taasisi wa Serikali

Taasisi za serikali zilitakiwa kuripoti tu kiasi kilichopokelewa wakati wa 2016/17, bila kujali ikiwa mapato hayo yalirekodiwa katika mwaka uliopita wa fedha au uliofuata.

3 HALI YA SEKTA YA MADINI, MAFUTA NA GESI ASILIA

3.1 Taarifa Muhimu za Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia

3.1.1 Sekta ya Madini

Tanzania imejaliwa aina mbalimbali za madini yanayopatikana katika makundi makuu matano. Makundi haya yanajumuisha madini ya metali, madini ya vito, madini ya viwandani, madini ya nishati, na malighafi za ujenzi.³ Kundi la madini ya metali linajumisha madini ya Dhahabu, Chuma, Fedha, Shaba, Nikeli, Platinamu na Bati wakati kundi la madini ya vito linajumuisha madini ya Almasi, Tanzanaiti, Rubi, Ganeti, Zamaradi, Yakuti, na Alexandrite. Kundi la madini ya viwandani linajumuisha madini ya Kaolini, Fosifeti, Chokaa, Jasi, Chumvi, Diatomiti, Bentonite, na mchanga wa pwani. Kundi la madini ya nishati lina makaa ya mawe na urani wakati malighafi za ujenzi zinajumuisha mchanga na mawe ya ujenzi.

Rasilimali hizi za madini zinapatakanwa kwa viwango tofauti tofauti. Jedwali namba 3 linaonesha aina kuu na kiasi halisi cha madini yanayopatikana nchini Tanzania.

Jedwali Na. 3: Aina Kuu na Kiasi cha Madini Yanayopatikana Tanzania

Na.	Aina ya Madini	Kizio	Kiasi Kilichothibitishwa
1.	Dhahabu	Tani	2,222.00
2.	Nikeli	Tani	40.00
3.	Shaba	Tani	13.65
4.	Makaa ya Mawe	Tani	1.50 bilioni
5.	Tanzanaiti	Tani	12.60
6.	Almasi	Karati	50.90 milioni
7.	Urani	Ratili	35.90 milioni

Chanzo: Poncian and Kigodi (2018)⁴

Kati ya rasilimali za madini zinazopatikana Tanzania, madini ya dhahabu yanaongoza kibiashara. Tanzania inashika nafasi ya nne kwa uzalishaji mkubwa wa dhahabu barani Afrika baada ya Afrika Kusini, Ghana, na Mali. Migodi mikubwa inayozalisha madini ya dhahabu nchini Tanzania ni mgodi wa dhahabu wa Geita uliopo mkoani Geita, mgodi wa dhahabu wa North Mara uliopo mkoani Mara, mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu na mgodi wa dhahabu wa Buzwagi inayopatikana mkoani Shinyanga. Mingine ni pamoja na mgodi wa dhahabu wa Luika unaopatikana mkoani Songwe, na mgodi wa STAMIGOLD-Biharamulo, ambao zamani ulikuwa unajulikana kama mgodi wa dhahabu wa Tulawaka, unaopatikana mkoani Kagera.

Mbali na uzalishaji wa madini ya dhahabu unaofanywa na makampuni makubwa, dhahabu pia inazalishwa na wachimbaji wadogo. Takwimu za Wizara ya Madini zinaonesha kuwa dhahabu inayozalishwa na wachimbaji wadogo ni karibu tani 1.1.⁵ Taarifa za Wizara ya Madini zinaonesha kuwa takribani asilimia 24 ya dhahabu inayozalishwa na wachimbaji wadogo inatoka Mkoa wa Geita. Maeneo mengine

³ http://www.teiti.or.tz/wp-content/uploads/2014/03/0014_11032013_Mineral_Policy_of_Tanzania_20091.pdf

⁴ <https://doi.org/10.1080/21665095.2018.1486219>

⁵ <https://pubs.iied.org/pdfs/16641IIED.pdf>

ambayo wachimbaji wadogo huzalisha dhahabu ni pamoja na mikoa ya Mara, Singida, Mbeya, Tanga, Morogoro, na Arusha.

Katika mwaka 2019, Wizara ya Madini ilifanya jitihada mbalimbali za kukuza sekta ya madini. Jitihada hizi ni pamoja na kuanzisha masoko ya madini Tanzania, kuanzisha vituo vya umahiri na kujenga vituo vya mfano kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa madini.

i. Kuanzishwa kwa Masoko ya Madini

Mnamo mwaka 2019, Serikali ilifungua masoko ya madini ikiwa ni moja ya mikakati ya kukuza biashara ya madini nchini na kuzuia utoroshaji wa madini nje ya nchi. Soko la madini la kwanza lilifunguliwa katika Mkoa wa Geita tarehe 17 Machi 2019. Masoko mengine yaliendelea kufunguliwa sehemu mbalimbali na kufikia mwezi Februari 2020, jumla ya masoko 28 yalianzishwa kama sehemu ya mpango wa kukomesha biashara haramu ya madini pamoja na kuongeza faida ya biashara ya madini kwa Serikali, wachimbaji wadogo, wafanyabiashara wa madini, na madalali.⁶ Sambamba na mpango wa kuanzisha masoko hayo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha muswada wa sheria uliolenga kuwapunguzia mzigo wa kodi wachimbaji wadogo. Kufuatia kupitishwa kwa sheria hiyo, wachimbaji wadogo hawatozwi asilimia tano ya kodi ya zuio na asilimia 18 ya kodi ya ongezeko la thamani wakati wa kuuza madini yao.

Kwa upande mwingine, masoko ya madini yanarahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu za wachimbaji, madalali, na wafanyabiashara wa madini katika mikoa ambayo masoko hayo yameanzishwa. Vilevile, taarifa zinazokusanya kutoka katika masoko ya madini zinasaidia serikali na wadau wengine kufuatilia makusanyo ya ushuru na mapato yatokanayo na uzalishaji wa madini. Pia zinasaidia kubuni hatua stahiki za kukuza biashara ya madini nchini.

ii. Kuanzishwa kwa Vituo vya Umahiri na Vituo vya Mfano

Uchimbaji wa madini unaofanywa na wachimbaji wadogo ni shughuli kuu ya kiuchumi katika jamii zinazoishi pembezoni mwa migodi ya madini nchini Tanzania. Katika juhudzi za kukuza uwezo wa wachimbaji wadogo wa madini, Wizara ya Madini kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini, imeanzisha vituo saba vya umahiri. Vituo hivyo vimejengwa katika maeneo ya Mpanda, Bariadi, Handeni, Musoma, Chunya, Songea, na Bukoba. Lengo la vituo hivyo vya umahiri ni kutoa mafunzo ya jiolojia katika utafiti wa madini, uongezaji thamani madini, biashara ya madini, na uchenjuaji wa madini kwa kutumia teknolojia rafiki kwa mazingira, hususani teknolojia isiyotumia Zebaki.

Vilevile, Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Umoja wa Kuwasaidia Wachimbaji Wadogo Wanaozunguka Migodi Mikubwa, imeanzisha vituo vitatu vya mfano. Vituo viwili vya Lwamgasa na Katente, Bukombe mkoa wa Geita. Kituo cha tatu kipo Itumbi,

⁶ <https://drive.google.com/file/d/1GQsqFWboRhVzJ0IXXse1MUqc8nuaDUWL/view>

Chunya mkoa wa Mbeya.⁷ Vituo hivi vya mfano vina vifaa vya kisasa vya kuchakata madini ambavyo vinatoa ujuzi kwa vitendo kwa wachimbaji wadogo katika fani ya uchakataji madini. Kituo cha Lwamgasa kimetengwa mahususi kwa kuchakata dhahabu wakati vituo vya Itumbi na Katente vimejengewa uwezo wa kuchakata madini ya aina mbalimbali.

Aidha, Wizara ya Madini imetenga maeneo 11 yenye jumla ya hekta 38,952 kwa ajili ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini. Maeneo hayo yapo Biharamulo II, Itigi, Kyerwa, D-Reef, Ibinda, Kapanda, Ngapa, Nzega, Kitowelo, Msasa na Matabe.⁸

3.1.2 Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia

Tanzania inatajwa kuwa na kiwango kikubwa cha rasilimali ya mafuta na gesi asilia. Hata hivyo, hadi kufikia mwisho wa mwaka 2017, mafuta yalikuwa hayajagunduliwa, lakini shughuli za utafutaji zinaendelea katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa gesi asilia unaongezeka kwa kasi ukichochewa na nia ya serikali ya kukuza uchumi kupitia rasilimali ya gesi asilia.

Takwimu za rasilimali ya gesi asilia za mwaka 2017, zinaonesha kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na hifadhi ya gesi asilia zenye futi za ujazo trilioni 57.54.⁹ Kufuatia ugunduzi wa kiasi kikubwa cha gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini, serikali imefanya mabadiliko makubwa katika sheria na udhibiti kwa lengo la kuboresha usimamizi na utawala wa sekta hii. Vilevile, mabadiliko hayo yanalenga kuhakikisha kuwa serikali na wananchi kwa ujumla wanafaidika na rasilimali zinazopatikana kutoka kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia.

Vivyo hivyo, Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli, ni mbia katika mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki. Mradi huu unatarajiwa kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda hadi bandari ya Tanga, Tanzania. Mradi huuunamilikiwa na washirika watano ambao ni kampuni ya Total SA inayomiliki asilimia 35, China National Offshore Oil Corporation inayomiliki asilimia 35, Kampuni ya Bomba la Mafuta ya Uganda inayomiliki asilimia 15. Wamiliki wengine ni kampuni ya Tullow Oil inayomiliki asilimia 10, na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linalomiliki asilimia 5. Bomba la mafuta linatarajiwa kuwa na urefu wa kilomita 1,443 litakapokamilika. Bomba na linatarajiwa kusafirisha mapipa 230,000 ya mafuta ghafi kwa siku. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi April 2020, wabia wa mradi walikuwa bado hawajafikia uamuzi wa mwisho wa uwekezaji katika mradi, pamoja na tarehe ya kukamilika kwa mradi huo.

⁷ https://drive.google.com/file/d/1BxWAK1A_hRq9sg3hBjEAnSdvvoHkX9Nu/view

⁸ https://drive.google.com/file/d/1BxWAK1A_hRq9sg3hBjEAnSdvvoHkX9Nu/view

⁹ National Environment Statistics Report (NESR, 2017) – Tanzania Mainland.

3.2 Mfumo wa Sheria na Udhibiti katika Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia

3.2.1 Sekta ya Madini

Shughuli za madini nchini Tanzania zinaongozwa na kusimamiwa na sera ya madini ya mwaka 2009, sheria ya madini ya mwaka 2010 na kanuni mbalimbali za madini. Mnamo mwaka 2017, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya marekebisho makubwa kwenye sheria ya madini kuitia kwenye sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali ya mwaka 2017. Vilevile, Serikali ilitunga sheria mpya kwa lengo la kuboresha usimamizi wa shughuli za sekta ya madini. Sheria hizo ni sheria ya mapitio na majadiliano kuhusu mikataba ya maliasili za nchi yenyе vifungu kandamizi ya mwaka 2017 na sheria ya mamlaka ya nchi kuhusu umiliki wa utajiri asilia na maliasili za nchi ya mwaka 2017. Utekelezaji wa sheria hizi umeleta mabadiliko chanya kwenye shughuli za sekta ya madini.

i. Sheria ya Madini ya Mwaka 2018

Shughuli za sekta ya madini nchini zinafanywa kwa mujibu wa sheria ya madini [Sura ya 123, R.E. 2018]. Sheria ya madini inatoa mwongozo katika maeneo ya mgawanyo na usajili wa haki za madini na utaratibu wa utoaji wa leseni za kushiriki katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini. Vilevile, sheria ya madini pia inaelekeza masuala ya mrabaha na ada zingine zinazopaswa kulipwa na waendeshaji wa sekta ya madini. Sheria pia inatoa mwongozo kuhusu masuala ya manufaa ya sekta ya madini kwa watanzania, wajibu wa kampuni za madini kwa jamii, kiapo cha uadilifu, na usuluhishi wa migogoro.

ii. Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010

Serikali ilifanya marekebisho makubwa kwenye sheria ya madini mwaka 2017 kwa lengo la kulinda maslahi ya watanzania na kuongeza faida ambazo nchi inastahili kuzipata kutoka kwenye sekta ya Madini. Marekebisho hayo yaliletwa kuitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 na sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali ya mwaka 2017. Marekebisho hayo ya sheria yaliongeza kiwango cha mrabaha kutoka asilimia nne hadi sita kwa madini yanayouzwa nje ya nchi kama dhahabu, shaba, fedha, na platinamu na kutoka asilimia tano hadi sita kwa madini ya vito na almasi. Kuongeza viwango vya mrabaha kulikusudiwa kuongeza mchango wa sekta ya madini katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Vilevile, marekebisho ya sheria yalianzisha ada ya ukaguzi (kama sharti jipya la kisheria) ambayo ni asilimia 1 ya thamani ya madini yote yanayosafirishwa. Ada hii ya ukaguzi ilianza kutozwa tarehe 1 Julai 2017.

Vilevile, marekebisho yaliweka sharti jipya kwenye muundo wa umiliki wa kampuni za Madini. Sharti hilo linawataka wamiliki wa Leseni za Madini au Leseni Maalum za Madini kuipatia serikali angalau asilimia 16 katika umiliki wa kampuni zao bila serikali kulazimika kuchangia mtaji. Sambamba na sharti hilo, marekebisho haya yanaipa

serikali haki ya kumiliki hadi asilimia 50 ya hisa katika kampuni za madini, kutegemea na thamani ya kodi ambayo kampuni ya madini inapaswa kuilipa serikali.

Marekebisho haya pia yameiwezesha serikali kuanzisha Tume ya Madini ambayo ilichukua nafasi ya Bodi ya Ushauri ya Madini. Tume ya Madini imepewa mamlaka ya kufanya kazi nyingine za ziada mbali na jukumu la ushauri ambalo lilikuwa jukumu kuu la Bodi ya Ushauri wa madini. Kazi hizi ni pamoja na (i) kutoa leseni, (ii) kudhibiti na kufuatilia sekta ya madini na utendaji wake, na (iii) kuhakikisha utafutaji na uchimbaji wa madini (pamoja na matumizi ya madini) unafanyika kwa kufuata utaratibu uliowekwa. Sambamba na majukumu hayo, Tume ya Madini pia imepewa mamlaka ya kutatua migogoro inayotokana na shughuli za madini na kufanya ukaguzi na uchunguzi juu ya masuala ya usalama katika sekta ya madini.

Kupitia marekebisho hayo, kuanzia tarehe 2 Machi 2017 serikali pia imezuia usafirishaji wa makinikia nje ya nchi yanayosaidikiwa kuwa na madini kama dhahabu, shaba, nikeli, na fedha. Tume ya Madini imepewa mamlaka ya kuchambua na kuthaminisha makinikia hayo ili yaweze kuchenjuliwa ndani ya nchi. Hatua hii ilikusudiwa kukuza shughuli za kuongeza thamani ya madini nchini. Kukua kwa kushughuli za kuongeza thamani ya madini kulitarajiwa kutengeneza ajira mpya, kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za madini, na kuchochea matumizi ya teknolojia ya kisasa kwenye sekta ya madini.

Marekebisho ya sheria hii pia yameweza vifungu vinavyoitaka sekta ya madini iwe na manufaa kwa watanzania. Vifungu hivyo vinawataka wamiliki wa leseni za madini kununua bidhaa na huduma (bima, huduma za kisheria, na kifedha) kutoka kwa kampuni za wazawa za ndani ya nchi. Utekelezaji wa namna sekta ya madini inavyopaswa kuwanufaisha wazawa hususani kwenye huduma za bima, huduma za kisheria na kifedha umebanishwa katika vifungu vya 30, 32, na 34 vya Kanuni za Madini (ushirikishwaji wa watanzania) za mwaka 2018.

Kwa upande wa huduma za kifedha, kanuni zinazitaka kampuni za madini kumiliki akaunti katika benki za Tanzania na kutumia huduma za kifedha kutoka taasisi za kifedha za kitanzania kwa miamala yote inayohusiana na shughuli za madini. Hata hivyo, kukiwepo na sababu za msingi, kampuni za madini zinaruhusiwa kutumia huduma za kifedha za taasisi za kigeni baada ya kupata idhini ya Tume ya Madini. Kwa mujibu wa kanuni hizi, benki ya kitanzania ni ile ambayo inamilikiwa na watanzania kwa asilimia mia moja au ambayo watanzania wanamiliki sio chini ya asilimia ishirini ya hisa zake.¹⁰

Sharti hili linazitaka kampuni za madini kusitisha uhusiano wao na taasisi za kifedha za kigeni na kupata huduma kutoka kwa taasisi za kifedha zilizoidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania. Hivyo, kampuni za madini zilipaswa kuhamisha akaunti zao za

¹⁰ <https://www.madini.go.tz/wp-content/uploads/2019/02/THE-MINING-LOCAL-CONTENTAMENDMENTS-REGULATIONS-2019 GN-NO-139-OF-2019.pdf>

kibashara kutoka benki za kigeni kwenda kwenye benki ambazo zinamilikiwa na Watanzania. Kwa bahati nzuri, benki zote kubwa zinazomilikiwa na wageni isipokuwa benki nane tu zimepewa leseni ya kufanya kazi nchini na hivyo kukidhi mahitaji yaliyowekwa katika Kanuni za Madini.

Kwa upande wa huduma za bima, kifungu cha 30 (1) na (2) cha Kanuni za madini kinazitaka kampuni za uchimbaji madini kutii masharti ya Sheria ya Bima na kukata bima zote zinazohusiana na shughuli za madini kutoka kampuni za bima za wazawa. Hata hivyo, kifungu cha 31 (1) kinampa Kamishna wa Bima mamlaka ya kuzipa kampuni za madini kibali cha kutumia huduma za bima kutoka kampuni za kigeni kukiwa na sababu za kipekee. Kwa mujibu wa kifungu cha 31 (2) idhini ya kutumia huduma za bima toka kwenye kampuni za kigeni itatolewa endapo Tume ya Bima ya Taifa itahakikisha kuwa kampuni za bima za ndani hazina uwezo wa kutoa huduma za bima zinazopaswa kutolewa na kampuni za kigeni.

Kwa upande wa huduma za kisheria, kifungu cha 32 cha kanuni kiwataka wakandarsi, wamiliki wa leseni za madini, au washirika wao kutumia huduma za kisheria kutoka kwa wanasheria au kampuni za wanasheria wa kitanzania ambao ofisi zao kuu ziko nchini. Vilevile, kanuni za madini zinatoza adhabu na faini ya hadi shilingi za kitanzania bilioni tano au kifungo cha hadi miaka mitano jela kwa kutofufata masharti yaliyowekwa katika sheria hii.

iii. Sheria ya Mapitio na Majadiliano Kuhusu Mikataba ya Maliasili za Nchi yenye Vifungu Kandamizi ya Mwaka 2017

Sheria hii inaipa Serikali fursa ya kupitia na kuanzisha upya majadiliano kuhusu makubaliano yaliyofikiwa kati ya serikali na kampuni za madini kabla ya kutungwa kwa sheria hii. Sehemu ya 4 na 6 ya sheria hii inatoa mamlaka kwa bunge kupitia makubaliano yaliyofanywa na serikali, na inapobidi kuielekeza serikali kujadili upya masharti yoyote yasiyokuwa ya kawaida hasa yale ambayo yanazuia uhuru wa nchi kwenye rasilimali zake.

iv. Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri Asilia na Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017

Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri Asilia na Maliasili za Nchi ya Mwaka 2017 imeweeka sharti kwamba migogoro inayohusiana na madini, mafuta na gesi asilia au matumizi ya maliasili na rasilimali inapaswa kusuluhishwa ndani ya nchi. Kabla ya kutungwa kwa sheria hii, kampuni za uziduaji na wadau wengine walikuwa na uhuru wa kuchagua sheria na mamlaka za kuhusishwa katika utatuzi wa migogoro. Sheria zingine zinazosimamia sekta ya uziduaji ni pamoja na Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, na marekebisho yake ya mwaka 2018; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004; na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, toleo la mwaka 1977.

Kufuatia mabadiliko ya sheria ya madini, serikali imetengeneza kanuni kadhaa zinazosaidia utekelezaji wa sheria mpya ya madini. Kanuni hizi ni pamoja na Kanuni za Madini (haki madini) za mwaka 2018, Kanuni za Madini (biashara ya madini na makinikia) za mwaka 2018, Kanuni za Madini (ushirikishwaji wa watanzania) za mwaka 2018 na mabadiliko yake, na Kanuni za Madini (madini mionzi) ya mwaka 2018. Kanuni nyingine ni pamoja na Kanuni za Madini (ongezaji thamani madini) za mwaka 2018, Kanuni za Madini (utafiti wa kijilojia) za mwaka 2018, Kanuni za Madini (ukaguzi na uchunguzi wa kumbukumbu za madini) za mwaka 2018 na Kanuni za Madini (eneo liliodhibitiwa la Mirerani) za mwaka 2019.

3.2.1.1 Mfumo wa Udhhibit wa Sekta ya Madini

Kwenye mfumo wa udhibiti wa sekta ya madini, Wizara ya Madini ndio taasisi ya juu inayodhibiti shughuli za madini nchini na ambayo inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Madini ya mwaka 2018. Vilevile, mwaka 2018, serikali ilifanya mabadiliko kwenye muundo na taasisi zinazodhibiti shughuli za madini. Mabadiliko hayo yaliivunja taasisi ya Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania kwa mujibu wa Amri ya Raisi ya kuuvunja Wakala huo ya mwaka 2018. Kufuatia kuvunjwa kwa wakala huo, majukumu yake kwa sasa yamerithiwa na Tume ya Madini, ambayo ilianzishwa chini ya Sheria ya Madini, Sura ya 123. Vilevile, mabadiliko hayo yalihusisha kuuvunja Wakala wa Utafiti wa Jiolojia kwa mujibu wa Amri ya Raisi ya kuuvunja Wakala huo ya mwaka 2018. Taasisi ya Jiolojia na utafiti wa madini Tanzania imeaanzishwa kuchukua nafasi ya Wakala wa Utafiti wa Jiolojia.

Kwa ujumla, mfumo wa udhibiti wa sekta ya madini umeundwa na taasisi kubwa saba. Taasisi hizi ni Wizara ya Madini, Wizara ya Maliasili na Utalii, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Tume ya Madini, na Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

i. Wizara ya Madini

Wizara ya Madini inasimamia shughuli za wachimbaji wakubwa na wadogo wa madini nchini. Wizara inawajibika kutoa leseni za madini, kutekeleza sheria na kanuni za uchimbaji madini, na kulinda mazingira kwenye maeneo ambayo shughuli za madini zinafanyika, ikiwa ni pamoja na kufanya ufuutiliaji na ukaguzi wa mazingira. Pia inawajibika kutatua migogoro inayotokana na shughuli za madini na kuratibu jitihada za wajibu wa kampuni za madini kwa jamii.

ii. Wizara ya Maliasili na Utalii

Wizara ya Maliasili na Utalii inasimamia sheria na kanuni za usimamizi wa rasilimali za misitu, uhifadhi wa misitu, na utalii. Pia inawajibika kutoa vibali vya kufanya shughuli za uchimbaji katika misitu na maeneo yaliyohifadhiwa.

iii. Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira

Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira limeundwa kwa madhumuni ya kutoa elimu ya mazingira na kuongeza uelewa kwa umma juu ya usimamizi wa mazingira. Pia linaishauri serikali juu ya masuala ya mazingira na kufanya ukaguzi wa mazingira katika sekta zote. Baraza pia lina jukumu la kuhakikisha sheria na kanuni za mazingira zinafuatwa na hatua za kudhibiti uchafuzi wa mazingira zinatekelezwa. Katika sekta ya madini, Baraza la Mazingira ni chombo muhimu cha kuhakikisha shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini ni rafiki kwa mazingira.

iv. Mamlaka ya Mapato Tanzania

Mamlaka ya Mapato Tanzania inawajibika kusimamia sheria za kodi kwa madhumuni ya kutathmini, kukusanya, na kusimamia mapato yote kwa mujibu wa sheria.

v. Tume ya Madini Tanzania

Tume ya Madini imeanzishwa kutekeleza majukumu ya kiutendaji ambayo awali yalikuwa zikifanywa na Idara ya Madini iliyokuwepo chini ya Wizara ya Nishati na Madini na kazi zilizokuwa zikifanywa na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania na TANSORT. Vilevile, Tume inawajibika kumshauri Waziri wa madini juu ya mambo yote yanayohusiana na sekta ya madini. Uamuvi wa kuanzisha Tume ya Madini ulilenga kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini na kuhakikisha kuwa serikali inafaidika na mapato yanayotoka na sekta hii.

vi. Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia

Taasisi ya Uhamasishaji Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia ilianzishwa kwa lengo la kuhamasisha uwazi na uwajibikaji katika mtiririko wa mapato kutoka kwenye sekta ya madini, mafuta na gesi asilia . Taasisi hii inafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya TEITA ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2019. Sheria ya TEITA na kanuni zake zimeipa nguvu taasisi hii kuomba na kuchapisha taarifa za kifedha, uzalishaji, na umiliki wa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zinazofanya kazi hapa nchini.

3.2.2 Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia

Mfumo wa kisheria wa sekta ya mafuta na gesi asilia ndio muhimili mkuu wa maendeleo endelevu ya sekta ya mafuta na gesi asilia. Sera, sheria, na kanuni zinazongoza sekta ya mafuta na gesi asilia nchini ni pamoja na Sera ya Taifa ya Gesi Asilia ya 2013, Sera ya Nishati ya mwaka 2015, na Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996. Kwa upande wa sheria ni pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2015, Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, na Kanuni za Petroli (Ushirikishwa wa Watanzania) za mwaka 2017. Kwa upande mwingine, shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia zinaongozwa na muongozo wa makubaliano ya kushirikiana katika uzalishaji wa mafuta wa mwaka 2013.

i. Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015

Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 inashughulika na masuala muhimu yafuatayo:

- Marekebisho ya Kampuni ya Taifa ya Nishati: Sera ya nishati inapendekeza kampuni hii igawanywe kuwa kampuni huru za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati. Hata hivyo, hadi sasa pendelezo hili la kisera halijatekelezwa. Kampuni ya Nishati ya Taifa bado inaendelea kufanya kazi tatu za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati.
- Kuweka kipaumbele kwa soko la ndani kwenye matumizi ya bidhaa za mafuta na gesi asilia: Sera inaweka msisitizo kuwa bidhaa za mafuta na gesi asilia zipewe kipaumbele cha kuuzwa kwenye soko la ndani kuliko masoko ya nje kwa madhumuni ya kukuza matumizi ya bidhaa za mafuta na gesi asilia ndani ya nchi.
- Kukusanya rasilimali fedha ili kuendeleza miradi ya nishati: Sera ya nishati inabainisha umuhimu wa kukusanya rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango na miradi ya nishati. Kupitia sera hii, serikali inakusudia kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ili kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya nishati.
- Bei ya Nishati: Kupitia sera hii, serikali inakusudia kuwa na bei nzuri ya nishati itakayochocha ukuaji endelevu wa sekta ya nishati. Hata hivyo, utekelezaji wa azma hii ya kisera unakabiliwa na changamoto kama kubadilika na kushuka kwa viwango vya ubadilishaji fedha, mfumuko wa bei, na uwezo mdogo wa kipato wa watumiaji wa nishati.
- Ubia wa sekta ya umma na binafsi: Sera inahimiza ubia kati ya sekta binafsi na za umma katika kuleta ukuaji wa haraka wa sekta ya nishati. Vilevile, sera inalenga kuhakikisha uwepo wa miundombinu sahihi na utapitakanaji wa ralisilimali fedha za kugharamia miradi ya ubia katika sekta ya nishati.

Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 pia imezingatia masuala muhimu ambayo yaliyokuwepo katika Sera ya Taifa ya Gesi Asilia (NNGP) ya mwaka 2013 na sera ya ushirikishwaji wa watanzania kwenye sekta ya mafuta na gesi ya mwaka 2014.

ii. Sera ya Uwekezaji wa Taifa ya mwaka 1996

Msisitizo wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996 ni kukuza, kuvutia, na kuwezesha uwekezaji wa moja wa moja wa kigeni katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya madini, mafuta na gesi asilia. Kwa kuwa uwezo wa makampuni ya ndani kushiriki katika shughuli za madini, mafuta na gesi asilia ni mdogo, sera ya uwekezaji inaweka mazingira mazuri kwa kampuni za kigeni kuwekeza nchini.

iii. Sheria ya Mafuta ya Petroli ya Mwaka 2015

Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 imetoa mwogozo wa udhibiti wa shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchakataji, na usambazaji wa mafuta na gesi asilia. Sehemu ya 11 ya sheria hii inaunda Mamlaka ya Udhibiti wa uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Vivyo hivyo,

kifungu cha 8 cha sheria hiyo kinanzisha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kama Kampuni ya Taifa ya Mafuta. Kwa mujibu wa sheria hii, shirika hili limepewa haki za kipekee za kununua, kukusanya na kuuza mafuta na gesi asilia kutoka kwa wazalishaji. Vilevile, sheria ilimelipa shirika mamlaka ya kumiliki hisa zisizopungua asilimia 25 kwa kila mradi wa mafuta na gesi asilia unaofanywa nchini Tanzania. Sheria pia imeiruhusu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuunda kampuni tanzu zinazoweza kutekeleza shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Kwa kuongezea, Sheria hii imeanzisha Ofisi ya Mafuta na Gesi chini ya ofisi ya Rais ili kulishauri Baraza la Mawaziri kuhusu masuala ya kimkakati ya uchumi wa mafuta na gesi asilia.

iv. Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya Mwaka 2015

Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015 ndiyo sheria kuu inayosimamia mapato yanayopatikana kutoka katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Sheria imeanzisha mfuko wa mafuta na gesi ili kuongeza ustawi wa kiuchumi, uwekezaji, kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kulinda rasilimali hii kwa ajili vizazi vijavyo. Mfuko wa mafuta na gesi unapokea michango kutoka kwenye vyanzo vya fedha kama mrabaha, faida ya serikali, gawio, na kodi ya mapato inayotozwa kwenye shughuli za utafutaji, uzalishaji na uendelezaji wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia.

v. Kanuni za Mafuta ya Petroli (Ushirikishwaji wa Watanzania) za Mwaka 2017

Kanuni za Petroli (Ushirikishwaji wa Watanzania) za mwaka 2017 zinatoa muongozo kwa serikali kuhusu namna ya kunufaisha wazawa na nchi kutoka kwenye miradi ya mafuta na gesi asilia nchini. Kanuni zinalenga kuhamasisha ukuaji wa ajira kuitia ushiriki wa wataalam wa ndani na matumizi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini. Vilevile, kanuni zinatoa muongozo kuhusu jamii inavyoweza kushiriki na kuchangia katika ukuaji wa sekta ya mafuta na gesi asilia.

vi. Muongozo wa Makubaliano ya Ushikirikiano kwenye Uzalishaji wa Mafuta na Gesi wa Mwaka 2013

Muongozo wa Makubaliano ya Ushikirikiano kwenye Uzalishaji wa Mafuta na Gesi unatumika kuongoza majadiliano kati ya kampuni za mafuta na gesi asilia za kigeni, Serikali, na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Muongozo unaweka masharti ya shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia. Chini ya Muongozo huu kampuni za utafutaji na uzalishaji zinabeba gharama za uendeshaji na kisha kuzifidia kutoka kwenye faida itokanayo na mapato ya mafuta na gesi asilia kabla ya kugawana na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Vipengele muhimu kwenye Muongozo vyenye manufaa kwa nchi ni pamoja na umiliki wa serikali wa kuanzia asilimia 25 kwenye vitalu vya gesi, mrabaha kutokana na uzalishaji wa gesi, na kodi kutoka kwenye faida iliyopatikana. Muongozo wa Makubaliano ya Ushikirikiano kwenye

Uzalishaji wa Mafuta na Gesi wa 2013 unasisitiza utoaji mafunzo na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa ndani kwa kuweka sharti la kutenga kila mwaka kiasi kisichopungua dola za kimarekani 500,000 kwa ajili ya mafunzo ya kwa wafanyakazi. Kwa ujumla, Muongozo unatoa msukumo kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kupata mafanikio kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia.

vii. Sheria ya TEITA ya Mwaka 2015

Sheria ya TEITA ya mwaka 2015¹¹ ilitungwa ili kuhakikisha uwepo wa uwazi na uwajibikaji wa taasisi na makampuni yanayofanya shughuli katika sekta ya madini, mafuta na gesi asilia . Kifungu cha 4 cha sheria hii kinaiunda Kamati ya TEITI, ambayo inasimamia na kukuza uwazi na uwajibikaji katika sekta hii. Utaratibu wa namna Kamati ya TEITI inatekeleza majukumu yake unaelezwu katika kifungu cha 5 hadi 10 cha sheria hii. Vilevile, vifungu namba 10 (1) (b) na (c) vya sheria hii vinaipa mamlaka Kamati kuomba na kupewa taarifa kutoka kwa makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia kuhusiana na shughuli zao.

Kwa kuongezea, kifungu cha 15 (1) hadi (3) cha sheria hii kimeweka sharti kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kutoa taarifa juu manufaa yatolewayo kwa watanzania, wajibu wa makampuni kwa jamii, na ghamama za uwekezaji katika uendeshaji. Vivyo hivyo, kifungu cha 16 (1) (a) na (b) kinaitaka Kamati ya TEITI ichapishe taarifa za kampuni za madini, mafuta na gesi asilia, pamoja na kuweka wazi mikataba na wamiliki wanufaika wa kampuni hizo. Sehemu ya 23 ya sheria hii inaweka adhabu kwa watu binafsi na makampuni yatakayoshindwa kutoa nyaraka au taarifa zinazohitajika kutolewa. Mtu binafsi atalipa faini ya hadi shilingi milioni 10.0 wakati kampuni italipa faini isiyozidi shilingi milioni 150 za kitanzania.

viii. Kanuni za Sheria ya TEITA za Mwaka 2019

Kanuni za sheria za TEITA za mwaka 2019¹² zimeandaliwa kusaidia utekelezaji wa Sheria ya TEITA ya mwaka 2015. Kanuni hizi zinatoa mwongozo kuhusu utunzaji wa kumbukumbu za shughuli za madini, mafuta na gesi asilia zinazofanywa na makampuni (kanuni ya 3), uwasilishaji wa taarifa (kanuni ya 4), uthibitishaji wa taarifa (kanuni ya 9), utoaji wa taarifa za wamiliki wanufaika (kanuni ya 12), na namna ya kushugulikia taarifa za siri (kanuni ya 13).

3.2.2.1 Mfumo wa Udhibiti wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia

Sekta ya mafuta na gesi asilia inasimamiwa na kudhibitiwa na taasisi tano kuu. Taasisi hizi ni Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Udhibiti wa Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, na Benki Kuu ya Tanzania.

¹¹ <http://parliament.go.tz/polis/uploads/bills/acts/1452053429-ActNo-23-2015-Book-21-25.pdf>

¹² <https://www.madini.go.tz/wp-content/uploads/2019/02/TEITA-REGULATIONS-GN-NO.141-OF-2019.pdf>

i. Wizara ya Nishati

Wizara ya Nishati ni msimamizi mkuu wa masuala ya nishati na ina jukumu la kuratibu na kutengeneza sera, sheria, na kanuni zinazosaidia kuleta maendeleo endelevu ya sekta ya mafuta na gesi asilia. Mbali na jukumu hili nyeti, wizara pia inawajibika kusimamia taasisi zilizo chini ya mamlaka yake. Taasisi hizi ni pamoja na Shirik aloa Maendeleo ya Petroli Tanzania, Mamlaka ya Udhiliti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Umeme Tanzania, na Wakala wa Nishati Vijiji.

ii. Wizara ya Fedha na Mipango

Wizara ya Fedha na Mipango ina jukumu la kuimarisha uwazi na matumizi sahihi ya mapato yanayozalishwa kutoka sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya nishati. Wizara pia ina jukumu la kutengeneza sera ambazo zinalenga kukuza pato la taifa kwa kukuza uzalishaji wa nishati mbadala kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia. Vilevile wizara, kuititia Mamlaka ya Mapato inakusanya kodi ya ongezeko la thamani na kutoa misamaha ya kodi kwenye vifaa vinavyotumika kuhifadhi, kusafirisha nje, na kusambaza gesi asilia.

iii. Mamlaka ya Udhiliti wa Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia

Mamlaka ya Udhiliti na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ilianzishwa chini ya kifungu namba 11 cha Sheria ya Petroli ya 2015. Jukumu kuu la mamlaka hii ni kudhibiti na kufuatilia shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia Tanzania Bara na kutoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa serikali na kwa waziri nishati.

iv. Mamlaka ya Udhiliti wa Huduma za Nishati na Maji

Mamlaka ya Udhiliti wa Huduma za Nishati na Maji imepewa jukumu la kudhibiti masuala yote ya kiufundi na kiuchumi kwenye sekta ndogo ya umeme, mafuta, gesi asilia, na maji nchini Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya EWURA, sura ya 414 ya mwaka 2006 na mabadiliko yake ya mwaka 2019. Mamlaka pia inawajibika kukuza ushindani na ufanisi wa kiuchumi, kulinda maslahi ya watumiaji, na kukuza upatikanaji wa huduma zinazodhibitiwa kwa watumiaji wote.

v. Benki Kuu ya Tanzania

Benki Kuu ya Tanzania inashiriki katika shughuli za sekta ya mafuta na gesi kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Gesi Asilia ya 2013. Wajibu mkuu wa Benki Kuu kwenye sekta ya mafuta na gesi ni kuandaa taratibu za kifedha zinazolenga kuzuia mfumko wa bei. Sera hii pia inaitaka Benki Kuu kuhakikisha kuwa shughuli za uziduaji hazileti athari hasi kwenye udhibiti wa fedha na uchumi wa nchi.

3.3 Mfumo wa Utawala wa Kodi na Malipo

3.3.1 Sekta ya Madini

Serikali ya Tanzania inakusanya mapato kutoka kwenye makampuni ya madini kupitia kodi, ada, na tozo mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2018. Jedwali namba 4 linawasilisha muhtasari wa kodi na malipo mbalimbali yanayotozwa na serikali kutoka kwenye sekta ya Madini.

Jedwali Na. 4: Aina za Malipo katika Sekta ya Madini

Na	Aina ya Malipo	Maelezo
1	Mrabaha	Kampuni za madini zinapaswa kulipa mrabaha kwa Wizara ya Madini kwa mujibu wa Sheria ya Madini. Kuanzia mwezi Julai 2017, marekebisho yaliyofanywa kwenye Sheria ya Madini inazitaka kampuni za madini kulipa mrabaha wa asilimia 6 kwa madini ya almasi, vito, na metali kama shaba, dhahabu, fedha na platinamu.
2	Ada ya Ukaguzi	Mabadiliko ya sheria ya madini inazitaka kampuni za madini kulipa asilimia 1 ya thamani ya mauzo yote ya madini kwa Wizara ya Madini kama ada ya ukaguzi.
3	Umiliki wa Kampuni Usiochangia Mtaji	Mabadiliko ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017 yameanzisha sharti la serikali kuwa sehemu ya wamiliki wa makampuni yenye leseni au leseni maalum za kuchimba madini kwa kiwango kisichopungua asilimia 16 bila ya kuwekeza mtaji kwenye kampuni husika.
2	Kodi ya Makampuni	Kampuni za madini, mafuta na gesi zinapaswa kulipa kodi ya makampuni kwa kiwango cha asilimia 30 ya mapato yanayopaswa kulipiwa kodi
3	Kodi ya Ongezeko la Thamani	Kodi ya Ongezeko la Thamani inatozwa kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma kwa kiwango cha asilimia 18. Wauzaji wote wa bidhaa na huduma wenyе mauzo ya angalau shilingi za kitanzania milioni 40 lazima wasajiliwe kwa ajili ya kodi hii. Katika sekta ya madini, makampuni za madini hulipwa marejesho ya kodi hii kwa madini yanaliyosafirishwa nje ya nchi. Hata hivyo, marekebisho ya sheria yamefuta marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye usafirishaji wa makinikia nje ya nchi.
5	Punguzo la Uchakavu kwenye Rasilimali katika Shughuli za Madini.	Kiambatisho cha tatu cha Sheria ya Ushuru na Mapato, Sura ya 233 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Fedha 2016 iliweka punguzo la uchakavu kwenye rasilimali katika shughuli za madini kwa kiwango cha asilimia 20 kwa kipindi cha miaka mitano.
6	Hasara Inayofidiwa	Ikiwa kampuni itapata hasara kwenye shuguli za biashara zake, inaruhusiwa kuondoa kiasi hicho cha hasara toka kwenye mapato ya mwaka unaofuata kwa muda wa miaka mitano mfululizo, lakini kuanzia mwaka wa tatu kampuni itatozwa ushuru kwa kiwango cha asilimia 0.3 cha mauzo.
7	Kodi ya Zuio kwenye Mapato ya Gawio.	Kwa mujibu wa sheria ya kodi ya mwaka 2004, Sura ya 233, kampuni za madini zinapaswa kulipa kodi ya zuio kwenye mapato ya gawio kwa kiwango cha asilimia 5 ikiwa zinapokea gawio kutoka kwenye kampuni zilizosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam. Vilevile, kampuni zinapaswa kulipa kodi ya zuio kwenye mapato ya gawio kwa kiwango cha asilimia 10 ikiwa zinapokea gawio kutoka kwenye kampuni zingine zisizosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.
8	Kodi ya Zuio kwenye Riba ya Mikopo ya Nje.	Kwa mujibu wa sheria, kampuni za madini zinapaswa kulipa kodi ya zuio kwenye riba ya mikopo ya nje kwa kiwango cha asilimia 10. Riba isiyokuwa imelipwa miaka ya nyuma inatambulika kama malipo halali, hivyo nayo pia itatozwa kodi ya zuio.
9	Kodi ya Zuio kwenye Malipo ya Huduma za	Kodi ya zuio itatozwa kwa kiwango cha asilimia 5 kutoka kwenye malipo ya huduma za kitaalam au ada za menejiment zinazolipwa kwa mtu binafsi au kampuni ya kitanzania au kwa kiwango cha asilimia 15 kama zinalipwa kwa

Na	Aina ya Malipo	Maelezo
	Kitaalam na Ada za Menejimenti.	mtu binafsi au kampuni za kigeni. Hata hivyo, kampuni zilizosaini makubaliano ya uendelezaji vitalu nya madini kabla ya mwaka 2014, zitalipa kodi ya zuio kwa kiwango cha asilimia 3.
10	Ushuru wa Forodha kwenye Vifaa na Vitendea Kazi nya Madini	Kwa mujibu wa Sheria ya forodha, kampuni za madini au washirika wake hawatalipa ushuru wa forodha kwenye mwaka wa kwanza wa shughuli za utafutaji wa madini. Baada ya mwaka wa kwanza, watalipa ushuru wa forodha kwa kiwango kisichozi asilimia 5.
11	Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mtaji	Kwa mujibu wa sheria, makampuni ya madini yanawajibika kulipa kodi ya ongezeko la thamani ya mtaji kwa kiwango cha asilimia 30.

3.3.2 Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia

Kama ilivyo katika sekta ya madini, Serikali ya Tanzania inakusanya mapato kutoka kwa makampuni ya mafuta na gesi kupitia kodi, ada, ushuru, na tozo nyingine kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Mapato, ya mwaka 2004, Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015, na muongozo wa makubaliano ya ushirikiano kwenye uzalishaji wa mafuta na gesi asilia ya mwaka 2013. Jedwali namba 5 linawasilisha muhtasari wa kodi na malipo mbalimbali yanayotozwa na serikali kutoka kwenye sekta ya mafuta na gesi.

Jedwali Na. 5: Aina za Malipo Kwenye Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia

Na	Aina ya Malipo	Maelezo
1	Mrabaha	<ol style="list-style-type: none"> 1. Mrabaha kutoka kwenye uzalishaji wa mafuta na gesi unalipwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kama ilivyo elekezwa kwenye sehemu ya 113 ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015. Mrabaha unatozwala kulingana na eneo uzalishaji unaofanyika. Mrabaha kwa uzalishaji unaofanywa kwenye eneo la pwani ya bahari ni asilimia 12.5 na kwenye eneo la ndani ya bahari ni asilimia 7.5. 2. Kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 na muongozo wa makubaliano ya ushirikiano kwenye uzalishaji wa mafuta na gesi, mrabaha utalipwa kutoka kwenye uzalishaji ghafi kabla kiwango kilichozaishwa hakijagawanywa kwa wabia.
2	Kiwango cha Kufidia Gharama	Kampuni za mafuta na gesi zinaruhusiwa kufidia gharama za uzalishaji kwa kiwango cha asilimia 50 kwa kipindi chote. Hata hivyo, muongozo wa masharti ya gesi unaruhusu kufidia gharama kwa kiwango cha asilimia 70. Faida toka kwenye hidrokaboni inagawanya kulingana na ujazo uliozalishwa.
3	Faida toka kwenye Mapato ya Mafuta au Gesi	Faida hii inapatikana baada ya kutoa mrabaha na gharama za uzalishaji kwenye mapato ghafi ya mafuta au gesi asilia. Faida inayopatikana inagawanywa katika ya Kampuni ya mafuta ya Taifa, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (kwa niaba ya serikali), na kampuni iliyozaishwa kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa awali kuhusu mgawanyo wa faida. Makubaliano ya ushirikiano kwenye uzalishaji wa mafuta na gesi ya mwaka 2013 yamependekeza viwango vya hiyari vya mgawanyo wa faida.
4	Kodi kwenye Faida ya Ziada	Kodi kwenye faida ya ziada hulipwa na kampuni za mafuta na gesi kwa mujibu wa kipengele namba 17 cha Muongozo wa Makubaliano ya Ushirikiano kwenye Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2013 na hukokotolewa kwa kuzingatia eneo la kitalu cha mafuta au gesi cha kampuni husika. Ulipaji wa kodi kwenye faida ya ziada ni jukumu la kimkataba na sio kwa mujibu wa sheria za kodi. Kampuni zitalipa kodi hii kwa kiwango cha asilimia 25 kwenye mkusanyiko wa kwanza wa fedha taslimu na kwa kiwango cha asilimia 35% kwenye mkusanyiko wa pili wa fedha taslimu.

Na	Aina ya Malipo	Maelezo
5	Kodi ya Mapato	<p>1. Kampuni za mafuta na gesi zinapaswa kulipa kodi ya makampuni kwa mujibu wa sheria ya kodi na mapato.</p> <p>2. Endapo kampuni inamiliki zaidi ya kampuni moja, kila kampuni ina wajibika kulipa kodi yake yenyewe.</p> <p>3. Kampuni ya kitanzania itatozwa kodi kwa kiwango cha asilimia 30 toka kwenye kipato kilichopatikana popote duniani na kampuni ya kigeni italicpa asilimia 30 toka kwenye kipato kilichopatikana kwenye shughuli zake hapa nchini. Kampuni mpya italicpa kodi ya asilimia 25 kama imesajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam na angalau asilimia 30 kama hisa zake zinamiliikiwa na umma.</p>
6	Kodi ya Faida ya Tawi	Kodi ya Faida ya Tawi inatozwa kwenye mapato yanayosafirishwa nje ya nchi. Mapato yanayosafirishwa nje ya nchi yanakokotolewa na kanuni mahsus kwa kuzingatia mienendo katika hesabu mizania ya tawi.
7	Kodi ya Zuio	Kodi ya zuio hutozwa kwa kiwango cha asilimia 5 kutoka kwenye malipo ya watoa huduma za kitaalam au huduma za menejimenti kutoka kwa wazawa. Mapato ya gawio hutozwa kodi ya zuio ya asilimia 10. Lakini, kama gawio linalipwa kutoka kwenye kampuni iliyosajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam au asilimia 25 ya hisa za kampuni zinamiliikiwa na wazawa, kodi ya zuio itakuwa ni asilimia 5.
8	Ada ya Mwaka ya Kitalu	<p>Kampuni za mafuta na gesi hulipa ada ya kitalu inayozingatia mfumuko wa bei kwa dola za kimarekani (kwa mujibu wa Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano katika Uchimbaji wa Mafuta na Gesi wa Mwaka 2013) kama ifuatavyo:</p> <ul style="list-style-type: none"> i. Dola za kimarekani 50 kwa kilomita za mraba wakati wa kipindi cha awali cha utafutaji mafuta au gesi. ii. Dola za kimarekani 100 kwa kilomita za mraba wanapopewa nyongeza ya muda wa utafutaji kwa mara ya kwanza; na iii. Dola za kimarekani 200 kwa kilomita za mraba wanapopewa nyongeza ya muda wa utafutaji kwa mara ya pili.
9	Msamaha wa Ushuru wa Forodha	Vifaa na vitendea kazi vinavyoingizwa nchini kutoka nje ya nchi kwa ajili ya shughuli za utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi asilia vitasamehewa ada zote na ushuru wa forodha. Hata vinaporudishwa tena nje ya nchi havitatozwa kodi au ushuru ya mauzo ya nje. Wataalamu wa nje watapewa msamaha huu wa kodi kwa vifaa vyao binafsi.
10	Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Mtaji	Kodi ya ongezeko la thamani ya mtaji inatozwa endapo kuna mabadiliko ya muundo wa umiliki wa kampuni au kampuni ikiongeza rasilimali. Uhamishaji wa hisa ambaa unaleta ongezeko la thamani ya mtaji utatozwa kodi kwa kiwango cha asilimia 30 ya mauzo ya hisa. Kuanzia mwaka 2012, uhamishaji wa hisa usio wa moja kwa moja unatozwa kodi ya ongezeko la thamani ya mtaji. Mabadiliko ya umiliki wa kampuni kwa asilimia 50 yanatambulika kama rasilimali au deni hivyo hutozwa kodi ya ongezeko la thamani ya mtaji.
11	Kodi ya Ongezeko la Thamani	Kodi ya Ongezeko la Thamani hutuzwa kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma kwa kiwango cha asilimia 18. Wauzaji wote wa bidhaa na huduma wenye mauzo ya angalau shilingi milioni 40 lazima wasajiliwe kwa ajili ya kulipa kodi hii. Kampuni za utafutaji wa mafuta na gesi zimesamehewa kulipa kodi hii kwa kiwango kilicho ainishwa kwenye Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano Katika Uchimbaji wa Mafuta na Gesi wa Mwaka 2013.
12	Bonasi	Makampuni ya kigeni ya mafuta na gesi yanalipa aina mbili za bonasi ambazo ni ya saini na uzalishaji. Hizi ni kodi ambazo hulipwa kabla ya uzalishaji kwa serikali. Bonasi hizi zilianzishwa na kipengele cha 11(c) kwenye kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano ya ushirikiano katika uchimbaji wa mafuta na gesi wa mwaka 2013 lakini pia zimeainishwa kwenye sehemu ya 115 na 116 ya Sheria ya Petroli. Bonasi ya saini inalipwa kwa kiwango kisichopungua dola za kimarekani milioni 2.5 na bonasi ya uzalishaji ni dola za kimarekani

Na	Aina ya Malipo	Maelezo
		zisizopungua millioni 5. Kwa mujibu wa mkataba wa wa makubaliano ya ushirikiano katika uchimbaji wa mafuta na gesi, bonasi hizi hazifidiwi lakini hutolewa kabla ya kukokotoa kodi inayopaswa kulipwa na kampuni.
13	Kodi ya Uzio	Kodi ya Uzio imeanzhishwa ili kutenganisha mapato na hasara yatokanayo na shughuli za uendeshaji mbalimbali katika sekta ya mafuta na gesi. Gharama za kimkataba zinakuwa halali kama zipo ndani ya eneo la linalotambuliwa na mkataba uliosainiwa na gharama za kimkataba zitakazofidiwa lazima ziwe ziliingiwa kabla ya kuanza kwa uzalishaji wa mafuta na gesi asilia.
14	Miamala baina ya Makampuni yaliyo chini Umiliki Mmoja	Shughuli zote baina ya kampuni za madini na mafuta zinapaswa kuzingatia kanuni ya uwiano. Kanuni hii inazitaka kampuni zilizopo chini ya umiliki mmoja kufanya miamala baina yao kwa uhuru lakini kwa kuzingatia usawa. Wizara ya Fedha na Mipango imetoa kanuni za miamala ya kampuni zenye umiliki mmoja ili kusaidia utekelezaji wa kipengele kilichopo kwenye sheria ya kodi ya mapato kuhusu miamala ya aina hiyo. Mkataba wa Makubaliano ya Ushirikiano katika Uchimbaji wa Mafuta na Gesi wa Mwaka 2013 umeweka kanuni za miamala ya kampuni zenye umiliki mmoja ambazo hutumika wakati wa kugawanya faida itokanayo na shughuli za mafuta na gesi na wakati wa kukokotoa kiasi cha gharama zinazopaswa kufidiwa.
15	Ada ya Mafunzo na Utafiti	Makampuni yanayofanya kazi kwenye sekta ya mafuta na gesi hulipa kiasi cha dola za kimarekani 500,000 kama ada ya mafunzo na utafiti kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kama mchango wa kuendeleza utaalamu wa sekta ya mafuta na gesi.

3.4 Mchango wa Sekta ya Madini, Mafuta Na Gesi Asilia kwenye Uchumi

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, sekta ya uchimbaji madini na mawe inahusisha uchimbaji wa makaa ya mawe na lignite na uchimbaji wa mboji, mafuta ya ghafi, na gesi asilia, uchimbaji wa madini ya chuma na madini mengine.¹³ Kwa hivyo, takwimu zilizowasilishwa katika sehemu zifuatazo hapo chini zinajumuisha mchango wa jumla wa sekta hii katika uchumi.

3.4.1 Mchango wa Sekta Kwenye Pato la Taifa

Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia inachangia kwenye uchumi wa Tanzania kwa njia mbalimbali. Mnamo mwaka 2016 na 2017, mchango wa sekta ya madini, mafuta na gesi asilia kwenye pato la taifa ulikuwa asilimia 4.8 kwa kila mwaka kama ilivyooneshwa katika Jedwali namba 6. Kwa ujumla, mchango wa mapato wa sekta hii umekuwa ukiongezeka kama inavyoonekana katika jedwali hilo. Katika miaka tajwa hapo juu, sekta hiyo ilichangia TZS trilioni 4.98 na TZS trilioni 5.56, kwa kila mwaka.

Jedwali Na. 6: Mchango wa Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia Katika Pato la Taifa

Mwaka	Kiasi (TZS milioni)	Mchango wa Kisekta %
2016	4,975,991	4.8%
2017	5,560,120	4.8%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu¹⁴

¹³ https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/na/Highlights_for_the_Second_Quarter_GDP_2019.pdf

¹⁴ https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/na/Highlights_for_the_Second_Quarter_GDP_2019.pdf

Kwa kuongezea, Pato la Taifa na Sekta, Asilimia Shiriki katika pato la taifa kwa Bei za Sasa, Tanzania Bara ni kama inavyoonekana katika Jedwali namba 7.

Jedwali Na. 7: Pato la Taifa kwa Sekta (kwa Bei ya Sasa)

Sekta	2016 (Asilimia)	2017 (Asilimia)
Mazao	15.6	17
Mifugo	7.7	6.9
Misitu na Uwindaji	3.9	4
Uvubi	2	2.2
Madini, mafuta na gesi asilia	4.8	4.8
Viwanda	4.9	5.5
Umeme na Usambazaji	0.8	0.5

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania (2018)

3.4.2 Mchango wa Sekta Kwenye Ajira

Kulingana na Utafiti wa ajira na kipato wa mwisho wa mwaka 2016 uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, sekta ya madini, mafuta na gesi asilia iliajiri watu wapatao 35,900 (ajira za kawaida) ambayo ni sawa na asilimia 1.4 ya wafanyakazi wote nchini.¹⁵ Viwango vya ajira katika sekta hii vimeonesha ukuaji kidogo ikilinganishwa na mwaka 2015, ambapo jumla ya ajira kutoka sekta hii ziliwa 30,259 ambayo ni sawa na asilimia 1.3 ya jumla ya ajira katika sekta zote za uchumi.¹⁶

3.5 Uzalishaji na Uuzaji wa Madini, Mafuta na Gesi Asilia Nje

Sehemu hii inatoa taarifa kuhusu uzalishaji na uuzaji wa madini, mafuta na gesi asilia nje ya nchi. Katika shughuli za uchimabji mafuta, Tanzania haijawahi kupata maliasili hii mpaka sasa. Kifupi mpaka sasa hakuna takwimu zozote kutoka mamlaka mbalimbali zikionesha kiasi cha mafuta yaliyowahi kuchimbwa na kusafirishwa/kuuzwa nje ya nchi. Hata hivyo, Tanzania imezalisha na kusafirishaji kiasi kikubwa cha madini nje ya nchi. Vilevile, hadi leo, nchi imezalisha kiasi kikubwa cha gesi asilia kama inavyoonyeshwa katika sehemu zifuatazo.

3.5.1 Uzalishaji na Uuzaji wa Madini Nje

(i). Uzalishaji wa Madini

Jedwali namba 8 hapo chini linawasilisha takwimu za uzalishaji wa madini katika mwaka wa fedha 2016/17. Kwenye jedwali hili, inaonesha uzalishaji wa madini ulikuwa na jumla ya thamani ya TZS trilioni 4.78. Uzalishaji wa dhahabu uliongoza aina nyingine za madini kwa kuwa na thamani ya TZS trillioni 3.2.

Jedwali Na. 8: Uzalishaji wa Madini katika Mwaka wa Fedha 2016/17

Aina ya Madini	Kipimo	Bei kwa Kipimo	Jumla (Uzito)	Thamani (TZS)
Dhahabu	kilo	73,502,684.91	43,759.99	3,216,476,759,838.89
Almasi	kilo	549,278.63	249,911.05	137,270,798,016.00
Fedha	karati	1,275,427.85	14,767.64	18,835,053,622.27

¹⁵ https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/labour/EES_2016_REPORT.pdf

¹⁶ https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/labour/EES_2015_REPORT.pdf

Aina ya Madini	Kipimo	Bei kwa Kipimo	Jumla (Uzito)	Thamani (TZS)
Shaba	ratili	5,231.25	10,395,693.40	54,382,519,484.83
Mawe Chokaa	tani	116,892.51	4,004,241.73	468,065,849,169.00
Chumvi	tani	97,535.73	148,637.80	14,497,495,848.57
Mchanga/Udongo/Udongo Mwekundu	tani	16,960.39	4,646,806.23	78,811,655,123.52
Jasi (Gypsum)	tani	63,147.28	181,080.34	11,434,730,549.75
Aggregates	tani	23,906.68	6,070,808.37	145,132,887,071.66
Marumaru	tani	148,753.59	255,568.95	38,016,799,406.29
Bati	tani	17,343.36	180,064.80	3,122,928,741.49
Kaolin	tani	101,215.92	2,326.80	235,509,204.23
Galena	kilo	5,235.60	185,231.00	969,795,423.60
Bauxite	tani	141,928.08	8,299.00	1,177,861,111.87
Tanzanite	karati	6,538,260.43	8,817.88	57,653,579,442.60
Makaa ya Mawe	tani	87,496.29	429,709.85	37,598,019,450.90
Vito vya Mawe Vingine	tani	47,154.04	1,589,732.59	74,962,321,927.47
Phosphates	tani	97,773.00	213,306.00	20,855,567,114.26
Dolomite	tani	21,147.48	6,836.47	144,574,090.49
Pozzolana	tani	24,052.72	138,051.49	3,320,513,789.69
Mchanga, Mawe na Matofali	tani	15,616.82	5,628,598.59	87,900,825,792.70
Dioksidi Kaboni (CO2)	tani	1,446.53	7,557,612.79	10,932,322,581.22
Madini ya Shaba	kilo	557,490.53	2,013.04	1,122,250,884.23
Madini ya Chuma	kilo	48,454.41	16,555.53	802,188,387.36
Madini Mengineyo	tani	212,220.00	1,411,965.85	299,647,392,663.88
Jumla				4,783,370,198,736.77

Chanzo: Tume ya Madini Tanzania

(ii). Uuzaji wa Madini Nje

Thamani ya mauzo ya madini nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 13.3 hadi Dola za Kimarekani milioni 1,860.52 mwaka 2017 kutoka Dola za Kimarekani milioni 2,145.17 mwaka 2016 kama ilivyooneshwa katika jedwali hapa chini. Hii ilitokana na kuendelea kupungua kwa mauzo ya madini nje kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya 2010 kama iliviorekebishwa mnamo 2017, ambayo inakataza usafirishaji wa madini ghafi na inahimiza usafirishaji wa madini yaliyoongezwa thamani. Hatua hii ya serikali ililenga kulinda masilahi ya kitaifa kwa faida ya umma wa Watanzania wote.¹⁷

Jedwali Na. 9: Uuzaji wa Madini Nje

Aina ya Madini	Kipimo	Idadi katika Kipimo		Thamani ya Mauzo (Dola za Marekani '000')	
		2016	2017	2016	2017
Almasi (Ghafi)	Karati ('000')	239,305	304,456	85,090	67,510
Dhababu	Gramu ('000')	45,155	43,490	1,824,815	1,636,535
Vito vya mawe	Gramu ('000')	2,944,107	1,185,697	60,483	53,596
Chumvi	Tani	145,718	100,017	4,806	3,803
Phosphate	Tani	23,658	1,351	721	585
Mawe Chokaa	Tani ('000')	4,170	3,301	22,710	27,610
Bati	Tani	138	91	1,499	1,037

¹⁷ <https://mof.go.tz/docs/ECONOMIC%20SURVEY%20BOOK%202017%20FINAL.pdf>

Aina ya Madini	Kipimo	Idadi katika Kipimo		Thamani ya Mauzo (Dola za Marekani '000')	
		2016	2017	2016	2017
Jasi (Gypsum)	Tani	213,744	123,675	6,279	3,187
Makaa ya Mawe	Tani	276,030	563,053	11,580	22,250
Graphite	Tani	1,180	128	2,132	18
Fedha	Gramu ('000')	17,984	10,911	9,901	5,850
Shaba	Ratili ('000')	16,247	2,934	35,421	7,741
Madini ya Viwandani	Tani	4,769,577	708,047	78,491	29,896
Bauxite	Tani	74,660	12,090	1,242	898
Jumla				2,145,170	1,860,516

Chanzo: Wizara ya Madini¹⁸

Katika mwaka huu wa fedha, sehemu kubwa ya mauzo ya madini nje ya nchi ilichangiwa na miradi mikubwa ya madini ya Bulyanhulu, STAMIGOLD, Buzwagi, Geita, New Luika, na North Mara. Miradi hii ya madini pekee imechangia jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 1,357.37 (sawa na Shillingi za Kitanzania trillioni 3.14).¹⁹ Jedwali namba 10 linaonesha mchango wa kila mradi katika uuzwaji wa madini nje ya nchi.

Jedwali Na. 10: Miradi Mikubwa Iliyouza Madini Nje 2016/2017

Mradi	Thamani ya Madini (Dola za Kimarekani Milioni)
Geita Gold Mine	465.76
North Mara	381.02
Bulyanhulu	245.00
Buzwagi	174.35
New Luika	76.15
STAMIGOLD	15.09
Jumla	1,357.37

Chanzo: Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

3.5.2 Uzalishaji na Uuzaji wa Mafuta na Gesi Asilia Nje

Katika shughuli za utafutaji na uchimbaji mafuta, Tanzania haikurekodi uzalishaji wowote wa mafuta. Nchi bado inategemea kwa sana uagizaji wa mafuta kutoka nchi zingine. Hata hivyo, nchi imezalisha kiasi kikubwa cha gesi asilia mnamo 2016 na 2017. Kufikia sasa, kiasi cha gesi asilia inayozalishwa inachangiwa kwa sehemu kubwa na makampuni makubwa mawili, ambayo ni, M & P Exploration Production (T) Limited (eneo la Mnazi Bay na Pan African Energy Tanzania Limited (eneo la Songosongo). Kampuni zote mbili zilizalisha jumla ya futi za ujazo bilioni 35.54. Uzalishaji wa gesi asilia umechochewa na mahitaji makubwa ya bidhaa hii kwa ajili ya matumizi ya viwandani na majumbani.²⁰ Jedwali namba 11 linawasilisha uzalishaji wa jumla wa gesi asilia na thamani zake.

¹⁸ <https://mof.go.tz/docs/ECONOMIC%20SURVEY%20BOOK%202017%20FINAL.pdf>

¹⁹ <https://www.parliament.go.tz/uploads/budgetspeeches/1496328593-Hotuba%20ya%20Bajeti-%20Nishati%20na%20Madini.pdf>

²⁰ https://www.nbs.go.tz/nbs/takwimu/na/National_Accounts_Statistics_Popular_Version_2018.pdf

Jedwali Na. 11: Uzalishaji wa Gesi Asilia

Kampuni	Eneo (Kitatu)	Kiasi (Ujazo wa Scf) '000'		Thamani (Dola za Kimarekani)	
		2016	2017	2016	2017
M & P Exploration (T) Limited	Mnazi Bay	5,792,142	17,960,300	13,818,715	19,466,121
Pan African Energy Tanzania Limited	Songosongo	29,747,400	29,496,560	38,172,718	22,795,142
Jumla		35,539,542	47,456,860	51,991,433	42,261,263

Chanzo: Wizara ya Fedha²¹

Kwa mujibu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Tanzania haijaanza kusarisha gesi asilia nje ya nchi. Gesi asilia yote inayozalishwa inatumika kwa matumizi mbalimbali ya ndani ya nchi.

3.6 Mashirika Yanayomilikiwa na Serikali

Serikali inashiriki kwenye shughuli za madini, mafuta na gesi asilia kupitia mashirika yake mawili. Kwenye sekta ya madini, serikali inashiriki kupitia Shirika la Taifa la Madini, na kwenye sekta ya mafuta na gesi inashiriki kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Uanzishwaji na majukumu ya kisheria za mashirika haya yapo kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1969.

3.6.1 Shirika la Taifa la Madini

Shirika la Taifa la Madini lilianzishwa upya kwa agizo la serikali la kuanzisha mashirika ya umma la mwaka 2015 kwa lengo la kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye uchumi wa nchi na kutengeneza fursa za ajira kwa watanzania. Shirika linafanya shughuli zake chini ya usimamizi wa Wizara ya Madini na Bodi yake ya wakurugenzi. Bodi inaongozwa na Mwenyekiti ambaye ni mteule wa Mheshimiwa Rais ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ina wajumbe nane ambao huteuliwa na Waziri wa madini.

Shirika la Taifa la Madini inaendesha mgodi wa dhahabu wa Birahamulo kupitia kwa kampuni ya STAMIGOLD ambayo inaimiliki kwa asilimia 100. Kampuni ya STAMIGOLD pia inafanya majukumu ya kutafuta, kuendeleza, kuzalisha, kuchakata, na kutafuta masoko/kuuza dhahabu nchini na nje ya nchi. Vilevile, Shirika la Taifa la Madini pia linamiliki kampuni ya kuzalisha madini ya bati ya Kyerwa (Kyerwa Tin Company Limited) kwa asilimia 100. Kampuni ya Kyerwa inanunua madini aina ya "Cassiterite" kutoka kwa wachimbaji wadogo na vilevile inaendesha mradi wa makaa ya mawe uliopo kwenye safu ya milima ya Kabulo na ndani ya mgodi wa makaa ya mawe wa Kiwira, mkoani Songwe.

Vilevile, Shirika la Taifa la Madini linamiliki miradi ya madini kwa ushirikiano na makampuni mbalimbali. Miradi hii ya madini ni:

²¹ <https://mof.go.tz/docs/ECONOMIC%20SURVEY%20BOOK%202017%20FINAL.pdf>

- Mgodi wa Tanzanaiti uliopo kwenye kitalu C eneo la Mirerani Wilayani Simanjiro Mkoa wa Manyara. Shirika la Taifa la Madini inamili asilimia 50 ya hisa za mgodi huu na asilimia nyingine 50 zinamilikiwa na kampuni ya madini ya TanzaniteOne. Makubaliano ya kuendesha mgodi huu kwa ushirikiano yalianza tangu mwaka 2013.²²
- Mgodi wa dhahabu wa Buckreef unaopatika kusini mwa Ziwa Viktoria na takribani kilomita 110 kusini magharibi mwa mkoa wa Mwanza. Chini ya ushirikiano wa kuendesha mgodi huu, Shirika la Taifa la Madini linamiliki asilimia 45 ya hisa zote na kampuni ya TAZAM 2000, ambaye ndio inafanya shughuli za uendeshaji.²³
- Miradi na migodi mingine ya Shirika la Taifa la Madini iliyopo kwenye hatua mbalimbali za uendelezaji na ambayo inaweza kuendeshwa kwa ushirikiano na kampuni nyingine ni pamoja na mradi wa nishati ya makaa ya mawe ya Kiwira, mgodi wa dhahabu wa Buhemba, na mradi wa machimbo ya mawe ya Ubena Zomozi. Kwa mgodi wa dhahabu wa Buhemba, Shirika la Taifa la Madini lipo kwenye hatua za mwisho kumpata mwekezaji ambaye ataendesha naye mgodi huu kwa ubia.

Shirika la Taifa la Madini limepewa leseni 14 za kutafuta madini ya aina mbalimbali kama dhahabu, fosifeti, na madini adimu sehemu yoyote nchini. Vilevile, shirika limepewa leseni za msingi 44 za kuchimba madini ya aina mbalimbali. Mbali na leseni lilizonazo, Shirika limepeleka kwa Tume ya Madini maombi ya kupatiwa leseni mpya za awali za kuchimba madini 12, leseni ya madini 1, na leseni za kutafuta madini 2.

Kwa upande wa muundo wa umiliki wa Shirika na miradi yake, kwa mwaka wa fedha 2016/17 hakukuwa na badiliko lolote, wala kampuni tanzu zake au miradi yake ya madini. Kwa upande wa kifedha, Shirika lilipata hasara ya TZS 20,140,709,000 na hivyo, hakukuwa na faida kutoka kwenye shughuli za shirika katika mwaka huu wa fedha. Vilevile, Shirika halikuwekeza mtaji mpya au kulipa gawio au kuchangia kwenye mfuko wa serikali japokuwa lilipokea kiasi cha TZS 3,291,373,000 kutoka serikalini kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi na matumizi mengineyo. Shirika linatakiwa kulipa gawio na malipo mengine kwa serikali kwa mujibu wa kufungu cha 47 (f) cha sheria ya fedha ya mwaka 2015²⁴ na kifungu cha 23 (1) mpaka (6) cha sheria ya mashirika ya Umma ya mwaka 1992.

Kwa mwaka wa fedha wa 2016/17, Shirika halikutoa mikopo au kufadhili mkopo wa kampuni yoyote ya madini. Hata hivyo, hakuna utaratibu au sharti lolote la kisheria linalolitaka shirika kugharamia mahitaji ya kifedha ya makampuni ya madini. Kama sehemu ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo, Shirika liliwapatia msaada wa

²² More information regarding operations of this Tanzanite mine can be accessed at <http://www.tanzaniteone.com>

²³ Additional information about the Buckreef Gold project can be accessed at http://www.stamico.co.tz/wp-content/uploads/2017/10/Buckreef_Profile.pdf.

²⁴ <https://www.tro.go.tz/en/documents/>

kitaalamu wa kuandaa mipango ya biashara ya miradi yao ya madini ili iweze kufadhiliwa na taasisi za fedha.

Kwa upande wake pia, Shirika halikupata mkopo au ufadhilli wa mkopo toka serikalini katika mwaka wa fedha wa 2016/17. Vilevile, Shirika halikupokea fedha kutoka vyanzo vya nje kama taasisi za fedha ijapokuwa linaruhusiwa kwa mujibu wa kifungu 23 (1) cha Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992. Pia, Shirika halikugharamia miradi au shughuli zozote za kijamii au za umma nje ya bajeti yake katika mwaka wa fedha 2016/17. Taarifa zaidi kuhusu ushiriki wa Shirika kwenye shughuli za madini imetolewa kwa ufupi kwenye Jedwali namba 12.

Jedwali Na. 12: Ushiriki wa Shirika la Taifa la Madini Kwenye Shughuli za Madini

I. Kiwango na Masharti ya Ushiriki wa Nchi									
Kampuni/mradi unaoshiriki kwa niaba ya nchi	Kiwango cha umiliki au ushiriki (%)	Hali kisheria ya ya Kampuni	Masharti/Vigezo ya Umiliki	Mabadiliko ya Kiwango cha umiliki mwaka 16/17	Masharti ya muamala wa madiliko	Viunga vyenye taarifa za ziada			
Kampuni ya STAMIGOLD	100%	Kampuni tanzu	Kuchangia gharama za mtaji	Hakuna	Hakuna	Hakuna			
Kampuni ya Madini ya Bati Kyerwa	100%	Kampuni tanzu	Kuchangia gharama za mtaji	Hakuna	Hakuna	Hakuna			
Kampuni ya Madini ya Dhahabu Buckreef	45%	Kampuni Mshirika	Kuchangia gharama za mtaji	Hakuna	Hakuna	Hakuna			
Kampuni ya TanzaniteOne	50%	Kampuni Mshirika	Kuchangia gharama za mtaji	Hakuna	Hakuna	Hakuna			
II. Mahusiano ya kifedha kati ya Shirika la Taifa la Madini na Serikali									
Sheria au kanuni zinazoongoza mahusiano ya kifedha kati ya Shirika la Taifa la Madini na Serikali	Faida Halisi (TZS)	Kiwango za Uwezekazaji (TZS)	Gawio liliopewa Serikalini (TZS)	Michango mingine ya kifedha kwenda Serikalini	Fedha zilizopokewa toka serikalini (TZS)				
Uhusiano wa kifedha kati ya Mashirika ya Umma (pamoja na Shirika la Taifa la Madini) unaainishwa katika kifungu cha 23 cha Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992 na kifungu cha 47 (f) cha Sheria ya Fedha, 2015.	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	3,291,373,000				
III. Mikopo na Dhamana ya Mikopo inayotolewa na Shirika la Taifa la Madini kwa Kampuni za Madini.									
Sheria au kanuni zinazoongoza Mashirika ya umma kutoa mikopo au kudhamini mikopo ya kampuni za madini	Mikopo au dhamana iliyotolewa na Mashirika ya Serikali kwa kampuni za madini	Tarehe Mkopo au dhamana ilipotolewa	Tarehe ya kumaliza kulipa mkopo	Taasisi iliyotoa Mkopo au Dhamana	Taasisi iliyopewa mkopo au dhamana	Thamani ya mkono au Dhamana	Salio la mkopo kwa mwaka 16/17	Kiwango cha riba ya Mkopo	Muda Mkopo ratiba kulipa wa na ya
Hakuna sheria / mfumo wa kisheria unaoipa Shirika la Taifa la Madini mamlaka ya kutoa mikopo au dhamana kwa kampuni za uchimbaji madini.	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
IV. Mikopo na Dhamana ya Mikopo inayotolewa na Serikali kwa Kampuni za Madini, ikiwemo Shirika la Taifa la Madini									
Sheria au kanuni zinaipa Serikali mamlaka ya kutoa	Mikopo au dhamana iliyotolewa na Serikali	Tarehe Mkopo au dhamana ilipotolewa	Tarehe ya kumaliza kulipa mkopo	Taasisi iliyopokea Mkopo au Dhamana	Taasisi Serikali ya iliyotoa	Thamani ya mkono au Dhamana	Salio la mkopo kwa mwaka 16/17	Kiwango cha riba ya Mkopo	Muda Mkopo ratiba kulipa wa na ya

mikopo au dhamana kwa kampuni za Madini					mkopo au dhamana				
Utoaji wa mikopo au dhamana kutoka kwa serikali kwenda kwa mashirika ya umma unafanyika kwa mamlaka ya kifungu cha 23 (6) cha Sheria ya Shirika la Umma, 1992.	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
V. Fedha za mtaji kutoka vyanzo vya fedha za nje ya Serikali									
Sheria au kanuni zinazotoa mamlaka kwa mashirika ya Serikali kutafuta fedha kutoka vyanzo vya nje ya serikali	Thamani ya fedha za mtaji zilizotolea na taasisi za nje ya Serikali kwa mwaka 16/17	Thamani ya salio la Mkopo toka Kampuni za Madini	Thamani ya salio la mkopo toka taasisi za nje ya Serikali	Thamani ya salio la mikopo yote	Viunga vyenye taarifa za ziada				
Shirika la Taifa la Madini inaweza kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine nje ya serikali kwa idhini ya msajili wa Hazina (Wizara ya Fedha na Mipango). Vilevile, utaratibu huo ni kwa mujibu wa kifungu cha 23 cha Sheria ya Mashirika ya Umma, 1992.	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna
VI. Matumizi kwenye Shughuli za kijamii au umma nje ya bajeti ya Shirika kwa niaba ya Serikali									
Muda/Kipindi	Aina ya Matumizi	Wanufaika	Kiwango	Sheria au Kanuni zinazoruhusu matumizi	Maelezo Sheria/kanuni hizo ya	Maelezo ya ziada			
2016/17	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna

3.6.2 Shirika la Taifa la Maendeleo

Shirika la Taifa la Maendeleo linamilikiwa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Shirika linafanya shughuli zake katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya madini. Katika sekta hii, Shirika linaendesha miradi minne ya madini kwa ushirikiano na kampuni nyingine. Miradi hii ni pamoja na mradi wa madini ya chuma Liganga, mradi wa madini ya chuma Sponge, mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma, na mradi wa makaa ya mawe Ngaka. Taarifa za kina za miradi hii zinazelezewa kwenye Jedwali namba 13.

Jedwali Na. 13: Miradi ya Shirika la Taifa la Maendeleo kwenye Sekta ya Madini

Na	Madini	Jina la Mradi	Maelezo ya mradi
1	Madini ya chuma	Mradi wa madini ya chuma Liganga	Mradi huu unapatikana Wilaya ya Ludewa, takribani kilomita 850 kutoka Dar es Salaam. Mgodi unaendeshwa na kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources Ltd ndani ya Mgodi wa Mchuchuma. Tanzania China International Mineral Resources Ltd ndani ya Mgodi wa Mchuchuma ni kampuni ilioanzishwa kwa ushirikiano kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo na kapuni ya Sichuan Hongda Group ya China. Mradi unagharimu dola za kimarekani takribani bilioni 1.8 na utajenga mgodi unaozalisha tani 2.9 za chuma kwa mwaka. Vilevile, mradi utajenga mgodi wa chuma na chuma cha pua utakaozalisha tani 1.0 za bidhaa za chuma cha pua, vanadiamu, pentosaidi, na titaniamu dioksidi.
		Mradi wa madini ya chuma Sponge	Mradi huu utajenga mtambo wa kuzalisha chuma wa Sponge wenyewe uwezo wa 440,000 tpa ambaa utazalisha tani 300,000 za bidhaa za chuma na chuma cha pua kwa mwaka. Mradi unajengwa Wilaya ya Ludewa na utatumia madini ya chuma kutoka Maganga Matitu and makaa ya mawe kutoka Katedwaka. Mradi unaendeshwa na kampuni ya Maganga Matitu Resource Development Limited ambayo wamiliki wake ni Shirika la Taifa la Maendeleo na MM Steel Resources Public Limited Company.
2	Makaa Mawe ya	Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma	Mradi upo Wilaya ya Ludewa na unataraji kujenga mgodi wa makaa ya mawe unaozalisha tani 3.0 kwa mwaka, kituo cha nishati ya maji chenye uwezo wa mega wati 600, na kujenga njia ya kusafirisha nishati umeme ya 220 kVA kutoka Mchuchuma-Liganga. Mradi unaendeshwa na kampuni ya Tanzania China International Mineral Resources Ltd ilioanzishwa kwa ushirikiano kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo na kampuni ya Sichuan Hongda Group ya China.
		Mradi wa makaa ya mawe Ngaka	Mradi huu unaendeshwa na kampuni ya Tancoal Energy Ltd ambayo ilianzishwa kwa ushirikiano kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo na kampuni ya Intra Energy Corporation Ltd ya Australia. Mradi huu unapatika bonde la Ruhuhu, Wilaya ya Mbinga, takribani kilomita 1,100 kutoka Dar es Salaam. Vitalu vya makaa ya mawe vya Ngaka vinakadiriwa kuwa na tani milioni 423 za makaa yam awe. Uzalishaji uliana mwezi Agosti 2011 na makaa ya mawe yanazalishwa huuzwa kwenye soko la ndani na nje, hususani Malawi, Kenya, Zambia na Uganda.

Shirika la Taifa la Maendeleo halishiriki katika shughuli za uendeshaji wa kila siku wa kampuni hizi, bali linasimama kama mmiliki. Usimamizi wa shughuli zote za kila siku za mradi husika unafanywa na kampuni inazoshirikiana nazo. Maelezo ya ushiriki wa Shirika

la Taifa la Maendeleo katika miradi hii minne yanatolewa kwa ufupi katika Jedwali namba 14.

Jedwali Na. 14: Ushiriki wa Shirika la Taifa la Maendeleo kwenye Miradi ya Madini

Jina la Mradi	Kiwango cha Umiliki (%)	Hali kisheria ya Kampuni inayoendesha mradi	Masharti ya Umiliki	Mabadiliko ya umiliki kwa mwaka 16/17	Mashari ya muamala wa mabadiliko	Viunga vyenye taarifa za ziada
Mradi wa madini ya chuma Liganga	20%	Ushirikiano	Mtaji usiohusisha kulipa fedha	Hakuna	Hakuna	Taarifa za kina za mradi ²⁵
Mradi wa madini ya chuma Sponge	50%	Ushirikiano	Mtaji unaohusisha kulipa fedha	Hakuna	Hakuna	Taarifa za kina za mradi ²⁶
Mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma	20%	Ushirikiano	Mtaji usiohusisha kulipa fedha	Hakuna	Hakuna	Taarifa za kina za mradi ²⁷
Mradi wa makaa ya mawe Ngaka	30%	Ushirikiano	Mtaji usiohusisha kulipa fedha	Hakuna	Hakuna	Taarifa za kina za mradi ²⁸

3.6.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ni shirika la mafuta ya laifa ambalo linashiriki kwenye mnyororo wa thamani wa mafuta kupitia kampuni zake tanzu mbili zinazojulikana kama Kampuni ya Gesi Tanzania na kampuni ya uwekezaji ya TANOIL. Kampuni hizi zilianzishwa kama kampuni za kibiasara zinazomilikiwa moja kwa moja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania.

Kupitia kampuni hizi, Shirika linashiriki katika miradi ya usambazaji na uuzaaji wa bidhaa za mafuta na gesi. Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2016/17 ilionesha kuwa miradi mikubwa miwili ya usambazaji wa gesi ilitekelezwa. Miradi hii ni mradi wa bomba la kusafirisha gesi asilia na mradi wa mifumo ya kusambaza gesi asilia. Mradi wa usambazaji gesi unayo miradi midogo midogo tisa inayohusika kusambaza gesi kutoka kwenye bomba kuu kwenda maeneo mbalimbali.

Vilevile, Shirika lilitekeleza miradi mitano ya utafutaji gesi asilia kwenye vitalu vya Songosongo. Miradi hii ni pamoja na mradi wa songosongo magharibi, mradi kwenye kitalu 4/1B na 4/1C, mradi wa Nomenklecha ya Stratigrafiki, mradi wa Eyasi Wembere, na mradi wa kujenga miundombinu ya kusafirisha gesi asilia. Jedwali namba 15 linawasilisha taarifa za kina za miradi hii ya Shirika katika mwaka wa 2016/17.

²⁵ <http://ndc.go.tz/iron-and-steel-metallurgical-complex/>.

²⁶ <https://motisungroup.com/mining.php>

²⁷ <http://ndc.go.tz/power-production/>

²⁸ <http://ndc.go.tz/power-production/>

Jedwali Na. 15: Maelezo ya Miradi ya Gesi Asilia ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Na	Jina la Mradi	Shughuli za Mradi	Hatua Mradi Ulipofikia
1	Mradi wa Gesi Asilia Songosongo	Mradi huu unafanya shughuli za utafutaji na uchimbaji wa gesi asilia katika Vitalu vya Songosongo. Katika mradi huu Shirika inamiliki asilimia 29 ya hisa zote za mradi.	Hatua ya utekelezaji
2	Mradi wa Gesi asilia Mnazi Bay	Mradi wa Mnazi Bay unafanya kwenye kitalu cha gesi chenye ukubwa kwa kilomita za mraba 756 kinachopatikana kati ya Mkoa wa Ruvuma na pwani ya Kitalu namba 1 cha gesi. Mradi huu unaendeshwa na kampuni ya Maurel & Prom, ambapo Shirika linamiliki asilimia 20 ya hisa.	Hatua ya utekelezaji
3	Mradi wa Utafutaji gesi kwenye vitalu 4/1B na 4/1C	Mradi huu unahusisha utafutaji gesi asilia katika vitalu 4/1B na 4/1C ambavyo vilitengwa kwa maslahi ya umma. Shughuli za mradi zilizokamilika mpaka mwaka 2016/17 ni pamoja na uchambuzi wa kijiomikali na kibaostratigrafia na ufanuzi wa sampuli kutoka Kitalu namba 1.	Hatua ya maandalizi
4	Mradi Nomenklecha Stratigrafiki	Katika mradi huu shughuli ambazo zimekwisha fanywa ni pamoja na kukusanya na kufafanua taarifa zilizopo, uwiano wa visima, na kazi za kijiolojia katika mabonde ya Tanga na Ruvu.	Hatua ya maandalizi
5	Mradi wa Eyasi Wembere	Katika mradi huu, shughuli za kijiolojia zimekwisha tekelezwa pamoja na ukaguzi bayana wa eneo la mradi.	Hatua ya maandalizi
6	Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha gesi nje ya nchi (Liquefied Natural Gas)	Shirika linashirikiana na Kampuni tano za Kimataifa za Mafuta (Shell Tanzania Ltd, Ophir, Pavilion, Statoil, na ExxonMobil) kutathmini uwezekano wa kujenga na kuendesha mradi wa miundombinu ya kusafirisha gesi asilia nje ya nchi. Mradi huo bado uko kwenye mazungumzo ndani ya Serikali ya Tanzania.	Hatua ya maandalizi

Chanzo: Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, 2016/17

Sheria ya mafuta ya Petroli ya mwaka 2015, imeipa serikali mamlaka ya kumiliki angalau 25% katika kila kitalu cha mafuta na gesi nchini kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Hivyo, serikali inashiriki kwenye uendelezaji wa rasilimali ya mafuta na gesi nchini kupitia Shirika. Kimajukumu, Shirika linashiriki katika utafutaji na uendelezaji wa miradi ya gesi kwa namna kuu mbili: Kwanza, linafanya shughuli za utafutaji na uendelezaji wa vitalu vya gesi yenewe. Hadi kufikia mwezi Mei 2020, Shirika limeshafanya shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi katika vitalu vinne vya kimkakati. Pili, linafanya miradi ya gesi kwa kushirikiana na kampuni za kimataifa za mafuta kupitia mikataba wa kushiriki uzalishaji. Kulingana na mikataba ya kushiriki uzalishaji, Shirika halitashiriki wala kuchangia gharama za utafutaji mafuta au gesi, lakini baada ya mafuta au gesi kupatikana linaruhusiwa kushiriki katika uzalishaji kama itakavyokuwa imeanishwa katika mkataba. Ushiriki wa Shirika katika uzalishaji wa gesi au mafuta ni sharti la kisheria ambalo linazitaka kampuni za mafuta na gesi kushirikiana nalo na kuingia

Mikataba ya kushiriki uzalishaji ya wabia watatu. Hadi kufikia mwaka 2016/17, kulikuwa na mikataba ya kushiriki uzalishaji mafuta na gesi asilia 13.²⁹

Muundo wa umiliki wa Shirika, kampuni zake tanzu pamoja na miradi yake haikubadilika katika mwaka wa fedha 2016/17. Vilevile, katika mwaka huu wa fedha shirika liliripoti hasara ya TZS 648,393,000,000; hivyo, hakukuwa na mapato za ziada kutoka kwenye shughuli za uendeshaji wa shirika. Sehemu ya 6 ya sheria ya usimamizi wa mapato ya mafuta na gesi ya mwaka 2015 inainisha vyanzo vya mapato vya Shirika ambavyo ni bonasi, ada ya vitalu, ada ya mafunzo, na mgawo wa faida unaotokana na uwekezaji na ushiriki wa moja kwa moja wa Shirika katika shughuli za utafutaji wa mafuta au gesi asilia. Vivyo hivyo, katika mwaka huu wa fedha Shirika halikuwekeza au kuilipa gawio au kutoa mchango wowote kwa serikali licha ya kupokea jumla ya TZS 3,629,578,900 kugharamia mishahara ya wafanyakazi na matumizi mengine. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linapaswa kuilipa serikali gawio kwa mujibu wa kifungu cha 47 (f) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 na kifungu cha 23 (1) hadi (6) cha Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992.

Katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika halijatoa mkopo au kuiwekea dhamana ya mkopo kampuni yoyote ya mafuta na gesi. Hatahivyo, hakuna sharti la kisheria linalolitaka Shirika kutoa mkopo au kuiwekea dhaman kampuni ya mafuta na gesi. Kwa upande mwingine, katika kipindi hiki Shirika halikupokea mkopo au kupewa dhamana ya mkopo kutoka serikalini. Taarifa zaidi kuhusu ushiriki wa serikali katika shughuli za mafuta na gesi kuititia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania imetolewa kwa ufupi kwenye Jedwali namba 16.

²⁹ <http://www.teiti.go.tz/storage/app/uploads/public/5e0/b07/e9a/5e0b07e9af5bd943977987.pdf>

Jedwali Na. 16: Ushiriki wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania Kwenye Shughuli za Mafuta na Gesi Asilia

I. Kiwango na Masharti ya Ushiriki wa Nchi

Kampuni/mradi unaoshiriki kwa niaba ya nchi	Kiwango cha umiliki au ushiriki (%)	Hali kisheria ya Kampuni	Masharti/Vigezo ya Umiliki	Mabadiliko ya Kiwango cha umiliki mwaka 16/17	Masharti ya muamala wa madiliko	Viunga vyenye taarifa za ziada
GASCO	100%	Kampuni Tanzu	Mtaji umelipwa kikamilifu	Hakuna	Hakuna	
COPEC/TANOIL	100%	Kampuni Tanzu	Mtaji umelipwa kikamilifu	Hakuna	Hakuna	
Mradi wa gesi asilia Songsosongo	29%	Mmiliki wa hisa	Mtaji umelipwa kikamilifu	Hakuna	Hakuna	
Mradi wa gesi asilia Mnazi bay	20%	Mshirika	Una riba	Hakuna	Hakuna	

II. Mahusiano ya kifedha kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Serikali

Sheria au kanuni zinazoongoza mahusiano ya kifedha kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Serikali	Faida Halisi (TZS)	Kiwango za Uwezekazaji (TZS)	Gawio liliopwa Serikalini (TZS)	Michango mingine ya kifedha kwenda Serikalini	Fedha zilizopokewa toka serikalini (TZS)
Uhusiano wa kifedha kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Serikali kuhusu mapato yaliyosalia hutolewa katika kifungu cha 6 cha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi, 2015, na kifungu cha 114 na 115 cha Sheria ya Petroli, 2015. Vile vile, sharti la malipo ya gawio kwa Serikali limetolewa katika kifungu cha 47 (f) cha Sheria ya Fedha, 2015. Pia, kifungu cha 23 (1) hadi (6) cha Sheria ya Mashirika ya Umma, 1992 kinatoa uhusiano wa kifedha kati ya mashirika ya Umma (ikiwemo Shirika) na Serikali.	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	3,629,578,900

III. Mikopo na Dhamana ya Mikopo inayotolewa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa Kampuni mafuta na gesi

Sheria au kanuni zinazoongoza Mashirika ya umma kutoa mikopo au kudhamini mikopo ya kampuni za mafuta na gesi	Mikopo au dhamana iliyotolewa na Mashirika ya Serikali kwa kampuni za mafuta na gesi	Tarehe Mkopo au dhamana ilipotolewa	Tarehe ya kumaliza kulipa mkopo	Taasisi iliyotoa Mkopo au Dhamana	Taasisi iliyopewa mkopo au dhamana	Thamani ya mkonon au Dhamana	Salio mkopo kwa mwaka 16/17	Kiwango cha riba ya Mkopo	Muda Mkopo ratiba kulipa wa na ya
Hakuna sheria au mfumo wa kisheria unaopia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania mamlaka ya kutoa mikopo au dhamana ya mikopo kwa	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna

kampuni za uchimbaji au utafutaji gesi na mafuta.										
IV. Mikopo na Dhamana ya Mikopo inayotolewa na Serikali kwa Kampuni za Madini, ikiwemo Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania										
Sheria au kanuni zinaipa Serikali mamlaka ya kutoa mikopo au dhamana kwa kampuni za mafuta na gesi	Mikopo au dhamana iliyotolewa na Serikali	Tarehe Mkopo au dhamana ilipotolewa	Tarehe ya kumaliza kulipa mkopo	Taasisi iliyopokea Mkopo au Dhamana	Taasisi Serikali iliyotoa mkopo dhamana	Thamani ya mkonon au Dhamana	Salio la mkopo kwa mwaka 16/17	Kiwango cha riba ya Mkopo	Muda Mkopo ratiba kulipa	wa na ya
Utaratibu utoaji mikopo au dhamana ya mikopo kutoka kwa serikali kwenda kwa Mashirika yanayomilikwa na Serikali umeanishwa kwenye kifungu cha 23 (6) cha Sheria ya mashirika ya Umma ya mwaka 1992. ³⁰	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	
V. Fedha za mtaji kutoka vyanzo vya fedha za nje ya Serikali										
Sheria au kanuni zinazota mamlaka kwa mashirika ya Serikali kutafuta fedha kutoka vyanzo vya nje ya serikali	Thamani ya fedha za mtaji zilizotolea na taasisi za nje ya Serikali kwa mwaka 16/17	Thamani ya salio la Mkopo toka Kampuni za Mafuta na gesi	Thamani ya salio la mkopo toka taasisi za nje ya Serikali	Thamani ya salio la mikopo yote	Viunga vyenye taarifa za ziada					
Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania inaweza kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine nje ya serikali kwa idhini ya msajili wa Hazina (Wizara ya Fedha na Mipango). Vilevile, utaratibu huo ni kwa mujibu wa kifungu cha 23 cha Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1992.	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna					
VI. Matumizi kwenye Shughuli za kijamii au umma nje ya bajeti ya Shirika kwa niaba ya Serikali										
Muda/Kipindi	Aina ya Matumizi	Wanufaika	Kiwango	Sheria au Kanuni zinazoruhusu matumizi	Maelezo Sheria/kanuni hizo	ya	Maelezo ya ziada			
2016/17	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna	Hakuna					

³⁰ <https://www.parliament.go.tz/polis/uploads/bills/acts/1566551814-The%20Public%20Corporations%20Act,%201992.pdf>

3.7 Ukusanyaji na Usambazaji wa Mapato yatokanayo Shughuli za Madini, Mafuta na Gesi Asilia

3.7.1 Mchakato wa Bajeti

Tanzania inatumia bajeti ya Mfumo wa Mapato na Matumizi ya Muda wa Kati. Utayarishaji na utekelezaji wa bajeti unaongozwa na Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Sehemu ya IV ya Sheria ya Bajeti inatoa hatua za mchakato wa bajeti ambazo zinaweza kugawanywa katika hatua kuu nne zinazojumuisha utengenezaji wa bajeti, mjadala na idhini, utekelezaji wa bajeti na usimamizi na udhibiti.

i. Uundaji wa Bajeti (Oktoba - Machi)

Uundaji wa bajeti ni hatua ya kwanza katika mchakato wa bajeti. Kawaida hufanywa kutoka Oktoba hadi Machi ikijumuisha michakato michache ifuatayo:

- Uundaji wa sera ya bajeti na makadirio ya rasilimali
- Utoaji wa miongozo ya mipango na bajeti
- Kukadiria mapato na matumizi ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mikoa, Mashirika ya Umma, na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Uchunguzi wa makadirio ya kamati ndogo za bunge na kamati ya kiufundi ya mawaziri
- Idhini ya baraza la mawaziri la makadirio ya bajeti.

ii. Mjadala na Kibali cha Bunge (Aprili-Juni)

Hatua ya pili katika mchakato wa bajeti ni kujadili na kupitisha makadirio ya bajeti. Hii hufanyika kutoka Aprili hadi Juni ikijumuisha shughuli muhimu zifuatazo:

- Kuwasilisha katika bunge
- Hotuba za sajeti zilizowasilishwa (siku ya bajeti)
- Mjadala katika bunge kamili
- Bajeti kupigiwa kura kuwa sheria

iii. Utekelezaji wa Bajeti (Julai - Juni)

Utekelezaji wa bajeti unafuata kama hatua ya tatu katika mchakato wa bajeti. Huanza kutoka Julai 1 hadi 30 Juni (ndani ya mwaka mmoja wa fedha). Inajumuisha shughuli zifuatazo:

- Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mikoa, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa huandaa mipango ya utekelezaji (mipango ya kazi)
- Bajeti inatekelezwa na mfumo wa bajeti wa fedha taslimu.
- Hazina inatoa fedha kwa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mikoa, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Huduma zinazotolewa
- Miradi ya maendeleo inafanywa
- Shughuli zinazohusiana na uhasibu, ununuzi na taratibu za kuripoti

- Kuandaa taarifa za kifedha za ufungaji wa hesabu

iv. Ukaguzi, Usimamizi na Udhibiti

Hatua ya nne na ya mwisho katika mchakato wa bajeti ni ukaguzi, usimamizi na udhibiti. Ni hatua inayoendelea ndani ya mwaka na inajumuisha shughuli kuu zifuatazo:

- Ufutiliaji wa ndani ya mwaka pamoja na ukaguzi wa ndani
- Ukaguzi wa nje unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- Ripoti ya ukaguzi inayojadiliwa katika kamati za uangalizi za bunge yaani Kamati ya Hesabu za Umma, Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya Uwekezaji wa Umma na baadaye kuwasilishwa katika bunge na hatua za ufutiliaji zinazochukuliwa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa hupokea mapato ya moja kwa moja kutoka kwa kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zinazofanya kazi ndani ya mamlaka yao kwa njia ya ushuru wa huduma na wajibu wa shirika kwa jamii. Uhamishaji kutoka serikali kuu kawaida huwa katika mfumo wa fedha za maendeleo, ambazo hutolewa kuititia hazina kutoka kwa mfuko uliojumuishwa (ambayo ni pamoja na mapato yaliyopatikana kutoka kwa sekta ya madini, mafuta na gesi asilia katika ngazi ya kitaifa), kwa kuzingatia formula ya kawaida ya ugawaji katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ushuru wa huduma ni mionganini mwa mapato makuu ya vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Sehemu ya 6 hadi 9 ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Kwa hiyo mapato hayo yanapangiwa, yanawekewa bajeti, na kutumiwa kulingana na kanuni na miongozo ya kifedha ya kitaifa na ya Serikali za Mitaa, ambayo ni pamoja na Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2010, na Sheria ya Fedha ambayo hutolewa kila mwaka baada ya kuitishwa kwa makadirio ya bajeti na bunge. Nyingine ni Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 na kanuni zake, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2016 na kanuni zake. Pia, miongozo juu ya matumizi ya mapato ya vyanzo vya ndani vya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (yaani asilimia 60 ya mapato ya vyanzo vya miradi ya maendeleo) na mchango wa asilimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu.³¹

Mapato na matumizi ya Halmashauri yanakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kila mwaka. Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa inasimamia matumizi sahihi ya fedha za maendeleo kutoka kwa vyanzo vya ndani kwa kuzingatia sana dhamana ya masuala ya thamani halisi ya fedha kwa huduma na bidhaa

³¹<https://www.mof.go.tz/mofdocs/budget/Guideline/GUIDELINES%20FOR%20THE%20PREPARATION%20OF%20PLANS%20AND%20BUDGET%20FOR%20201718.pdf>

zilizonunuliwa (Uchumi na ufanisi katika matumizi ya fedha). Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa pia inasimamia matumizi ya mfuko wa wajibu wa mashirika kwa jamii, ambao kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zilitumia moja kwa moja kwa jamii zinazozunguka katika maeneo yao (walivyokubaliana kwa pamoja na jamii husika).

3.7.2 Ukusanyaji wa Mapato

Mwaka wa fedha wa serikali unaanza tarehe 1 Julai na unamalizika tarehe 30 Juni mwaka unaofuata. Kampuni za madini, mafuta na gesi asilia hufanya malipo katika mashirika mbalimbali ya serikali katika mwaka wa fedha. Mashirika haya yamegawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni, wapokeaji wa ushuru, ada, na tozo, ambalo linajumuisha Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wizara ya Fedha na Mipango, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Wizara ya Madini, Msajili wa Hazina na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Kundi la pili linajumuisha wapokeaji wa michango ya hifadhi za jamii, ambao ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Utumishi wa Umma na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

Mamlaka ya Mapato Tanzania ndio linapokea mapato mengi ambayo serikali hukusanya kutoka kwa sekta ya madini, mafuta na gesi. Pia inakusanya ushuru mbalimbali ikiwa ni pamoja na kodi ya mapato ya kampuni, kodi ya kuendeleza Ufund Stadi, kodi ya ongezeko la thamani, ushuru wa kuagiza na ushuru kwa bidhaa ziendazo nje ya nchi. Msajili wa Hazina hupokea gawio kwa hisa za serikali na mapato kutokana na uuzaaji wa hisa ambazo serikali inashikilia katika kampuni za madini, mafuta na gesi asilia. Zaidi ya hayo, Msajili wa Hazina anapokea mrabaha, faida kutoka kwa mapato ya ziada ya gesi, faida kutokana na mikataba ya ushirikiano wa uzalishaji, bonasi ya saini na bonasi ya uzalishaji kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania.


Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania linakusanya mapato yasiyo ya kodi kama vile mrabaha, Mapato ya Gesi iliyohifadhiwa, mapato ya gesi ya ziada, na faida ya serikali kulingana na mikataba ya ushirikiano wa uzalishaji, ada ya zuio ya kila mwaka, bonasi za saini na ada ya mafunzo kutoka kwa kampuni za mafuta na gesi. Sehemu ya 6 ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015 inaipa nguvu Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kubakiza bonasi, ada ya kitalu na ada ya mafunzo kwa madhumuni ya kukuza maendeleo ya sekta ya mafuta na gesi asilia. Mkondo mwingine wa mapato ambao Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania wanaruhusiwa kubakiza ni faida inayotokana na uwekezaji na ushiriki wa moja kwa moja wa Shirika katika shughuli za madini, mafuta na gesi asilia .

Pia, kulingana na kifungu cha 9 cha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya mwaka 2015 na Kanuni zake, na kifungu cha 113 cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, mirabaha na sehemu ya faida ya serikali inayolipwa na kampuni za mafuta na gesi na wamiliki

wa leseni hukusanya na TPDC na kupelekwa kwenye Mfuko³² wa Mafuta na Gesi ambao akaunti yake ipo Benki Kuu ya Tanzania (BOT) chini ya usimamizi wa Hazina. Kwa kuongezea, Shirika inakusanya ushuru wa usafirishaji wa gesi kupitia bomba la gesi la Mtwara-Dar es Salaam na Songas. Katika kipindi cha mwaka 2016/17, Shirika lilikusanya TZS 22,820,860,869,562.91 kutoka kwa Pan African Energy (Tanzania) Limited.

Kwa upande mwingine, Wizara ya Madini inapokea mrabaha, ada ya Leseni, ada ya maombi, na ada ya kila mwaka ya kukodisha kutoka kwa kampuni za madini, pamoja na makampuni yanayomilikiwa na serikali. Wizara ya Maliasili na Utalii inakusanya ada ya usimamizi wa misitu kupitia Wakala wa Misitu Tanzania. Mamlaka za Serikali za Mitaa hukusanya ushuru wa huduma na mifuko ya hifadhi ya jamii hukusanya michango ya usalama wa jamii. Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inazipa mamlaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoza kampuni za madini, mafuta na gesi asilia zinazofanya kazi katika mamlaka yao ushuru wa huduma hadi asilimia 0.3 ya mapato ya kila mwaka. Mfumo wa makusanyo ya mapato ya madini, mafuta na gesi asilia umefupishwa kwa kielelezo kwenye Kielelezo namba 1.

³² See for the example, the report of the Controller and Auditor General on the consolidated and Separate Financial statements of TPDC for the year ended 30 June 2017. <https://tpdc.co.tz/downloads.php>



Kielelezo Na. 1: Mtiririko wa Malipo ya Ukusanyaji wa Mapato ya Madini, mafuta na gesi asilia

3.7.3 Mgawanyiko wa Mapato

Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inatoa taratibu za kisheria za bajeti zinazohusiana na mapato, udhibiti wa matumizi na uwajibikaji. Sehemu ya 11 ya sheria hii inaanlisha mfuko mkuu wa jumla. Sheria inataka mapato yote au fedha nyingine zilizokusanywa au kupokelewa kuwekwa kwenye mfuko isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo na Bunge. Kwa hiyo, mapato yanayopatikana kutoka kwa sekta ya madini, mafuta na gesi asilia huwekwa kwenye Mfuko. Sheria ya Matumizi ya mwaka fedha husika, kwa upande mwingine, inampa Waziri wa Fedha mamlaka ya kutoa fedha kutoka kwenye mfuko mkuu wa hazina kuzipanga katika kasma mbalimbali. Malipo yaliyofanywa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kwenye mfuko huu hujumuishwa na malipo kutoka sekta nyingine. Hivyo ni vigumu kufahamu matumizi ya serikali yanatokana na chanzo kipi cha fedha.

3.8 Leseni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia

3.8.1 Utoaji wa Leseni

Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Madini ya mwaka 2018, inaelezea taratibu za utoaji na uhamishaji wa aina mbalimbali za leseni za madini. Jedwali namba 17 linaonesha aina za leseni za madini zitolewazo.

Jedwali Na. 17: Aina za Leseni za Madini

Aina ya Leseni	Maelezo ya Utoaji wa Leseni
Leseni ya Utafutaji	Leseni za utafutaji madini hutolewa kwa watu au taasisi, ambazo zinataka kufanya shughuli za utafutaji. Leseni hii hutolewa mwanzoni kwa kipindi kisichozidi miaka minne. Baada ya kipindi cha miaka minne kuisha, mmiliki anaweza kuomba kusasisha leseni hii. Mmiliki atapewa umiliki wa leseni kwa mara nyingine kwa kipindi cha miaka mitatu. Leseni ya utafutaji haitatolewa tena kwa mmiliki baada ya kipindi cha pili kuisha.
Leseni Maalum ya Madini	Leseni Maalum ya Madini hutolewa kwa shughuli kubwa tu za madini zenye uwekezaji usiopungua kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 100. Leseni hii inaruhusu uchimbaji wa madini katika upeo wa ukubwa wa eneo la kilomita 35 za mraba, kwa hifadhi za madini ya juu juu, ukubwa wa mwisho wa eneo ni kilomita za mraba 70. Leseni hii hutolewa kwa kipindi kisichozidi miaka kumi kutegemeana na makadirio ya muda ambao hifadhi ya madini itachimbwa au kipindi ambacho mwombaji anaweza kuomba. Muda wa leseni utategemea kipindi kipi kifupi kati ya hivi. Leseni Maalum ya Madini inaweza kutolewa kwa kipindi kingine ikiwa ombi la kusasisha limepokelewa mwaka mmoja kabla ya kumalizika muda kwa leseni ya awali.
Leseni ya Madini	Leseni ya Madini hutolewa kwa operesheni ya uchimbaji wa kati, ambao uwekezaji wake ni kati ya Dola za Kimarekani 100,000 na 100,000,000 au sawa na hiyo katika Shilingi ya Kitanzania. Muda wa wa umiliki wa leseni hii hauzidi miaka 10. Leseni ya Madini inaweza kutolewa kwa kipindi kingine ikiwa ombi la kusasisha limepokelewa miezi sita kabla ya kumalizika kwa muda wa leseni ya awali. Eneo la linaloruhusiwa kuombwa si zaidi ya kilomita za mraba 10.
Leseni ya Awali ya Uchimbaji Madini	Leseni ya awali ya uchimbaji madini hutolewa tu kwa raia au taasisi za Kitanzania. Leseni hii hutolewa kwa kipindi cha miaka saba na inaweza kuombwa upya kwa muda huo huo baada ya muda wa awali kumalizika. Wamiliki wa leseni hii wanaruhusiwa kufanya shughuli za utafutaji na uchimbaji madini kwa eneo lenye ukubwa usiozidi hekta 10 kwa madini yote ukiondoa vito vya mawe na hekta tano kwa madini ya ujenzi. Wamiliki wa leseni wanaweza kutuma maombi ya kusasisha leseni zao miezi mitatu kabla ya muda wa leseni kumalizika.
Leseni ya Uchakataji Madini	Kwa kushauriana na Waziri na Tume ya Madini, wenyewe leseni za madini wanahitajika kutenga asilimia fulani ya madini kwa ajili ya kuchakata, kuyeyusha au kusafisha ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Leseni ya uchakataji madini hutolewa kwa kipindi kisichozidi miaka 10 na wamiliki wanaweza kutuma maombi kusasisha leseni zao.
Leseni za Kuyeyusha na Kusafisha Madini	Leseni ya kuyeyusha na Kusafisha inaweza kutolewa kwa watu binafsi au taasisi kwa kipindi kisichozidi miaka 25. Wamiliki wa leseni hizi wanaweza kuomba kusasisha leseni baada ya muda wa awali kumalizika.

Chanzo: Sheria ya Madini, 2015

Mbali na haki za uchimbaji madini, Sehemu ya tano (V) ya Sheria ya Madini, 2015 inatoa maelezo ya utoaji wa leseni zingine zinazoweza kutolewa kwa watu binafsi au taasisi ambazo zingetaka kushughulika na madini ikiwa sio moja kwa moja katika shughuli za uchimbaji. Jedwali namba 18 linaonesha aina ya leseni mbalimbali zitolewazo.

Jedwali Na. 18: Leseni za Kushughulika na Madini

Aina ya Leseni	Maelezo ya Utoaji wa Leseni
Leseni ya Uuzaji Madini	Leseni ya uuzaaji ya madini inaruhusu mmiliki kuuza na kuuza madini ndani au ne ya nchi kutoka kwa madalali wa madini walioidhinishwa. Leseni hii kama inahusisha vito vya thamani, inamtaka mwombaji awe ameweza kununua na kuanza kutumia mashine tano za kusanifu madini ikiwa ni Mtanzania na mashine thelathini (30) ikiwa ni mgeni katika kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ambayo leseni ilitolewa. Leseni ya muuzaji wa madini inahusisha aina mbalimbali za madini yafuatayo; dhahabu, madini yenye asilia ya chuma, vito vya rangi, almasi, makaa ya mawe, madini ya viwandani na madini ya ujenzi. Leseni hii inakuwa hai na halali kwa kipindi cha miezi kumi na 12 na itamalizika muda wake kila tarehe 30 Juni ya kila mwaka. Leseni ya uuzaaji madini inaweza kutolewa mara nyingine kama mwombaji atatuma ombi la kusasisha leseni mwezi mmoja kabla ya muda wake wa awali kumalizika.
Leseni ya Udalali wa Madini	Leseni ya Udalali wa Madini hutolewa kwa mtu au kampuni ambayo inataku kununua, kupata madini kutoka kwa mchimbaji aliyeidhinishwa na kuuza kwa muuzaji mwenye leseni. Leseni hii hutolewa kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na 12. Kwa hiyo, umiliki wa leseni hii hukoma tarehe 30 Juni ya kila mwaka. Mmiliki wa leseni anaweza kuomba kusasisha leseni yake mwezi mmoja kabla ya kumalizika kwa muda wake wa awali.

Chanzo: Sheria ya Madini, 2015

3.8.1.1 Leseni za Madini

Sehemu ya II ya Sheria ya Madini ya mwaka 2018, inatoa kanuni za jumla za kutoa na kuhamisha haki za umiliki wa leseni za madini katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

i. Utoaji wa Leseni za Madini

Nchini Tanzania, kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 2018, utoaji wa leseni za madini unafanyika kwa kufuata njia kuu mbili. Njia ya kwanza ni "wa kwanza kuomba wa kwanza kupata," ambapo mwombaji anatakiwa kuchagua eneo la madini analotaka na kuomba umiliki kutoka kwa Mamlaka ya Leseni kuititia rejista ya umma ya madini. Endapo mwombaji atatimiza vigezo na masharti yaliyowekwa katika sehemu ya IV na V ya sheria hii atapewa leseni ya eneo hilo. Utaratibu wa "wa kwanza kuomba wa kwanza kupata" unaweza kukosa ufanisi ikiwa waombaji wawili au zaidi watawasilisha maombi ya kumiliki eneo moja la madini kwa wakati mmoja. Katika hali kama hii, waombaji watajulishwa, na Mamlaka ya Leseni itatangaza zabuni ambapo waombaji hawa wanapaswa kushindana kwa kuwasilisha zabuni. Mamlaka ya Leseni itachagua

mzabuni ambaye ana utaalam bora wa kiufundi na uwezo wa rasilimali fedha. Jedwali namba 19 linaonesha vigezo vya utalaam wa kiufundi na kifedha vinavyotumiwa na Mamlaka ya Leseni kutoa leseni za madini.

Jedwali Na. 19: Mahitaji na Vigezo vya Kutoa Leseni za Madini

Na.	Vigezo vya Utalaam wa Kiufundi	Vigezo vya Rasilimali Fedha
1	Kuwasilisha data za kiasi cha madini kilichopo	Kwa leseni ya madini uwezo wa uwekezaji kati ya Dola za Kimarekani 100,000 hadi 100,000,000 kulingana na ukubwa wa shughuli za uchimbaji. Kwa Leseni Maalum ya Madini (SML) mahitaji ya chini ya uwekezaji ni Dola za Kimarekani 100,000,000
2	Programu na Mpango ya uchimbaji wa madini	
3	Mahitaji ya miundombinu inayohitajika	
4	Ripoti na cheti cha tathimini ya athari ya mazingira.	

Chanzo: Wizara ya Madini

Njia ya pili ya utoaji leseni za madini ni kupitia mchakato wa zabuni za wazi. Kwa kuzingatia masilahi ya umma, Waziri anaweza kukaribisha maombi ya leseni za utafutaji wa madini, uchimbaji madini, au leseni maalum za madini kupitia Gazeti la Serikali au gazeti la kila siku. Waombaji watawasilisha zabuni, na Mamlaka ya Leseni itatathmini zabuni zinazoshindana na kumchagua mzabuni ambaye anaonesha anaweza kukuza kwa haraka maendeleo ya eneo la amdin na pia iwe yenye kuleta faida ya rasilimali za eneo hilo. Vigezo vikuu vya kuchagua mzabuni katika njia hii ni utaalam wa kiufundi na rasilimali fedha, mpango uliopendekezwa, na matumizi au mtaji ambao mwombaji amepanga kutumia, na uzoefu wa awali wa mwombaji katika kufanya shughuli za uchimbaji madini. Hata hivyo, katika mwaka huu wa fedha, hakukuwa na leseni yoyote ya madini iliyotolewa kwa kupitia mchakato wa zabuni za wazi kwani hakuna kampuni ambazo zilizoomba leseni za madini za eneo moja.

Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Madini ilitoa jumla ya leseni 7,093.³³ Jedwali namba 20 linaonesha aina na idadi za leseni zilizotolewa kwa wamiliki kwa mwaka huu wa fedha.

Jedwali Na. 20: Leseni za Madini Zilizotolewa Mwaka 2016/17

Na.	Aina ya Leseni	2016/17
1	Leseni ya Utafutaji	359
2	Leseni Maalum ya Madini	0
3	Leseni ya Madini	18
4	Leseni ya Awali ya Uchimbaji Madini	6,716
5	Leseni ya Udalali wa Madini	0
6	Leseni ya Uuzaji Madini	0
7	Leseni ya Uyeyushaji Madini	0
	Jumla	7,093

Chanzo: Tume ya Madini

³³ <http://www.teiti.go.tz/storage/app/uploads/public/5e0/b34/fa8/5e0b34fa835fa138381948.pdf>
<http://www.teiti.go.tz/storage/app/uploads/public/5e0/b34/551/5e0b34551b839840599810.pdf>
<http://www.teiti.go.tz/storage/app/uploads/public/5e0/b4e/afc/5e0b4eafc63ca507322221.pdf>

ii. Uhamishaji wa Leseni za Madini

Sheria inaruhusu uhamishaji wa leseni za madini kutoka mtu mwenye umiliki wa leseni kwenda kwa mwininge. Pamoja na hili, sheria inaeelekeza kwamba haki zote za madini kwa leseni maalum ya madini na leseni ya madini haziwezi kuhamishwa bila idhini ya Mamlaka ya leseni. Katika uhamishaji wa leseni, Mamlaka Ya Leseni itamtathmini mwombaji kulingana na uwezo wake wa utalaam wa kiufundi na rasilimali fedha. Kwa upande wa utalaam wa kiufundi, mwombaji lazima awasilishe ripoti ya maendeleo ya eneo la madini aliloomba leseni na athibitishe uwezo wake wa kuchimba madini. Vigezo vya rasilimali fedha vinavyotumika kuhamisha leseni za madini ni sawa na vile vinavyotumika kutoa leseni. Jedwali namba 21 vigezo vinavyotumika kuhamisha leseni kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwininge.

Jedwali Na. 21: Vigezo vya Kuhamisha Umiliki wa Leseni za Madini

Na.	Vigezo vya Utalaam wa Kiufundi	Vigezo vya Rasilimali Fedha
1	Kuwasilisha data za kiasi cha madini kilichopo	
2	Programu na Mpango ya uchimbaji wa madini	
3	Mahitaji ya miundombinu inayohitajika	
4	Ripoti na cheti cha tathimini ya athari ya mazingira.	Kwa leseni ya madini uwezo wa uwekezaji kati ya Dola za Kimarekani 100,000 hadi 100,000,000 kulingana na ukubwa wa shughuli za uchimbaji. Kwa Leseni Maalum ya Madini (SML) mahitaji ya chini ya uwekezaji ni Dola za Kimarekani 100,000,000

Chanzo: Wizara ya Madini

Katika mwaka wa fedha 2016/17, Mamlaka ya Leseni ilihamisha jumla ya leseni 480 kama inavyoonekana katika Jedwali namba 22.

Jedwali Na. 22: Leseni za Madini Zilizohamishwa Mwaka 2016/17

Na.	Aina ya Leseni	2016/17
1	Leseni ya Utafutaji	63
2	Leseni Maalum ya Madini	0
3	Leseni ya Madini	18
4	Leseni ya Awali ya Uchimbaji Madini	399
5	Leseni ya Udalali wa Madini	0
6	Leseni ya Uuzaji Madini	0
7	Leseni ya Uyeyushaji Madini	0
Jumla		480

Chanzo: Tume ya Madini

Taratibu hizi za utoaji au kuhamisha leseni za madini huzingatiwa kuwa ni bora na zenye ufanisi kwani zinaendeshwa kwa njia ya uwazi. Taratibu hizi zinapunguza uwezekano wa vitendo vya rushwa na upendeleo katika kutoa au kuhamisha leseni kwa sababu maombi yote yanapita katika mfumo wa wazi wa uombaji leseni za madini (Mining Cadastre). Kwa kuongezea, kitu kingine kizuri kuhusu mfumo huu ni kuwa unaruhusu waombaji leseni kukata rufaa ikiwa hajaridhika na mchakato mzima na maamuzi yaliofanyika wakati wa kutoa au kuhamisha leseni ya madini kwa mtu mwininge au taasisi. Wizara ya Madini imetua taratibu na mahitaji ambayo mwombaji

atahitajika kutimiza na kuyafata wakati wa uombaji wa leseni ya madini. Mahitaji na utaratatibu wa utoaji na uhamishaji wa leseni za madini unatofautiana kutokana na aina ya leseni inayoombwa.³⁴ Rejista ya madini inatoa taarifa zote kuhusu leseni za madini zilizohamishwa, zilizotolewa, na kufutwa na Mamlaka ya Leseni.³⁵

iii. Kusitishwa na Kufutwa kwa Leseni za Madini

Sehemu ya 63 (1) ya Sheria ya Madini ya mwaka 2018 inatoa taratibu na masharti ambayo yanaweza kusababisha kusitishwa au kufutwa kwa leseni za madini. Mamlaka ya leseni inaweza kusitisha au kufuta leseni ikiwa mmiliki atashindwa kufuata sheria, kanuni, au masharti mengine yaliyokubaliwa wakati wa utoaji wa leseni. Hata hivyo, katika kuhakikisha haki inatendeka, mamlaka haipaswi kusitisha au kufuta leseni za madini isipokuwa ikiwa imeandika kwa maandishi kwa mwenye leseni ikielezea sababu za kusitishwa au kufutwa kwa leseni. Vilevile, Sehemu ya 65 ya sheria hii inatoa nafasi kwa wamiliki wa leseni za madini kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa kusitishiwa au kufutiwa leseni zao. Mmiliki wa leseni ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka ya Leseni anaweza kuomba Mahakama Kuu kuitia shauri lake la rufaa ndani ya siku sitini (60) kutoka tarehe ya uamuzi wa kusitishwa au kufutwa kwa leseni yake.

3.8.1.2 Rejista ya Leseni za Madini

Sehemu ya III ya Sheria ya Madini ya mwaka 2018, inahitaji Mamlaka ya Leseni kutunza cadastre ya madini. Cadastre ya Madini inapokea na kushughulikia maombi ya leseni za madini na pia inaonesha ramani ya maeneo ya madini kwa umma na rejista ya madini. Rejista inaruhusu waombaji na wamiliki wa leseni halali (Aina ya A, B, C, na D) kusasisha, kuachilia, kusitisha, na kufanya malipo yanayohusiana na leseni kuititia njia ya mtandao. Uwezo wa kuona taarifa zilizopo kwenye cadastre ya madini umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni kwa matumizi ya umma ambapo kila mtu anaweza kuona taarifa zilizopo kwenye cadastre. Sehemu ya pili ni waombaji wa leseni ambaa watahitajika kuititia mchakato mrefu wa usajili ili kuweza kuomba na kuona baadhi ya taarifa zilizopo ndani ya cadastre tofauti na zile zinazofikiwa na umma. Kusudi la kuweka mchakato mrefu ni kuhakiki taarifa zao kabla hawajapewa ruhusa ya kuingia kwenye mfumo huu. Kwa matumizi ya umma, Cadastre ya Madini inapatikana kwa njia ya mtandao na inaweza kuonwa na kila mtu.³⁶ Baadhi ya taarifa muhimu ambazo zinaweza kupatikana katika cadastre hii ni pamoja na nambari ya leseni, mmiliki wake, tarehe aliyoomba na aliyopewa, tarehe ya kumalizika muda wa leseni, aina za madini na maeneo ya madini yaliyotolewa na Mamlaka za Madini kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji madini.

³⁴ <https://www.madini.go.tz/wp-content/uploads/2017/12/procedures-for-applying-for-mineral-rights-in-tanzania.pdf>.

³⁵ <https://portal.madini.go.tz/site/CustomHtml.aspx?PageID=d7f3f61d-4689-4280-a59a-b865f002dd60>.

³⁶ <https://portal.madini.go.tz/site/CustomHtml.aspx?PageID=d7f3f61d-4689-4280-a59a-b865f002dd60>.

3.8.2 Utoaji wa Leseni za Mafuta

Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, inasimamia utoaji na uhamishaji wa umiliki wa leseni za mafuta na gesi nchini. Sheria hii inasimamia shughuli zote za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuna aina mbalimbali za leseni za mafuta na gesi zinazoweza kutolewa nchini kama inavyooneshwa kwenye Jedwali namba 23.

Jedwali Na. 23: Aina za Leseni za Mafuta na Gesi

Na.	Aina ya Leseni	Maelezo
1	Leseni ya Utafutaji	Leseni za Utafutaji hutolewa kwa Kampuni ya Taifa ya Mafuta kwa ajili ya kufanya shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Kampuni ya Taifa ya Mafuta inaweza kuomba kwa Waziri ili ipewe leseni hii kwa kitalu chochote. Maombi hayatakiwi kuzidi vitalu 40. Muda wa leseni ya utafutaji ni miaka minne kutoka tarehe ambayo leseni imetolewa. Mmiliki wa leseni ya utafutaji anaweza kuomba kuongezewa muda wa uhai wa leseni kwa kitalu chochote ndani ya eneo la utafutaji wa mafuta na gesi asilia. Leseni ya Utafutaji mafuta na gesi asilia inaweza kuongezewa muda kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu katika awamu ya kwanza na sio zaidi ya miaka miwili katika awamu ya pili ya kusasisha leseni hiyo. Waziri anaweza, baada ya kupokea ushauri kutoka kwa Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta kutoa au kukataa nyongeza ya muda wa uhai wa leseni kwa sababu ya masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Sehemu ya 59 ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.
2	Leseni ya Uchimbaji	Leseni ya Uchimbaji hutolewa kwa wamiliki wa leseni halali za utafutaji mafuta wa vitalu ambapo mafuta ya petroli yamegunduliwa. "Mmiliki wa leseni ya utafutaji ambaye Leseni yake ipo hai na inatumika katika shughuli za mafuta katika vitalu vinavyojumuisha eneo hilo, anaweza, ndani ya miaka miwili ikiwa ni mafuta ghafi na miaka mitatu ikiwa ni gesi asilia kutoka tarehe ambayo vitalu vilitangazwa kutolewa au kipindi kingine ambacho Waziri ataruhusu, atawasilisha ombi la leseni ya uchimbaji kwa vitalu ambavyo vina hifadhi au sehemu ya hifadhi ya mafuta." Leseni ya uchimbaji inaweza kuongezewa muda mara moja tu. Maombi ya kuongezewa muda yanapaswa kuwasilishwa miezi 12 kabla ya kumalizika kwa muda wa leseni ya awali. Waziri, kwa kushauriwa na Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta, anaweza kutoa au kukataa kutoa leseni ya maendeleo kutokana na hali fulani kama inavyoolekezwa na Sehemu ya 75 ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.

Chanzo: Sheria ya Mafuta, 2015

3.8.2.1 Leseni za Mafuta na Gesi Asilia

Sehemu ndogo ya II ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 inatoa taratibu za utoaji na uhamishaji wa leseni za mafuta na gesi asilia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

i. Utoaji wa Leseni za Mafuta na Gesi Asilia

Chini ya Sehemu ndogo ya II ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, Waziri anayehusika na Nishati baada ya kupokea ushauri kutoka kwa Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta ana mamlaka ya kutoa au kukataa kutoa leseni za mafuta na gesi. Haki zote za kipekee kwa shughuli za mafuta na gesi asilia ya petroli hutolewa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na haziwezi kuhamishiwa kwa mtu mwingine yeyote. Hata hivyo, kupata haki hizi, Shirika lazima litume maombi kwa Waziri wa Nishati, ambapo Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta itatathmini maombi kulingana na Sehemu ndogo ya II ya sheria. Sheria pia inairuhusu Shirika, kwa idhini ya Waziri, kushirikiana na taasisi nyingine za kitanzania au kigeni inaweza kuomba kitalu cha mafuta kupidia mchakato wa zabuni ya wazi na ushindani au kupatiwa kitalu husika moja kwa moja. Katika mashirikiano haya, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania litashikilia faida ya kushiriki isiyopungua 25% isipokuwa kama itaamuliwa vinginevyo. Pia, sheria inahitaji kwamba kampuni yoyote inayotaka kufanya shughuli za mafuta nchini Tanzania nje ya eneo la kibali cha utafiti itafanya hivyo pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Kampuni hiyo itastahili kushirikiana na Shirika ikiwa imesajiliwa kama kampuni chini ya sheria ya makampuni au sheria nyingine yoyote, na kampuni hiyo itambulisse uwezo wake katika nyanja za utalaam na rasilimali fedha.

Sheria inaruhusu waombaji wawili au zaidi kuingia makubaliano ya ushirikiano katika shughuli za mafuta na gesi. Makubaliano hayo yanatakiwa kuwasilishwa kwa Waziri wa Nishati kama sharti mojawapo la kuingia makubaliano hayo. Halafu, Waziri anaweza, baada ya kupokea ushauri kutoka kwa Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta na kwa niaba ya serikali, kuingia makubaliano na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na washirika wake. Hata hivyo, Waziri atafanya hivyo baada ya kupata idhini kutoka kwa baraza la mawaziri. Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta itaandaa Mkataba wa Faida ya Kushiriki Uzalishaji kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na washirika wake na kuuwasilisha kwa Waziri ambaye baadaye ataupeleka kwa baraza la mawaziri ili kupata idhini. Baraza la mawaziri litaidhinisha mikataba hiyo. Baada ya hapo, mikataba iliyoidhinishwa itakuwa mwongozo wa makubaliano yote yatakayofuata.

Kulingana na sheria hii, makubaliano yote ya shughuli za mafuta hayataanza kutumika isipokuwa yamepitia mchakato wa zabuni ya umma iliyo wazi na yenye ushindani. Waziri lazima atoe mwaliko wa zabuni au nia ya kuanzisha mazungumzo ya moja kwa moja. Endapo sehemu nzima au sehemu ya eneo lililopewa zabuni kupidia mchakato wa ushindani wa zabuni ya umma haujafanya kazi, na ni kwa masilahi ya umma, basi, waziri kwa ushauri aliopewa na Mamlaka ya Udhitibi ya Uchimbaji wa Mafuta, na kwa idhini ya baraza la mawaziri, anaweza kuanzisha mazungumzo ya moja kwa moja na taasisi iliyotimiza vigezo vya kisheria. Kanuni zinampa waziri mamlaka ya jinsi ya kuendesha mchakato wa zabuni. Kwa kuongezea, Waziri anaweza kutangaza vitalu fulani kutengwa kwa masilahi ya umma au kupewa moja kwa moja kwa Shirika la

Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa ilani iliyochapishwa kwenye Gazeti la serikali. Hakuna utoaji wa leseni wa vitalu vyote vilivyoifadhiwa utakaofanyika isipokuwa kama uhifadhi huo umerekebishwa au kubatilishwa na Waziri kupitia Gazeti la serikali.³⁷

Mchakato wa utoaji zabuni za wazi ni njia kuu ya kutoa leseni za mafuta na gesi katika eneo la wazi. Jedwali namba 24 linaonesha masharti ambayo lazima yatimizwe kwa taasisi kuweza kufikiriwa wakati wa mchakato wa utoaji leseni za mafuta.

Jedwali Na. 24: Vigezo na Utaratibu wa Utoaji Leseni za Mafuta na Gesi Asilia

Na.	Aina ya Leseni	Vigezo
1	Leseni ya Utafutaji Mafuta	Mwombaji awasilishe pendekizo la mpango kazi na kiasi cha chini cha rasilimali fedha atakachotumia katika kitalu alichochagua kwenye maombi yake.
		Mwombaji awasilishe maelezo ya sifa za kitalamu na kiufundi na uwezo wa wafanyakazi wake wote katika sekta ya mafuta.
		Mwombaji awasilishe maelezo ya sifa za kitalamu na kiufundi na rasilimali alizonazo katika kuwekeza kwenye sekta ya mafuta.
		Mwombaji awasilishe aina ya rasilimali fedha zilizopo, hii inajumuisha mtaji, huduma za mkopo, na dhamana.
		Mwombaji awasilishe pendekizo la mpango wa kuwanufaisha watanzania inayoonesha ushiriki wao katika utoaji wa mafunzo na ajira kwa watanzania.
2	Leseni ya Uchimbaji Mafuta	Leseni hii hutolewa moja kwa moja kwa mmiliki wa leseni ya utafutaji ikiwa atatimiza masharti yaliyowekwa katika sheria na kanuni. Endapo mwombaji hatakuwa na leseni ya utafutaji kwa ajili ya kitalu fulani, anaweza kupewa leseni ya uchimbaji ikiwa atamridhisha Waziri kwamba kitalu hicho kina hifadhi ya mafuta, na hakuna leseni za utafutaji au uchimbaji zilizokwisha tolewa kwa eneo hilo wakati wa maombi.
		Mmiliki wa leseni ya utafutaji anayeomba leseni ya uchimbaji lazima atoe ushahidi kwamba kitalu hicho kina hifadhi ya mafuta au sehemu ya hifadhi ya mafuta.
		Mwombaji awasilishe mpango wa kuendeleza kitalu. Maelekezo zaidi yameainishwa katika Sehemu ya 67 ya Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015.

Chanzo: Sheria ya Mafuta, 2015

Katika mwaka wa fedha 2016/17, Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta haikutoa leseni mpya za mafuta. Kulingana na Mamlaka, hawajafanya duru nyingine ya utoaji wa leseni za mafuta tangu duru ya nne ambayo ilifanyika mwaka 2013. Sababu kadhaa zimekuwa ni chanzo cha Mamlaka kushindwa kuzindua raundi ya tano ya kampeni ya kutoa leseni za mafuta na. Moja ya sababu kuu ni kuyumba kwa bei ya mafuta ambayo imekuwa ikiwakatisha tamaa waombaji kupitia mchakato wa zabuni

³⁷ http://pura.go.tz/sites/default/files/file_manager/PETROLEUM%20ACT%202015.pdf.

ya ushindani. Leseni za miradi yote ya mafuta na gesi asilia inayoendelea nchini zilitolewa katika miaka ya nyuma.

ii. Uhamishaji wa Leseni za Mafuta

Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, hairuhusu uhamishaji wa leseni za kipekee za operesheni ya mafuta iliyopewa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na haiwezi kuhamishiwa kwa mtu mwingine yeyote. Hata hivyo, kifungu cha 85 na 86 cha sheria kinatoa nafasi ya uhamishaji wa leseni za mafuta. Waziri lazima aidhinishe uhamishaji wa masilahi katika leseni. Maombi ya idhini ya uhamisho wa leseni ya Waziri lazima yatosheleze masharti kadhaa. Maombi ya uhamishaji lazima yaoneshe uwezo wa mhamishiwaji leseni katika kutekeleza majukumu ya mhamishaji, cheti cha usajili wa kampuni au cheti cha ufuataji sheria cha mhamishiwaji, na makubaliano ya mhamishiwaji na mhamishaji leseni. Pia, machakato huu unahitaji cheti cha idhini ya ulipaji ushuru kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania, ahadi ya uadilifu na yule anayehamishiwa, na maelezo ya sifa za kitalaam na kiufundi za wafanyakazi wake katika sekta ya mafuta na gesi. Kwa kuongezea, mwombaji anatakiwa kutoa maelezo ya aina ya rasilimali fedha, pamoja na mtaji, huduma za mkopo, na dhamana zinazopatikana. Vilevile, mchakato unamtaka mwombaji atoe maelezo ya rasilimali za kiufundi na kitalaam katika sekta ya mafuta, pendekeso kuhusu jinsi mradi unavyopanga kumfundisha Mtanzania, na mambo mengine ambayo Waziri anaweza kuona kuwa ni muhimu.

Licha ya sheria hiyo kuruhusu uhamishaji wa leseni za mafuta, katika mwaka 2016/17, hakukuwa na leseni zozote zilizohamishwa kutoka kwa taasisi moja kwenda nyingine. Leseni za miradi inayoendelea zilihamishwa miaka ya nyuma. Miradi hii inaripotiwa kama miradi inayoendelea katika ripoti hii.

iii. Ukiukwaji wa Sheria na Kanuni wakati wa Utoaji Leseni za Madini na Mafuta

Nchi wanachama wa EITI wanatakiwa kufichua ukiukwaji wa sheria na kanuni wakati wa utoaji/uhamishaji wa leseni za madini na mafuta. Katika mwaka wa fedha 2016/17, katika kutoa leseni za madini na mafuta, Tume ya Madini na Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta walizingatia na kufuata sheria na kanuni zinazosimamia utoaji na uhamishaji wa leseni za madini na mafuta. Hata hivyo, kulikuwa na ukikukwaji mdogo kuhusu ucheleweshaji wa kuarifu waombaji na umma kuhusu waliokubaliwa au kukataliwa leseni za madini. Kulingana na Kifungu cha 33 (i) cha Sheria ya Madini, ya mwaka 2018, kinaagiza mamlaka ya leseni kutoa taarifa ya kukubali au kukataliwa leseni kwa waombaji ndani ya wiki nne tangu tarehe aliyowasilisha maombi. Mamlaka ilibainisha baadhi ya sababu kama chanzo cha ucheleweshaji huo. Pamoja na mambo mengine, masuala ambayo yalikwamisha taarifa hizo ni mchakato wa kurekebisha Sheria ya Madini ya mwaka 2017 na kanuni zake, kuhamishwa kwa ofisi za Wizara ya Madini kutoka Dar es Salaam kwenda mji mkuu Dodoma, na mchakato wa kuanzisha Tume ya Madini ambayo ilirithi shughuli nyingi za utoaji leseni ambazo hapo awali

zilifanywa na Wizara ya Madini. Hakukuwa na upotovu wowote wa sheria na kanuni kuhusu utoaji na uhamishaji wa leseni za mafuta kwani Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta haikutoa leseni yoyote za mafuta na gesi katika mwaka wa fedha 2016/17.

iv. Kusalimisha, Kufuta, na Kusimamisha Leseni za Mafuta

Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, inamruhusu mwenye leseni yoyote anayetaka kusalimisha kitalu chochote anaweza kufanya hivyo kwa kuomba kwa Waziri. Waziri atatoa hati ya kusalimisha kitalu ikiwa mwombaji ametimiza masharti yote. Waziri atafanya hivyo baada ya kushauriwa na Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta. Cheti cha kusalimisha leseni ya mafuta na gesi hakitatolewa kwa mmiliki wa leseni ambaye ana makosa mbalimbali. Kusalimisha kitalu chochote hakutaathiri dhima yoyote iliyopatikana kabla ya usalimishaji haujaanza. Kwa upande wa ufutwaji na usimamishwaji wa leseni za mafuta na gesi, Waziri anaweza kusimamisha au kufuta haki hizo ikiwa mmiliki wa leseni amekosea. Waziri ataendelea mbele na mchakato wa kusimamisha au kufuta leseni baada ya kumpa mwenye leseni taarifa kwa maandishi inayoonesha nia hiyo. Kifungu cha 83 cha sheria kinatoa maelezo zaidi juu ya mazingira ambayo yanaweza kumlazimisha Waziri kufuta leseni za mafuta na gesi.

3.8.2.2 Rejista ya Leseni za Mafuta

Katika uhamishaji na taarifa za usajili wa leseni za mafuta na gesi, Sehemu ya 84 (1) - (6) ya Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 imeamuru Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta kuanzisha na kutunza usajili wa makubaliano ya uzalishaji wa mafuta na gesi, leseni, vibali vya idhini, na mabadiliko yoyote ya masilahi ya makubaliano kuhusu mafuta yaliyopo, idhini, au leseni. Rejista itakuwa na taarifa kuhusu leseni, kibali, au makubaliano ya mafuta na gesi, pamoja na maombi ya misaada, kazi, usasishaji, usalimishaji, ukomeshwaji, na ufutwaji wa leseni. Sheria inataka Rejista kuwa na taarifa kuhusu maamuzi ya mahakama, pamoja na usuluhishi, tuzo, hati au hati zinazohusiana na leseni. Sheria inataka taarifa zilizopo kwenye Rejista ya mafuta kupatikana kwa umma isipokuwa ikielekezwa vinginevyo na sheria. Mtu ye yoyote anaweza kuomba kupata taarifa zilizopo kwenye Rejista ya Mafuta. Kama ilivyo sasa, Mamlaka ya Udhibiti ya Uchimbaji wa Mafuta imetoa taarifa zinazohusu mafuta na gesi asilia kuititia ramani ya shughuli za mafuta.³⁸ Kwa sasa, kama inavyotakiwa na Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, Mamlaka iko kwenye utaratibu wa kuanzisha Rejista kuu ya mafuta.

3.9 Uwazi katika Mikataba ya Sekta ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia

Uwazi wa mikataba wa sekta ya madini, mafuta na gesi asilia ni muhimu sana kwa manufaa ya umma. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko mbioni kuanzisha chombo kitachosaidia uwekaji wazi mikataba (kama inavyohitajika katika Viwango vya EITI vya mwaka 2019). Viwango hivi vinahitaji kuwekwa wazi kwa

³⁸ https://www.pura.go.tz/sites/default/files/file_manager/Activity%20Map%2C%20September%20-%202019.pdf.

kandarasi yoyote ilioingiwa, iliyotolewa au kufanyiwa marekebisho kuanzia Januari 2021. Kuanzia sasa, Wizara ya Madini inataka kuanza kuchapisha mikataba yote ya madini iliyosainiwa kati ya kampuni za madini na serikali. Mchakato wa kuunda chombo ambacho kitachapisha mikataba hii unaendelea. Kwasasa, serikali inakagua na kujadili juu ya makubaliano na mikataba mbalimbali kama inavyotakiwa na kifungu cha 4 na 6 cha Sheria ya Mali na Mikataba ya Asili (Kupitia na Kujadili upya kwa Sheria za Masharti Yasiyo ya kifikra) ya 2017. Kufuatia upitiasi upya wa mikataba hii, imekubaliwa kusubiri kupata idhini kabla ya kuanza kuchapisha mikataba hiyo.

3.10 Taratibu za Ukaguzi na Uhakikisho

3.10.1 Makampuni ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia

Sheria ya Makampuni inataka kila mwaka makampuni kuteua mkaguzi wa nje anayetambuliwa kwa ajili kufanya ukaguzi wa hesabu za kampuni au taarifa za kifedha. Wakaguzi wa nje hutumia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi vilivyotolewa na Bodi ya Viwango ya Ukaguzi na Uhakikisho ya Kimataifa wakati wa ukaguzi. Baadaye, hesabu za kampuni au taarifa za kifedha zilizokaguliwa zinawasilishwa katika mukutano mkuu wa mwaka wa kampuni kwa ajili ya kupitishwa.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 1, 2016 hadi Juni 30, 2017 taasisi 25 zilizohusishwa katika ripoti hii, taarifa zao zilikuwa zimesainiwa na wakaguzi wa nje, ambao walikagua taarifa zao za kifedha. Mashirika 13 yanayoripoti yaliwasilisha fomu zao za kutolea taarifa ambazo hazikusainiwa na wakaguzi wao wa nje.

• Taasisi za Serikali

Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2010 inazitaka Taasisi zote za Umma kuandaa taarifa zao za kila mwaka za kifedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma na kuziwasilisha kwa ukaguzi wa nje.

Ukaguzi wa nje wa Taasisi za Umma unafanya kulingana na matakwa yaliyotolewa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 na Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Tanzania inayoongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina jukumu la kisheria la kufanya ukaguzi wa nje kwa taasisi zote za uma. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi na Taasisi Kuu za Ukaguzi za Afrika. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hutumia Viwango vya Kimataifa vilivyotolewa na taasisi za kimataifa.

Taasisi za Umma kila mwaka wa fedha zinahitajika kuwasilisha taarifa zao za kifedha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, yaani kabla au Tarehe 30 Septemba. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atafanya ukaguzi na mwishowe atatoa barua ya taarifa ya ukaguzi na maoni ndani ya miezi tisa baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha (yaani kabla au tarehe 31 Machi kila mwaka).

Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huandaa aina mbili za ripoti, Moja, ripoti ya binafsi inayotolewa kwa taasisi za umma husika (na maoni ya mkaguzi na barua ya kina ya taarifa ya ukaguzi) na mbili, ripoti Kuu ya mwaka inayohusiana na serikali kuu, mashirika ya umma na mamlaka za serikali za mitaa. Ripoti kuu ya mwaka inatoa habari iliyofupishwa kuhusu mamlaka ya ukaguzi, lengo, wigo, mbinu na viwango vinavyotumika; maoni ya ukaguzi; kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita; muhtasari wa masuala ya ukaguzi juu ya taarifa za kifedha za taasisi za umma na hitimisho la jumla na mapendekezo. Ripoti kuu ya mwaka ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na ripoti ya kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 zinapatikana kwenye wavuti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.³⁹

Hesabu au taarifa za kifedha za taasisi zote ambazo ziliripoti mapato na malipo ambayo yamefanyika katika kipindi cha ripoti cha 2016/17 yalikaguliwa na Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kuongezea, kama ilivyoainishwa katika Sheria ya TEITA ya mwaka 2015, Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana jukumu la kuchunguza endapo tofauti inayobakia baada ya zoezi la ulinganishi wa mapato na malipo ni zaidi ya asilimia moja ya makusanyo yote ya serikali katika ripoti za TEITI.

³⁹ www.nao.go.tz/CAG general reports.

4 UAMUZI WA WIGO WA ULINGANISHI

Kamati ya TEITI iliridhia kuwa wigo wa ulinganishi ujumuishhe taarifa za malipo ya makampuni zilizowasilishwa na taasisi za serikali kwa Mlinganishi Huru.

4.1 Aina za Mapato

Ili kufahamu mtiririko wa malipo Mlinganishi Huru aliwasiliana na taasisi za serikali ambazo zimepokea malipo kutoka katika makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia. Pia, Mlinganishi Huru amezingatia sheria na Ripoti za awali za TEITI kutambua aina za malipo katika sekta ya madini, mafuta na gesi asilia.

4.1.1 Wizara ya Madini

Jedwali namba 25 linaonesha ada na malipo yanayolipwa na kampuni za madini, mafuta na gesi asilia na wachimbaji wadogo kwa Wizara ya Madini. Ada na malipo yaliyolipwa kwa wizara yalijumuishwa katika wigo wa ulinganishi.

Jedwali Na. 25: Aina ya Ada na Malipo yanayolipwa kwa Wizara ya Madini

Aina ya Malipo	Kiasi (TZS)	Asilimia
Mrabaha	162,161,752,993.07	89.31
Kodi ya Pango ya Mwaka	15,372,499,581.79	8.47
Ada ya Jiolojia	3,091,375,181.84	1.70
Malipo Mengineyo	629,238,244.61	0.35
Hati ya Zabuni	122,527,729.80	0.07
Ada ya Maombi	74,701,271.04	0.04
Ada ya Uhamisho	72,950,460.00	0.04
Ada ya Maandalizi	13,263,720.00	0.01
Faini	11,392,722.17	0.01
Ada ya Kusalimisha	8,842,480.00	0.00
Kibali cha uuzaaji bidhaa nje	5,745,550.00	0.00
Kibali cha uingizaji bidhaa ndani ya nchi	3,758,054.00	0.00
Ada ya Kutafuta	1,326,372.00	0.00
JUMLA	181,569,374,360.32	100.0

4.1.2 Mamlaka ya Mapato Tanzania

Jedwali namba 26 linaonesha aina za kodi na ada zilizolipwa na makampuni ya madini, mafuta na gesi asilia kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Jedwali Na. 26: Aina ya Kodi na Ada zilizolipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania

Aina ya Malipo	Kiasi (TZS)	Asilimia
Kodi ya Ongezeko la Thamani	237,677,839,045.00	30.81
Kodi ya Kampuni	167,931,591,352.30	21.77
Kodi ya Mapato ya Ajira	133,716,212,174.64	17.34
Kodi ya Zui	102,058,859,992.66	13.23
Ushuru wa Forodha	30,876,156,455.00	4.00

Aina ya Malipo	Kiasi (TZS)	Asilimia
Ushuru wa Bidhaa	26,804,491,027.41	3.47
Kodi ya Kuendeleza Ufundu Stadi	25,677,278,692.34	3.33
Ushuru wa mafuta ya Taa, Gesi na Spiriti	18,719,370,844.00	2.43
Tozo ya kuendeleza Reli	14,008,025,755.00	1.82
Ushuru wa mafuta	7,926,049,443.00	1.03
Ada ya mchakato wa forodha	4,749,902,137.00	0.62
Ushuru wa Mapato Binafsi	1,061,424,045.62	0.14
Ada ya usajili wa chombo cha moto	141,370,000.00	0.02
Tozo la Biashara Zanzibar	9,644,446.00	0.00
Faini za kodi	1,650,000.00	0.00
Viwango vya kodi kwa wafanyabiashara wadogo wakazi	383,400.00	0.00
JUMLA	771,360,248,809.97	100.00

4.1.3 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania hukusanya mikondo kadhaa ya mapato kutoka kwa makampuni ya mafuta na gesi asilia. Shirika limeidhinishwa chini ya Sehemu ya 6 ya Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015 kukusanya mapato yasiyo ya kodi kama vile mrabaha, mapato ya gesi iliyotengwa kwa kazi maalum, mapato ya ziada ya gesi, faida kwa mujibu wa Mikataba ya Makubaliano ya Uzalishaji, bonasi za saini na ada ya mafunzo. Jedwali namba 27 linaonesha aina za ada zilizolipwa na makampuni ya mafuta na gesi asilia kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Jedwali Na. 27: Aina ya Ada zilizolipwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Aina ya Malipo	Kiasi (TZS)	Asilimia
Mrabaha katika Mafuta na Gesi Asilia	22,120,306,239.66	82.50
Tozo ya Mafunzo	3,230,003,922.30	12.05
Tozo ya Leseni	1,462,860,397.24	5.46
JUMLA	26,813,170,559.20	100.00

4.1.4 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inatoa mamlaka kwa serikali za mitaa kuitisha sheria ndogo za kutoza na kukusanya ushuru wa ndani, tozo, na ada ndani ya maeneo yao. Kulingana na sheria hiyo, kampuni za madini, mafuta, na gesi asilia zinalazimika kulipa ushuru wa huduma hadi asilimia 0.3 ya mapato ya kila mwaka kwa serikali za mitaa zilizopo kwenye maeneo ya miradi yao.

4.1.5 Wizara ya Fedha na Mipango

Wizara ya Fedha na Mipango hupokea gawio kutoka kwa mashirika yanayomilikiwa na serikali na mapato yaliyopatikana kutoka kwa uuzaji wa hisa za kampuni ambazo serikali ina masilahi. Katika mwaka wa fedha 2016/17 mapato haya yalijumuishwa katika ulinganishi

4.1.6 Wizara ya Maliasili na Utalii

Wizara ya Maliasili na Utali hupoke ada ya usimamizi wa misitu kutoka kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kupitia Wakala wa Huduma ya Misitu Tanzania kama sehemu ya usimamizi wa misitu na maliasili. Mapato haya yalijumuishwa katika ulinganishi wa mwaka wa fedha 2016/17.

4.1.7 Malipo ya Kijamii na Mengineyo

Malipo ya kijamii na mengine yanajumuisha michango yote inayotolewa na kampuni za madini, mafuta na gesi katika kukuza maendeleo ya ndani na kufadhili miradi ya kijamii. Michango hii hutolewa kwa fedha taslimu au kwa njia nyingine. Michango hii hupelekwa kwenye za elimu, afya, mazingira, usambazaji wa maji ya kunywa, misaada ya kibinadamu, huduma za maendeleo ya biashara ndogo, miundombinu na nyinginezo.

Kulingana na Kifungu cha 105 (1) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2018, mmiliki wa halali wa leseni ya madini anatakiwa aandae mpango wa kuaminika wa uwajibikaji wa kijamii kila mwaka. Mpango huo lazima uliokubaliwa na mamlaka husika ya serikali za mitaa kwa kushauriana na Waziri anayehusika na mamlaka za serikali za mitaa na Waziri anayehusika na Fedha. Makampuni yanapaswa kuwajibika katika shughuli za mazingira, kijamii, kiuchumi, na kitamaduni kulingana na vipaumbele vya mamlaka ya serikali za mitaa ya jamii husika. Kwa mwaka wa fedha 2016/17 malipo ya kijamii hayakulinganishwa.

4.1.8 Mchango wa Serikali katika Uzalishaji na Mapato yasiyo ya Kifedha

i. Mafuta na Gesi Asilia

Kulikuwa na Mikataba ya Ushirikiano ya Uzalishaji 13 ya mafuta na gesi asilia na Leseni mbili za uzalishaji katika mwaka wa fedha 2016/17.⁴⁰ Kwa hiyo, hakuna malipo ya kifedha yaliyofanyika katika sekta ya mafuta na gesi asilia kama ilivyoripotiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Sheria ya mafuta ya mwaka 2015 inatoa mipangilio ya ushiriki wa uzalishaji. Katika tukio la kuanza uzalishaji wa mafuta na gesi asilia, kampuni italipa mrabaha kwa kiwango cha asilimia 12.5 katika maeneo ya pwani ya bahari na asilimia 7.5 katika maeneo ya ndani ya bahari.⁴¹

ii. Madini

Kwa mwaka wa fedha 2016/17 utafiti wa wigo wa ulinganishi ulionesha kutokuwepo kwa mapato haukugundua yasiyo ya kifedha katika sekta ya madini. Kwa mwaka wa fedha 2016/17, Hilo lilithibitishwa kwa maandishi na Shirika la Taifa la Madini.

⁴⁰ <http://www.teiti.go.tz/storage/app/uploads/public/5e0/b07/e9a/5e0b07e9af5bd943977987.pdf>

⁴¹ <http://www.tpdc.co.tz/wp-content/uploads/2016/02/SHERIA-PETROLEUM-ACT-2015-Updated-version-15-6.pdf>

4.1.9 Taratibu za Kubadilishana Bidhaa kwa Bidhaa

Kwa mujibu wa viwango vya EITI, nchi mwanachama anapaswa kuripoti kama serikali taratibu na makubaliano ya kubadilishana bidhaa za madini, mafuta na gesi asilia dhidi ya bidhaa au huduma kama mikopo, misaada, na miundombinu. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Mlinganishi huru hakuona uwepo wa taratibu na makubaliano yaliyowekwa na serikali ili kufanikisha ubadilinishanaji wa bidhaa za madini, mafuta na gesi asilia dhidi ya bidhaa au huduma kama mikopo, misaada, na miundombinu.

4.1.10 Malipo Mengine Makubwa

Fomu ya kutolea taarifa ilijumuisha takwa la nyongeza la kuripoti malipo mengine yoyote makubwa yaliyokusanywa au yaliyolipwa katika mwaka wa fedha 2016/17 na hayakujumuishwa katika fomu.

4.1.11 Aina ya Mapato yaliyoingizwa katika Ulinganishi

Mtiririko wa aina ya mapato yaliyoingizwa kwenye zoezi la ulinganishaji ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali namba 28.

Jedwali Na. 28: Mtiririko wa Mapato kwa Zoezi la Ulinganishaji

Aina Ya Malipo	
Mrabaha katika Madini	Tozo ya kuendeleza Reli
Kodi ya Pango ya Mwaka	Ushuru wa mafuta
Ada ya Jiolojia	Ada ya mchakato wa forodha
Kodi ya Kampuni	Mrabaha katika Mafuta na Gesi Asilia
Ushuru wa Forodha	Tozo ya Mafunzo
Ushuru wa Bidhaa	Tozo ya Leseni
Kodi ya Kuendeleza Ufundu Stadi	Ushuru wa huduma
Ushuru wa mafuta ya Taa, Gesi na Spiriti	Ada nyingine za ushuru wa ndani na tozo

4.2 Makampuni ya Madini, Mafuta na Gesi Asilia

Serikali katika mwaka wa fedha 2016/17 ilipokea jumla ya TZS bilioni 980 kutoka makampuni 7,324 ikijumuisha ambayo hayakuhusikia moja kwa moja kwenye sekta ya madini, mafuta na gesi asilia. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lilipokea malipo kutoka kwa kampuni tisa kutoka sekta ya mafuta na gesi asilia. Makampuni mengine yalilipa malipo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania au Wizara ya Madini. Jedwali namba 29 linatoa picha ya malipo yaliyopokelewa na Serikali kupitia taasisi hizo.

Jedwali Na. 29: Malipo yaliyofanywa na Makampuni

Kiwango cha Ulipaji	Idadi ya makampuni	Mapato yaliyokusanywa (TZS bilion)
Kiasi > TZS 1 bilioni	64	929
TZS 500 milioni < Kiasi < TZS 1 billion	33	21
TZS 100 milioni < Kiasi < 500 milioni	82	16
TZS 50 milioni < Kiasi < 100 milioni	56	4
TZS 10 milioni < Kiasi < 50 milioni	186	4

Kiwango cha Ulipaji	Idadi ya makampuni	Mapato yaliyokusanywa (TZS bilion)
Kiasi <10 milioni	6,903	6
JUMLA	7,324	980

Kulingana na mapato yaliyopokelewa serikalini kwa mwaka wa fedha 2016/17, Kamati ya TEITI ilikubaliana kuwa kampuni zote zilizolipa kuanzia TZS milioni 900 zihusishwe katika zoezi la ulinganishia. Kwa hiyo, mchango wa makampuni yaliyoingia kwenye ulinganishi ulikuwa ni asilimia 95.52 ya mapato yote yaliyokusanywa kutoka sekta ya madini, mafuta na gesi asilia.

Jedwali Na. 30: Kampuni zilizoingia kwenye Ulinganishi 2016/2017

Na.	JINA LA KAMPUNI	MALIPO YALIYOKUSANYWA NA MAMILAKA YA MAPATO TANZANIA	MALIPO YALIYOKUSANYWA NA SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA	MALIPO YALIYOKUSANYWA NA WIZARA YA MADINI	JUMLA YA MALIPO YALIYOKUSANYWA	ASILIMIA
KAMPUNI						
1	GEITA GOLD MINING LIMITED	227,831,124,365.86		46,299,151,900.53	274,130,276,266.39	27.96
2	NORTH MARA GOLD MINE LIMITED	85,182,691,464.40		33,572,737,956.21	118,755,429,420.61	12.11
3	BULYANHULU GOLD MINE LIMITED	74,778,740,691.13		261,351,071.60	75,040,091,762.73	7.65
4	PAN AFRICAN ENERGY TANZANIA LIMITED	72,802,731,912.66	291,787,951.71		73,094,519,864.37	7.45
5	PANGEA MINERALS LTD	48,433,604,318.29		4,458,820.54	48,438,063,138.83	4.94
6	M&P EXPLORATION PRODUCTION TANZANIA LIMITED	25,829,769,847.44	21,522,208,306.33		47,351,978,153.77	4.83
7	SHANTA MINING COMPANY LIMITED	24,672,213,720.90		9,647,886,670.34	34,320,100,391.24	3.50
8	AUMS (T) LIMITED	25,048,989,872.88			25,048,989,872.88	2.55
9	SHELL EXPLORATION AND PRODUCTION TANZANIA LIMITED	17,567,247,496.66	1,077,887,604.45		18,645,135,101.11	1.90
10	WILLIAMSON DIAMONDS LTD.	13,516,091,062.12		100,000.00	13,516,191,062.12	1.38
11	HANIENDA GROUP LTD	-		11,680,973,860.00	11,680,973,860.00	1.19
12	NDOVU RESOURCES LIMITED.	7,628,808,535.42	1,674,653,557.73		9,303,462,093.15	0.95
13	POA POA COMPANY LTD	-		7,888,221,950.00	7,888,221,950.00	0.80
14	AFRICAN EXPLOSIVES (T) LTD.	7,200,101,874.47			7,200,101,874.47	0.73
15	EQUINOR TANZANIA AS	7,060,045,736.48			7,060,045,736.48	0.72
16	PANAFRICAN MINING SERVICES (TANZANIA) LIMITED.	7,008,004,568.99			7,008,004,568.99	0.71
17	JOSIA MASANJA & PTNS	-		6,139,672,240.00	6,139,672,240.00	0.63
18	MANTRA TANZANIA LIMITED.	3,885,388,463.55		2,199,474,053.96	6,084,862,517.51	0.62
19	SAHARA TANZANIA LIMITED	6,070,986,760.08			6,070,986,760.08	0.62
20	NYAMIGOGO	-		5,768,731,180.00	5,768,731,180.00	0.59
21	TANCOAL ENERGY LIMITED	4,305,834,190.46		1,074,125,211.39	5,379,959,401.85	0.55
22	OPHIR TANZANIA (BLOCK 1) LIMITED	5,248,810,766.41			5,248,810,766.41	0.54
23	TANZANITE ONE MINING LTD	4,016,109,628.00		882,663,707.50	4,898,773,335.50	0.50
24	AROBOGAST SILILO LULILA LIMITED	90,392,866.89		4,696,379,154.00	4,786,772,020.89	0.49
25	GLOBELEQ TANZANIA SERVICES LIMITED	4,736,743,921.61			4,736,743,921.61	0.48
26	ALLEN DIESELS LTD (UK)	4,208,183,903.86			4,208,183,903.86	0.43
27	GODFREY MITTI & PTNS	-		4,186,825,522.00	4,186,825,522.00	0.43
28	ALMAN GOLD CO. LIMITED	1,700,000.00		4,126,969,444.00	4,128,669,444.00	0.42
29	ENOCK LYAMBA & PTNS	-		3,524,315,404.00	3,524,315,404.00	0.36
30	NITRO EXPLOSIVES (T) LTD.	3,389,275,881.76			3,389,275,881.76	0.35
31	SAMAX RESOURCES LTD.	3,373,569,191.46			3,373,569,191.46	0.34
32	AL MUTHAAB TRADING & CO. LTD	-		2,825,784,222.00	2,825,784,222.00	0.29
33	MINDINGO MBARAKA MINDINGO	-		2,713,017,430.00	2,713,017,430.00	0.28
34	GSM PETROLEUM LIMITED	2,448,528,054.00			2,448,528,054.00	0.25
35	KAKOLA MINING COMPANY LIMITED	2,370,295,154.94			2,370,295,154.94	0.24
36	ABEL KAPENE	-		2,210,620,000.00	2,210,620,000.00	0.23
37	MINERAL OIL CORPORATION LIMITED	2,187,257,707.84			2,187,257,707.84	0.22

Na.	JINA LA KAMPUNI	MALIPO YALIYOKUSANYWA NA MAMILAKA YA MAPATO TANZANIA	MALIPO YALIYOKUSANYWA NA SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA	MALIPO YALIYOKUSANYWA NA WIZARA YA MADINI	JUMLA YA MALIPO YALIYOKUSANYWA	ASILIMIA
38	CATA MINING COMPANY LIMITED	1,505,795,266.73		547,530,553.33	2,053,325,820.06	0.21
39	PETER BUJASHI			2,048,139,044.00	2,048,139,044.00	0.21
40	KASUBUYA PLANT	-		1,986,798,570.00	1,986,798,570.00	0.20
41	RAS AL KHAIMAH GAS TANZANIA LTD.	1,981,907,864.98			1,981,907,864.98	0.20
42	JAC RIJK AFRICA LIMITED	1,720,610,289.90			1,720,610,289.90	0.18
43	ISACK MAYUNGA	-		1,628,342,692.00	1,628,342,692.00	0.17
44	ORECORP TANZANIA LIMITED	1,600,894,221.90		2,433,073.00	1,603,327,294.90	0.16
45	CHINA PETROLEUM TECHNOLOGY AND DEVELOPMENT CORPORATION	1,520,775,272.64			1,520,775,272.64	0.16
46	SEA SALT LIMITED	1,332,266,886.30		60,302,789.80	1,392,569,676.10	0.14
47	WAKEREKETWA MINING SACCOS	-		1,384,348,920.00	1,384,348,920.00	0.14
48	DODSAL HYDROCARBONS & POWER (TANZANIA) PVT LTD.	900,156,884.74	426,970,105.36	42,952,536.07	1,370,079,526.17	0.14
49	EVEN ENTERPRISES COMPANY LIMITED	1,366,958,819.50		160,000.00	1,367,118,819.50	0.14
50	CHINA PETROLEUM PIPELINE BUREAU (CPP)	1,326,577,404.77			1,326,577,404.77	0.14
51	KABANGA NICKEL COMPANY LIMITED	345,193,495.50		894,418,389.00	1,239,611,884.50	0.13
52	LOOTAH BC GAS LLC	1,218,231,526.36			1,218,231,526.36	0.12
53	MBOGO MINING AND GENERAL SUPPLY LIMITED	1,199,248,893.85		6,183,764.00	1,205,432,657.85	0.12
54	SUNSHINE MINING LIMITED	1,194,101,613.14		573,976.00	1,194,675,589.14	0.12
55	PETROBRAS TANZANIA LIMITED	1,135,565,254.30			1,135,565,254.30	0.12
56	BUSOLWA MINING LIMITED	518,882,218.63		598,533,750.82	1,117,415,869.45	0.11
57	KUSINI GATEWAY INDUSTRIAL PARK LIMITED	82,422,207.92		1,001,468,936.00	1,083,891,143.92	0.11
58	TRYPHONE AYOUB	-		1,077,617,630.00	1,077,617,630.00	0.11
59	BEARING MAN GROUP TANZANIA LIMITED	1,073,089,880.42			1,073,089,880.42	0.11
60	KATAVI MINING COMPANY LIMITED	1,023,753,846.35		20,184,014.53	1,043,937,860.88	0.11
61	EXXONMOBIL EXPLORATION AND PRODUCTION TANZANIA LIMITED	1,027,584,217.22			1,027,584,217.22	0.10
62	HERITAGE RUKWA (TZ) LIMITED	106,908,177.63	915,334,113.47		1,022,242,291.10	0.10
63	DIOMOND RAHIM KARMAI (MR)	999,701,228.00			999,701,228.00	0.10
64	ERONT PROCESSING	-		995,450,162.00	995,450,162.00	0.10
65	TNR LIMITED	986,637,291.07			986,637,291.07	0.10
66	ZEM (T) CO. LIMITED	931,349,648.51		29,444,614.14	960,794,262.65	0.10
67	ALLY SHARIF & PTNS	-		959,582,680.00	959,582,680.00	0.10
68	HENAN AFRO-ASIA GEO-ENGINEERING (TANZANIA) CO. LTD.	929,944,902.00			929,944,902.00	0.09
69	ABG EXPLORATION LIMITED	769,992,990.89		136,704,953.80	906,697,944.69	0.09
JUMLA NDOGO		717,691,792,261.81	25,908,841,639.05	163,124,630,846.56	906,725,264,747.42	92.46
MASHIRIKA YANAYOMILIKIWA NA SERIKALI						
70	SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA	28,547,457,111.98	-	400,000.00	28,547,857,111.98	2.91
71	STAMIGOLD COMPANY LIMITED	186,665,019.00	-	1,038,281,783.66	1,224,946,802.66	0.12
72	SHIRIKA LA TAIFA LA MADINI	257,317,312.40	-			0.03
JUMLA NDOGO		28,991,439,443.38	-	1,038,681,783.66	29,772,803,914.64	3.06
WIGO WA ULINGANISHI		746,683,231,705.19	25,908,841,639.05	164,163,312,630.22	936,498,068,662.06	95.52
73	MAKAMPUNI MENGINE AMBAYO HAYAJAINGIA KWENYE WIGO WA ULINGANISHI	24,934,284,417.18	904,328,920.15	17,982,870,021.12	44,078,807,948.85	4.48
JUMLA KUU		771,617,516,122.37	26,813,170,559.20	182,146,182,651.34	980,576,876,610.91	100.00

4.3 Wigo wa Ulinganishi

Aina 37 za mapato, makampuni 70 ya madini, mafuta na gesi asilia, na taasisi 26 za serikali ziliingizwa kwenye zoezi la ulinganishi la mwaka 2016/17 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Namba 31, 32, 33 na 34.

Jedwali Na. 31:Maelezo ya Mtiririko wa Kodi na Malipo kwa Serikali

Na.	Aina ya Mapato	Maelezo	
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA			
1	Kodi ya Kampuni	Kodi ya Mapato ya kampuni inatozwa kwenye shughuli zilizosajiliwa na/au zinazofanywa nchini Tanzania. Kiwango cha kodi ya mapato ya kampuni kinachotumika ni asilimia 30 ambayo kwa kawaida hulipwa katika hatua mbili. Kodi ya muda inalipwa kutokana na makadirio mwanzoni mwa mwaka wa biashara. Kodi ya mwisho hulipwa baada ya tathmini rasmi mapato ya jumla katika mwaka husika wa mapato.	
2	Ushuru wa bidhaa	Ushuru unaotozwa kwenye bidhaa na huduma mahususi zinazotengenezwa ndani au kuingizwa nchini pamoja na magari katika viwango mbalimbali. Ushuru unapaswa na unalipwa na mwingizaji bidhaa kama ni bidhaa zinazoingizwa mara moja kabla kusitishwa kuingia kwenye udhibiti wa forodha. Kama ni bidhaa zilizotengenezwa ndani ya nchi, unalipwa na mtengenezaji wa bidhaa, wakati kodi inapofikia kulipwa.	
3	Ushuru wa Forodha	Ushuru wa Forodha unatozwa kwenye bidhaa mahususi zinazoingizwa nchini Tanzania.	
4	Tozo ya Kuendeleza Ufundji Stadi	Kodi inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania chini ya Sheria ya Mafunzo ya Elimu ya Ufundji na Sheria ya Kodi ya Mapato. Tozo inatozwa kwa kuzingatia malipo ghafi ya malipo yote yanayolipwa na mwajiri kwa mwajiriwa. Tofauti na Kodi ya Mapato, Tozo hii inatokana na kulipwa na mwajiri	
5	Ushuru wa mafuta ya Taa, Gesi na Spiriti	Ushuru unatozwa kwenye mafuta ya petroli, dizeli, na mafuta ya taa	
6	Tozo ya kuendeleza Reli	Tozo ya kuendeleza Reli ni tozo ya maendeleo ya miundombinu ya asilimia 1.5 kwa uagizaji bidhaa. Tozo hii inatozwa kulingana na thamani ya forodha kwa bidhaa zilizoingizwa kwa matumizi ya Tanzania Bara. Tozo hii haitumiki kwa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ambazo zina unafuu au msamaha chini ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2004, bidhaa zinazosafiri, bidhaa za dawa, n.k.	
7	Ushuru wa Mafuta	Ushuru wa mafuta unatozwa kutokana na bidhaa za petroli zinazoingizwa nchini ambazo ni petroli na gasoil.	
8	Ada ya mchakato wa forodha	Ada hii inatozwa kwa Kampuni za madini, mafuta na gesi asilia kwa ukaguzi wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje bila kujali thamani yake.	
SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA			
9	Mrabaha katika Mafuta na Gesi Asilia	Mrabaha kutoka kwenye uzalishaji wa mafuta na gesi unalipwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kama ilivyoelekezwa kwenye sehemu ya 113 ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015. Mrabaha unatozwa kulingana na eneo uzalishaji unapofanyika. Mrabaha kwa uzalishaji unaofanywa kwenye eneo la pwani ya bahari ni asilimia 12.5 na kwenye eneo la ndani ya bahari ni asilimia 7.5. Kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 na muongozo wa makubaliano ya ushirikiano kwenye uzalishaji wa mafuta na gesi, mrabaha utalipwa kutoka kwenye uzalishaji ghafi kabla kiwango kilichozaishwa hakijagawanywa kwa wabia.	

Na.	Aina ya Mapato	Maelezo
10	Tozo ya Mafunzo	Makampuni yanayofanya kazi kwenye sekta ya mafuta na gesi hulipa kiasi cha dola za kimarekani 500,000 kama ada ya mafunzo na utafiti kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kama mchango wa kuendeleza utaalamu wa sekta ya mafuta na gesi
11	Tozo ya Leseni	Ni ada inayolipwa kwa maombi ya kufanya shughuli za mafuta na gesi katika maeneo yaliyoruhusiwa.
WIZARA YA MADINI		
12	Mrabaha	Haya ni malipo anayopewa mmiliki wa rasilimali. Hii ni kulingana na kifungu cha 113 cha Sheria ya Petroli, 2015.
13	Kodi ya Pango	Kodi ya pango ya mwaka
14	Ada ya Leseni	Ada ya leseni
15	Ada ya Maombi	Ada ya maombi ya leseni
16	Faini	Malipo yanayolipwa na mwenye leseni ya madini pale anapochelewesha malipo kama vile mrabaha, kodi ya pango n.k.
17	Kibali cha uuzaaji bidhaa nje	Malipo yanayolipwa kupata kibali cha kusafirisha sampuli na madini
19	Kibali cha uingizaji bidhaa ndani ya nnchi	Malipo yanayolipwa kupata kibali cha kuingiza sampuli na madini ndani ya nchi.
MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA		
19	Ushuru wa huduma	Ushuru wa huduma wa hadi asilimia 0.3 ni gharama za makampuni ya biashara yaliyomo ndani ya mipaka ya nchi (unaolipwa ama kwa kila mwezi au kila baada ya robo mwaka kutegemeana na mahitaji ya kila mamlaka ya mtaa)

Jedwali Na. 32: Kampuni zilizoingia katika zoezi la Ulingenishaji

NA. KAMPUNI	NA. KAMPUNI
1 GEITA GOLD MINING LIMITED	36 ABEL KAPENE
2 NORTH MARA GOLD MINE LIMITED	37 SUNSHINE MINING LIMITED
3 BULYANHULU GOLD MINE LIMITED	38 MINERAL OIL CORPORATION LIMITED
4 PAN AFRICAN ENERGY TANZANIA LIMITED	39 CATA MINING COMPANY LIMITED
5 PANGEA MINERALS LTD	40 PETRO BUJASHI
6 M&P EXPLORATION PRODUCTION TANZANIA LIMITED	41 KASUBUYA PLANT
7 SHANTA MINING COMPANY LIMITED	42 RAS AL KHAIMAH GAS TANZANIA LTD.
8 AUMS (T) LIMITED	43 SEA SALT LIMITED
9 SHELL EXPLORATION AND PRODUCTION TANZANIA LIMITED	44 JAC RIJK AFRICA LIMITED
10 WILLIAMSON DIAMONDS LTD.	45 ISACK MAYUNGA
11 HANCIENDA GROUP LTD	46 ORECORP TANZANIA LIMITED
12 NDOVU RESOURCES LIMITED.	47 EVEN ENTERPRISES COMPANY LIMITED
13 POA POA COMPANY LTD	48 CHINA PETROLEUM TECHNOLOGY AND DEVELOPMENT CORPORATION
14 AFRICAN EXPLOSIVES (T) LTD.	49 WAKEREKETWA MINING SACCOS
15 EQUINOR TANZANIA AS	50 DODSAL HYDROCARBONS & POWER (TANZANIA) LTD.

NA.	KAMPUNI	NA.	KAMPUNI
16	PANAFRICAN MINING SERVICES (TANZANIA) LIMITED.	51	CHINA PETROLEUM PIPELINE BUREAU (CPP)
17	JOSIA MASANJA & PTNS	52	KABANGA NICKEL COMPANY LIMITED
18	MANTRA TANZANIA LIMITED.	53	LOOTAH BC GAS LLC
19	SAHARA TANZANIA LIMITED	54	MOBOGO MINING AND GENERAL SUPPLY LIMITED
20	NYAMIGOGO	55	BUSOLWA MINING LIMITED
21	TANCOAL ENERGY LIMITED	56	PETROBRAS TANZANIA LIMITED
22	OPHIR TANZANIA (BLOCK 1) LIMITED	57	TRYPHONE AYOUB
23	TANZANITE ONE MINING LTD	58	BEARING MAN GROUP TANZANIA LIMITED
24	AROBOGAST SILILO LULILA LIMITED	59	EXXONMOBIL EXPLORATION AND PRODUCTION TANZANIA LIMITED
25	GLOBELEQ TANZANIA SERVICES LIMITED	60	KATAVI MINING COMPANY LIMITED
26	GODFREY MITTI & PTNS	61	HERITAGE RUKWA (TZ) LIMITED
27	ALLEN DIESELS LTD (UK)	62	ERONT PROCESSING
28	ALMAN GOLD CO. LIMITED	63	HENAN AFRO-ASIA GEO-ENGINEERING (TANZANIA) CO. LTD.
29	ENOCK LYAMBA & PTNS	64	KUSINI GATEWAY INDUSTRIAL
30	NITRO EXPLOSIVES (T) LTD.	65	DIOMOND RAHIM KARMALI (MR)
31	SAMAX RESOURCES LTD.	66	TNR LIMITED
32	AL MUTHAAB TRADING & CO. LTD	67	ZEM (T) CO. LIMITED
33	MINDINGO MBARAKA MINDINGO	68	ALLY SHARIF & PTNS
34	GSM PETROLEUM LIMITED	69	ABG EXPLORATION LIMITED
35	KAKOLA MINING COMPANY LIMITED		

Jedwali Na. 33: Mashirika Yanayomilikiwa na Serikali

Mashirika Yanayomilikiwa na Serikali

1	SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA
2	SHIRIKA LA TAIFA LA MADINI
3	STAMIGOLD COMPANY LIMITED

Jedwali Na. 34: Taasisi za Serikali

WIZARA NA TAASISI ZA SERIKALI

1	WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO	3	WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
2	WIZARA YA MADINI	4	MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
5	SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLITANZANIA		

MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

5	HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA	15	HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA
6	HALMASHAURI YA MJI WA GEITA	16	HALMASHAURI YA MJI YA KAHAMA
7	HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO	17	HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA
8	HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA	18	HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA
9	HALMASHAURI YA WILAYA YA SONGWE	19	HALMASHAURI YA WILAYA YA MTWARA
10	HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO	20	HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME
11	HALMASHAURI YA WILAYA YA KINONDONI	21	HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA
12	HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU	22	HALMASHAURI YA WILAYA YA KISHAPU
13	HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO	23	HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO
14	HALMASHAURI YA WILAYA YA CHALINZE		

Kati ya kampuni 72 zilizochaguliwa kushiriki zoezi la ulinganishaji, Mlinganishi huru aliweza kuwasiliana na kuzipatia fomu za ukusanyaji wa taarifa kampuni 53. Kati ya Kampuni hizi zilizopatiwa fomu za ukusanyaji wa taarifa ni kampuni 41 tu zilirejesha fomu zilizojazwa. Mchango wa kampuni hizi 41 ni 88.78% ya mapato ya serikali kutoka kwenye sekta ya madini, mafuta na gesi asilia kwa mwaka wa fedha 2016/17. Jedwali namba 35 linaonesha orodha ya kampuni zilizorejesha fomu na kiasi kilichopokelewa na taasisis za serikali.

Jedwali Na. 35: Kampuni zilizorejesha Fomu kwa Mwaka 2016/2017 (TZS Milioni)

Na.	Jina La Kampuni	Malipo Yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania	Malipo Yaliyokusanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	Malipo Yaliyokusanywa na Wizara ya Madini	Jumla ya Malipo Yaliyokusanywa	Asilimia
KAMPUNI ZA MADINI						
1	GEITA GOLD MINING LIMITED	227,831		46,299	274,130	27.96
2	NORTH MARA GOLD MINE LIMITED	85,182		33,572	118,755	12.11
3	BULYANHULU GOLD MINE LIMITED	74,778		261	75,040	7.65
4	PAN AFRICAN ENERGY TANZANIA LIMITED	72,802	291		73,094	7.45
5	PANGEA MINERALS LTD	48,433		4	48,438	4.94
6	M&P EXPLORATION PRODUCTION TANZANIA LIMITED	25,829	21,522		47,351	4.83
7	SHANTA MINING COMPANY LIMITED	24,672		9,647	34,320	3.50
8	AUMS (T) LIMITED	25,048			25,048	2.55
9	SHELL EXPLORATION AND PRODUCTION TANZANIA LIMITED	17,567	1,077		18,645	1.90
10	WILLIAMSON DIAMONDS LTD.	13,516		0.1	13,516	1.38
11	HANCIENDA GROUP LTD	-		11,680	11,680	1.19
12	NDOVU RESOURCES LIMITED.	7,628	1,674		9,303	0.95
13	POA POA COMPANY LTD	-		7,888	7,888	0.80
14	AFRICAN EXPLOSIVES (T) LTD.	7,200			7,200	0.73
15	EQUINOR TANZANIA AS	7,060			7,060	0.72
16	PANAFRICAN MINING SERVICES (TANZANIA) LIMITED.	7,008			7,008	0.71
17	JOSIA MASANJA & PTNS	-		6,139	6,139	0.63
18	MANTRA TANZANIA LIMITED.	3,885		2,199	6,084	0.62
19	NYAMIGOGO	-		5,768	5,768	0.59
20	TANCOAL ENERGY LIMITED	4,305		1,074	5,379	0.55
21	OPHIR TANZANIA (BLOCK 1) LIMITED	5,248			5,248	0.54
22	AROBOGAST SILILO LULILA LIMITED	90		4,696	4,786	0.49
23	GLOBELEQ TANZANIA SERVICES LIMITED	4,736			4,736	0.48
24	GODFREY MITTI & PTNS	-		4,186	4,186	0.43
25	NITRO EXPLOSIVES (T) LTD.	3,389			3,389	0.35
26	RAS AL KHAIMAH GAS TANZANIA LTD.	1,981			1,981	0.20
27	JAC RIJK AFRICA LIMITED	1,720			1,720	0.18
28	ORECORP TANZANIA LIMITED	1,600		2	1,603	0.16
29	SEA SALT LIMITED	1,332		60	1,392	0.14
30	DODSAL HYDROCARBONS & POWER (TANZANIA) PVT LTD.	900	426	42	1,370	0.14
31	KABANGA NICKEL COMPANY LIMITED	345		894	1,239	0.13

Na.	Jina La Kampuni	Malipo Yaliyokusanya na Mamlaka ya Mapato Tanzania	Malipo Yaliyokusanya na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania	Malipo Yaliyokusanya na Wizara ya Madini	Jumla ya Malipo Yaliyokusanya	Asilimia
32	MBOGO MINING AND GENERAL SUPPLY LIMITED	1,199		6	1,205	0.12
33	BUSOLWA MINING LIMITED	518		598	1,117	0.11
34	BEARING MAN GROUP TANZANIA LIMITED	1,073			1,073	0.11
35	KATAVI MINING COMPANY LIMITED	1,023		20	1,043	0.11
36	TNR LIMITED	986			986	0.10
37	HENAN AFRO-ASIA GEO-ENGINEERING (TANZANIA) CO. LTD.	929			929	0.09
38	ABG EXPLORATION LIMITED	769		136	906	0.09
MASHIRIKA YANAYOMILIKIWA NA SERIKALI						
39	SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA	28,547	-	0.4	28,547	2.91
40	STAMIGOLD COMPANY LIMITED	18	-	1,038	1,224	0.12
41	SHIRIKA LA TAIFA LA MADINI	257	-			0.03
JUMLA		709,404	24,990	136,210	870,526	88.78

